

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA PILI

**Kikao cha Saba – Tarehe 10 Februari, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatazo iliwasilishwa mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Taarifa ya Mwaka ya Benki Kuu ya Tanzania kwa Mwaka 2019/2020 (*The Annual Report of Bank of Tanzania for the year 2019/2020*).

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha Mapitio ya Nusu Mwaka, 2020/2021 (*Monitory Policy Statement: The Mid - Year Review 2020/2021*).

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Katibu.

## **NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI**

### **MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rarya, sasa aulize swali lake.

Na. 88

#### **Daraja la Mto Mori – Rarya**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja la Mto Mori kwani mto huo umekuwa ukisomba watu na kusababisha vifo kwa wananchi wanaofuata huduma upande wa pili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rarya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mto Mori unakatisha katika barabara ya Kirogo-Nyamaguku yenye urefu wa kilomita 15, ikiunganisha Tarafa za Luo-imbo, Suba na Nyancha katika Wilaya ya Rarya. Barabara hii ilifunguliwa mwaka 2008 kwa nguvu za wananchi kuitia Mpango wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mto huu umegawanyika katika matawi mawili ambayo ni Mto Mori Mkuu wenye upana wa mita 43 na Wamala wenye upana wa mita 16 ambapo madaraja mawili (2) yanahitajika kujengwa. Hivyo,

kwa sasa, barabara hii haipitiki kutokana na kutokuwepo kwa madaraja hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa barabara hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Rarya imewasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI, maombi maalum ya Shilingi bilioni 1.54 ambayo ni makisio kwa ajili ya ujenzi wa daraja katika Mto Mori na matengenezo ya kawaida katika Barabara ya Nyamaguku- Kirogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali itatenga fedha kuititia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (*TARURA*) kwa ajili ya usanifu wa madaraja mawili ya Mto Mori ili kufahamu mahitaji na gharama halisi za ujenzi wa madaraja hayo na kisha kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi. Aidha, ujenzi wa madaraja na miundombinu ya barabara hizi utatekelezwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na pia kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nataka niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa daraja hili linaunganisha tarafa zaidi ya tatu kwa maana Tarafa ya Suba, Nyancha pamoja na Luo-imbo na ni muhimu sana kwenye uchumi wa muunganiko wa watu wanaoishi ndani ya tarafa hizi.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kuna umuhimu wa kuharakisha daraja hili kwa kuwa si tu linaharakisha uchumi, lakini pia ni sehemu ambayo wananchi wengi wamekuwa wakipoteza maisha wanapovuka kutoka upande mmoja kwenda upande wa pili?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, Mheshimiwa Waziri haoni sasa baada ya Bunge hili, kuna umuhimu sasa wa kuongozana mimi na yeye ili kwenda pamoja kule ndani ya jimbo kuona namna gani tunaweza

tukatatua pamoja changamoto hii ili angalau wananchi hawa waweze kupata huduma hii kwa uharaka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Ranya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba daraja hilo ni muhimu sana kwa kuwa linaunganisha vijiji vingi na tarafa tatu katika Halmashauri ya Ranya na kiungo muhimu sana katika shughuli za kiuchumi na shughuli za kijamii katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoongea katika majibu yangu ya msingi kwamba Serikali inatambua sana umuhimu wa daraja hilo na ndiyo maana katika mwaka wa fedha ujao 2021/2022 Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kufanya tathmini na usanifu ili kutambua shughuli ambayo inahitaji kutekelezwa na gharama za daraja hilo ili kadri ya upatikanaji wa fedha daraja hilo liwezwe kujengwa na kutatua changamoto hizo kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kuambatana na Mheshimiwa Mbunge naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tuko tayari wakati wowote kufika kushirikiana naye Mheshimiwa Mbunge. Baada ya kikao hiki tutapanga tuone ratiba bora zaidi ya kwenda kupita eneo hilo na kuona namna gani tunakwenda kuwashudumia wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Matatizo yalioko katika Daraja la Ranya ni sawa kabisa na matatizo yaliyoko kwenye Jimbo la Geita Vijijiini kwenye Daraja la Blengete, Kata ya Isilobutundwe na tumeshaandika maandiko mengi lakini hatujawahi kupata majibu. Je, Wizara au Waziri yuko tayari sasa baada ya Bunge hili kuongozana nami kwenda kuona ili aone umuhimu wa kutupatia pesa hizo?

**NAIBU SPIKA:** Sasa Waziri sijui ataanzia wapi, ataanzia kwa mwenye swali au ataanzia kwa mwenye swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri unaulizwa kama utaenda jimboni kwa Mheshimiwa Musukuma, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita Vijijiini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameelezea daraja katika eneo hilo ni muhimu sana katika shughuli za kiuchumi za wananchi, lakini pia kwa shughuli za kijamii. Niwapongeze sana akiwemo mwenyewe Mheshimiwa Musukuma kwa jitihada za kufuatilia daraja hilo liweze kujengwa ili wananchi waweze kupata huduma. Naomba nimhakikishie kwamba, kadri ya upatikanaji wa fedha Serikali itaendelea kulipa kipaumbele eneo hilo la daraja na litaanza ujenzi pale bajeti itakapotengwa na fedha itakapopatikana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante Sana. Naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali la nyongeza. Daraja lililopo Jimbo la Moshi Vijijiini ilisombwa na maji mwaka mmoja uliopita na daraja hili ni

muhimu, linaunganisha kata nne katika Jimbo la Moshi Vijijini. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa daraja hili? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua maeneo yote korofi ambayo madaraja yetu kwa namna moja ama nyingine yameathirika na mafuriko kutokana na mvua ambazo zimeendelea kunyesha hapa nchini. Serikali imeweka mkakati wa kwenda kufanya tathmini ya mahitaji katika maeneo hayo korofi ili kulingana na upatikanaji wa fedha, fedha ziweze kutengwa na madaraja hayo yaweze kujengwa au kufanyiwa marekebisho ili kuwezesha wananchi kupata huduma kama Serikali inavyodhamiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Moshi Vijijini kwamba eneo hilo Serikali inalitambua na tutakwenda kadri ya upatikanaji wa fedha kutenga bajeti kwa ajili ya usanifu, lakini pia kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo ili tuweze kurahisisha shughuli kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu kule mnao watendaji wajitahidi kuwaletea taarifa zilizo sahihi. Kuna maeneo mengi ambayo yanakuwa hayana mawasiliano baada ya mvua kupita, imevunja daraja hapa, hata mimi Mbeya liko Mwasanga na Tembela watu hawaendi kabisa, yaani daraja halipo na watu watano walifariki na huu ni msimu mwingine na daraja bado halijajengwa. Sasa ikichukua miaka miwili kuunganisha eneo inakuwa kidogo mtihani.

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee, Mheshimiwa Naibu Waziri ana maswali mengi sana leo. Mheshimiwa Asia

Abdukarim Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 89

**Utekelezaji wa Sheria ya Kutoa Mikopo Asilimia 10  
katika Halmashauri**

**MHE. ASIA A. HALAMGA** aliuliza:-

Ni Halmashauri ngapi nchi zimetekeleza kwa asilimia 100 sheria ya utoaji mikopo asilimia 10 ya makusanyo ya ndani kwa makundi ya vijana, akinamama na watu wenyewe mahitaji maalum?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA  
SERIKALI ZA MITAA (DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Abdukarim Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu zilizopo hali ya utoaji wa mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenyewe Ulemavu katika Halmashauri nchini imeimarika hasa baada ya kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 yaliyofanyika Julai, 2018 kwa kuongeza Kifungu cha 37A kuhusu Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenyewe Ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanza kutumika kwa Sheria hii mwaka wa fedha 2018/2019 na 2019/2020 Halmashauri 79 zimetoa mikopo kwa asilimia 100 na Halmashauri 54 zimetekeleza kwa asilimia zaidi ya 85.

Mheshimwa Naibu Spika, utekelezaji wa shughuli hizi za mikopo umewezesha kuongezeka kwa mikopo inayotolewa na halmashauri nchini ikililinganishwa na kipindi kabla ya kufanya marekebiso ya sheria.

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 (kabla ya marekebiso ya sheria) shilingi bilioni 26.1 zilitolewa; mwaka wa fedha 2018/2019 (baada ya marekebiso ya sheria) shilingi bilioni 42.06 zilitolewa; na mwaka wa fedha 2019/2020 jumla ya mikopo iliyoolewa ilikuwa ni shilingi bilioni 40.7 zilitolewa.

Mheshimwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kifungu namba cha 24(2) cha Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za mwaka 2019, Mkurugenzi yejote ambaye atashindwa kusimamila utekelezaji wa Kanuni hizi atakuwa ametenda kosa la kinidhamu na mamlaka yake ya nidhamu inaweza, kwa kadri itakavyoona inafaa, kumchukulia hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naomba kutoa rai kwa Wakurugenzi wote nchini kote kuhakikisha kwamba wanazingatia takwa hilo la kisheria.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia Abdukarim Halamga swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali tayari Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba halimashauri 85 hazijaweza kutekeleza kwa asilimia mia moja utoaji wa mikopo. Je, Serikali haioni sasa ni wakati wa kuanzishwa kwa benki ya vijana ili iweze kusimamiwa na vijana wenywewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Serikali ina mpango ganijuu ya kuwakopesha vijana mmoja mmoja kwa sababu vijana wengi wanaopewa mikopo hii haiendi kuwanufaisha kwa kuwa mawazo yanakuwa tofauti? Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tumeona tangu kuanzishwa kwa mpango huu wa mikopo asilimia kumi kwa wanawake, vijana na watu wenyewe ulemavu kazi ya ukopeshaji katika ngazi ya halmashauri katika miaka mitatu iliyopita imeongezeka zaidi ya mara tatu. Kwa hivyo, kwa hatua hii bado Serikali inaendelea kutekeleza vizuri, lakini ni kweli kwamba bado kuna changamoto kwenye baadhi ya halmashauri kutokana na uwezo wa ukusanyaji wa mapato na ndiyo maana Serikali imeendelea kusisitiza halmashauri kuboresha vyanzo vyaa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na wazo la Mheshimiwa Mbunge kuanzisha benki ya vijana, naomba tulichukue kama Serikali, tukalifanyie tathmini na kuona njia bora zaidi ya kulitekeleza. Kuhusiana na mikopo ya vijana kwa maana kijana mmoja mmoja, pia ni wazo la Mheshimiwa Mbunge na sisi ni kazi yetu kuchukua mawazo ya Waheshimiwa Wabunge, kuyatathmini, kuyafanya kazi na kuona uwezekano wa kutekeleza hilo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inapokea mawazo hayo na tutakwenda kuyafanya kazi na kuona njia bora zaidi ya kuyatekeleza.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nina swali moja la nyongeza; katika halmashauri zetu zipo *SACCOS* za vijana na wanawake ambazo zimeundwa na wanawake na vijana, lakini *SACCOS* hizo hazikopeshwi kuititia Mifuko ya Halmashauri. Sasa, ni lini Serikali italeta sheria Bungeni ili *SACCOS* hizo za vijana na

wanawake ziweze kukopesheka kupitia Mfuko wa Halmashauri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika naomba kujibu mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika kuhusiana na SACCOS za vijana na wanawake kutokopessa kupitia halmashauri na wazo lake ni lini Serikali italeta sheria ili utaratibu huu uweze kutendeka, naomba nichukue wazo la Mheshimiwa Mbunge, tukalifanyile tathmini kama Serikali na kuona uwezekano wa kutekeleza jambo hili na kuona faida zake na changamoto zake ili tuweze kufanya maamuzi stahiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swalii la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kwa niaba yake Mheshimiwa Innocent Bilakwate.

Na. 90

#### **Matatizo ya Maji - Shirika ya Elimu - Kibaha**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE (K.n.y. MHE. SILVESTRY F. KOKA)** aliuliza:-

Miundombinu ya maji katika Shirika la Elimu Kibaha ilijengwa miaka 50 iliyopita kwa kutumia mabomba ya Asbestos ambayo siyo rafiki kwa afya za binadamu, lakini pia ni chakavu sana:-

(a) Je, ni lini Serikali itatatuwa changamoto ya maji katika shirika hilo?

(b) Je, ni lini Serikali itakarabati majengo ya Chuo cha FDC katika Shirika hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya maji katika Shirika la Elimu Kibaha inayotokana na miundombinu mibovu na ya muda mrefu ambayo ni kutokana na uwepo wa mabomba ya maji ya kipenyo cha milimita 200 yenye urefu wa kilomita nne na kipenyo cha milimita 150 yenye urefu wa kilomita mbili yaliyojengwa kwa *asbestos* tangu kuanzishwa kwa Shirika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali ilikwisheshabadilisha bomba la *asbestos* lenye urefu wa kilomita 0.75 la kipenyo cha milimita 200 na bomba lenye urefu wa kilomita moja na kipenyo cha milimita 150 kuwa PVC. Serikali itaendelea kubadilisha mabomba hayo kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, Shirika linaendelea kufanya matengenezo madogo madogo kwa kutumia mapato ya ndani pindi uharibifu unapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa shirika hili, imekamilisha ukarabati wa Shule ya Sekondari Kibaha kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.6. Vilevile katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imetoea kiasi cha shilingi milioni 80 kwa ajili ya ujenzi wa bweni katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Kibaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya tathmini ya ukarabati wa miundombinu ya majengo ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Shirika la Elimu Kibaha ambapo kiasi cha shilingi billioni 1.48 kinahitajika ili kufanya matengenezo. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati. Hata hivyo, Shirika la Elimu Kibaha lilifanya ukarabati mdogo wa madarasa na jengo la utawala kwa kutumia mapato ya ndani ambao uligharimu shilingi milioni 25.73.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Halmashauri ya Jimbo la Kyerwa, tunalo jengo la halmashauri. Jengo hili limechukua muda mrefu na halijakamilishwa. Nini ahadi ya Serikali kukamilisha lile jengo la halmashauri katika Wilaya ya Kyerwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali ndiyo inayojenga majengo yote ya halmashauri katika nchi yetu likiwemo jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa. Hivyo basi, kutohana na mahitaji na malengo ya Serikali ambayo imojiwekea na bajeti ambayo tumeitenga, tutalikamilisha lile jengo kadri bajeti yetu tulivyojewa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi.

Na. 91

### **Ujenzi wa Daraja la Mto Pangani**

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID** aliuliza:-

Je, ni lini utekelezaji wa ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne ya kujenga Daraja la Mto Pangani mpakani mwa Wilaya za Same na Simanjiro utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais –TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Jimbo la Same Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mto Pangani umekatisha kwenye kipande cha barabara ya Same – Ruvu – Mferejini chenye urefu wa kilomita 34.2. Barabara hiyo inaunganisha Kata za Same na Ruvu katika Wilaya ya Same na sehemu ya mto inayopendekezwa kujengwa daraja ina upana wa mita 70. Sehemu hii haipitiki kwa sasa kutokana na kukosekana kwa daraja la kuunganisha Wilaya ya Same, Mkoa wa Kilimanjaro na Wilaya ya Simanjiro Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais-TAMISEMI kupitia Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (*TARURA*) imekuwa ikikihudumia kipande cha barabara hiyo kwa kufanya matengenezo kwenye maeneo korofu ambapo katika mwaka wa fedha 2018/2019 kiasi cha shilingi milioni 48 kilitumika. Aidha, katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021

kiasi cha shilingi milioni 63 kimetengwa kwa ajili ya matengenezo ambapo kwa sasa mkandarasi anaendelea na matengenezo ya kipande cha kilomita 7.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (*TARURA*) umeponga kufanya usanifu wa daraja ikiwa ni pamoja na kipande cha barabara yenye urefu wa kilomita 34.2 kwa upande wa Same hadi kufikia eneo la Mto Pangani panapohitajika kujengwa daraja ili kuunganisha Wilaya za Same na Simanjiro. Serikali itatoa kipaumbele cha ujenzi wa daraja na miundombinu ya barabara hiyo muhimu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa daraja hili linaunganisha Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Kilimanjaro na hivyo ku-*facilitate* kusafirisha mifugo pamoja na mazao ya kilimo kwenda mikoa mbalimbali kutoka mikoa ya Kati kwenda Kaskazini. Kwa kuwa kuwepo kwa daraja hili kutafupisha safari ya kutoka Kilimajaro kwenda Dodoma kwa kilometra 172. Kwa kuwa fedha zinazotengwa *TARURA* ni ndogo sana na haziwezi zikatosheleza ujenzi wa daraja hili kwa haraka. Je, Serikali, Wizara ya TAMISEMI, haioni kwamba umefika wakati sasa wa kushirikiana na *TANROADS* au Wizara ya Ujenzi kwa sababu imekuwa inafanya hivyo katika *projects* mbalimbali ili kuweza kunusuru wananchi katika maeneo mbalimbali? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa wakati huu ni wakati wa amani na kwa kuwa Jeshi letu la Wananchi limekuwa linafanya kazi nzuri sana ya ujenzi wa miundombinu, je, katika madaraja haya ambayo yametajwa na Waheshimiwa Wabunge asubuhi ya leo pamoja na

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haioni kwamba inaweza kushirikisha Jeshi ili liweze kusaidia kujenga madaraja haya ili wananchi waweze kupita kwa urahisi na shughuli za uchumi zikaendelea vizuri? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Jimbo la Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Daraja hilo la Mto Pangani ni muhimu sana kwa sababu linaunganisha mikoa miwili; Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Kilimanjaro. Ni kweli kwamba bajeti ya kawaida ya kuhudumia Halmashauri ya Same haiwezi kukamilisha ujenzi wa daraja hilo kubwa; na hivyo katika utaratibu wa Serikali kuna ujenzi wa taratibu za kawaida lakini pia kuna ujenzi maalum kwa maana ya kutenga bajeti maalum kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu korofi kama ilivyo daraja hilo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mbinu hizi mbili za matengenezo ya muda wa kawaida kwa maana ya utaratibu wa kawaida na matengenezo maalum hutumika pale ambapo madaraja yanahitaji fedha kiasi kikubwa kuliko bajeti ya halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili *TARURA* tumeendelea kushirikiana kwa karibu sana na *TANROADS* kuona namna bora ya kushirikiana ili daraja hilo liweze kupata suluhu. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ushirikiano huu unaendelea vizuri na tunaamini kwamba katika mwaka wa fedha ujao tutakuwa tumefikia hatua nzuri ya utekelezaji wa ujenzi wa daraja hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la Jeshi kushiriki katika kujenga madaraja hayo, mara nyingi Serikali katika madaraja ambayo yanahitaji ujenzi wa dharura

kutokana na maafa mbalimbali kama mafuriko, sote tumekuwa mashahidi kwamba majeshi yetu yamekuwa yanafika na kufanya matengenezo hayo kwa haraka na kwa wakati ili kurejesha huduma kwa wananchi. Jambo hili litaendelea kutekelezwa kadri ya matukio hayo hayavyojitekeza.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Fredy Mwakibete, swali la nyongeza.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizopo Same Magharibi zinafanana sana na changamoto zilizopo Jimbo la Busokelo. Kata ya Ntaba tuna Daraja ambalo linaitwa Mto Ngubwisia, lilonidolewa na maji tangu tarehe 30 Aprili, 2019 na daraja hili linaunganisha Kata za Kisegese, Itete, Kambasegera pamoja na Luangwa.

Je, ni lini Serikali inakwenda kujenga daraja hili ili wananchi wangu wa Busokelo waunganishwe kama ilivyokuwa zamani? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fredy Makibete, Mbunge wa Busokelo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba daraja hilo muhimu ambalo linaunganisha kata na vijiji mbalimbali katika Jimbo la Busokelo livilunjwa na maji mwaka 2019. Serikali inatambua sana umuhimu wa kwenda kulifanyia tathmini na usanifu daraja hilo ili liweze kutengewa fedha kadri ya upatikanaji wa fedha na kuweza kujengwa ili liweze kurejesha huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kushirikiana na Halmashauri ya Busokelo na Mheshimiwa Mbunge ili kuweza kuona namna gani usanifu unafanyika na fedha zinatafutwa na kujenga daraja hilo kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba kabla barabara hazijajengwa tunatengeneza bajeti, tukishaipitisha ndiyo inaanza kutekelezwa. Wakati mwingine kuna miradi ambayo inatokana na majanga, mfano barabara imekatika ghafla na yenyewe haikuwa imetengewa fedha, lakini kila ukiomba fedha inakuwa ni maneno tu wala hazipatikani.

Sasa nataka kufahamu, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba tunapopata majanga kama madaraja yanapokatika, wa kutoa fedha za dharura ili kuyajenga kuliko hivi ilivyo sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ujenzi wa barabara zetu unatekelezwa kwa mujibu wa bajeti za Serikali. Pia unatekelezwa kwa mujibu wa mapato yanayopatikana kutokana na makusanyo mbalimbali ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu wa kutenga bajeti na kuanda fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo lakini pia utayari wa Serikali kuhudumia majanga pale yanapojitokeza na kukata mawasiliano ni jambo ambalo linapewa kipaumbele sana na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba ni kupata taarifa rasmi kutoka katika jimbo lake kwa hiyo barabara na daraja husika ili wataalam wa *TARURA* katika eneo husika na ngazi ya Wizara tuweze kuona namna ya kufanya thamini na usanifu na kutafuta fedha kwa ajili ya kwenda kufanya ujenzi na marekebisho ya daraja husika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 92

#### **Hitaji la Mawasiliano ya Simu – Mbulu Vijijini**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Je, ni lini minara ya simu itajengwa katika Kata za Endahagichen – Ndamilay, Mewadan – Magong na Endaghadat – Qamtananat katika Jimbo la Mbulu Vijijini ambazo hazina mawasiliano ya simu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** aliujibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile ni siku yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa katika Bunge lako hili tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa kuniamini ili nikatetee na kusimamia llani ya Chama cha Mapinduzi katika Jimbo la Bariadi. Pia naomba niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Bariadi kwa kunichagua kwa kishindo na hakika hawajapoteza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kuniamini na kunituea kuwa msaidizi wake katika Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote pamoja na wadau wengine wa sekta ya mawasiliano ina jukumu la kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo yote ya vijijini na mijini yasiyo na mvuto wa kibiashara. Mpaka sasa jumla ya kata 633 zimekwishapata huduma za mawasiliano nchi nzima ambapo ujenzi unaendelea katika kata zingine 361 kupitia ruzuku ya Serikali. Watoa huduma kwa uwekezaji wao wamefikisha huduma za mawasiliano katika kata 1,692.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tarehe 25 Januari, 2021 tuliwekeana sahihi ya mikataba ya kufikisha huduma za mawasiliano katika kata 59 zenye vijiji 166 katika zabuni ya awamu ya tano. Vilevile mwezi huu tunatarajia kutangaza zabuni nyingine ya awamu ya sita ya kufikisha huduma za mawasiliano katika kata 74 zenye vijiji 206.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) una miradi 15 katika Jimbo la Mbulu Vijijini katika kata 13. Kata zenye miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano ni pamoja na Yaeda Ampa, Yaeda Chini, Maghang, Masieda, Bashay, Eshkesh, Geterer, Gidihim,

Hayderer, Maretadu, Masqaroda, Endamilay, na Tumati. Jumla ya minara 14 imekamilika kujengwa katika kata 12 kati ya minara 15 inayopaswa kujengwa, hii ni sawa na asilimia 87.5 (87.5%) ya utekelezaji wa miradi hiyo. Bado mnara mmoja ambao unatarajiwa kujengwa na Shirika letu la Mawasiliano Tanzania (*TTCL*) ambao utakamilika kabla ya mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jithada hizo za Serikali, bado kuna takribani kata 1,365 kati ya Kata 3,956 zilizopo Tanzania Bara zikiwemo kata za Jimbo la Mbulu Vijijini na wadi 16 kati ya wadi 111 zilizopo Zanzibar ambazo bado zina changamoto ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) inavifanyia tathmini vijiji vingine vyote Tanzania Bara na Visiwani vikiwemo Vijiji ambavyo viko katika Jimbo la Mbulu Vijijini ambavyo ni Endahagichen – Ndamilay, Mewadan – Magong na Endaghadat – Qamtananat, na hatimaye vijiji husika vitaingizwa katika orodha ya vijiji ambavyo vitajumuishwa katika kutangaza zabuni katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Mbulu Vijijini tumepata minara sita ambayo imejengwa. Mwingine umejengwa 2017, mingine inayofuata imejengwa mpaka juzi hapa lakini sasa minara hii sita haifanyi kazi.

Je, Mheshimiwa Waziri ana mpango kuwafuata au kuwaona wakandarasi ili wawashe minara hii sita ambayo sasa wananchi wanaisubiri mpaka leo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, kwa kuwa amesema kata hizi atazipelekea mawasiliano na kujenga minara; je, kata zilizobaki lini zinakwenda kupata hiyo minara ambayo amekwishaisema?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijiini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kulingana na changamoto ambayo ilikuwepo ya masuala ya ujenzi, kata hizo zilikuwa zimechelewa kukamilishiwa miradi hiyo. Hata hivyo, hivi navyoongea wataalam wetu tayari wameshaanza kulifanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba kutumia fursa hii kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna hatua mbili katika ujenzi wa minara; kuna hatua ambayo inatokana na ujenzi wa mnara wenye we ambao tunaita *passive equipment* na hatua ya pili ambayo sasa ni kuweka vile vifaa ambavyo tunaita kwamba ndiyo *active equipment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa hivi tumekutana na changamoto ya wakandarasi wetu ambao walikuwa wamepewa majukumu ya kukamilisha miradi hii kwa sababu wanatumia sana vifaa kutoka nje na mwaka jana tulikumbana na changamoto ya Corona, hivyo tukaona kwamba tuwaongezee muda ili waweze kukamilisha ujenzi wa minara hii. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, suala hili tayari tunalifanya kazi na hizi kata ambazo amezisema tayari wataalam wetu wameshafika *site* kwa ajili ya kujua nini kinafanyika ndani ya muda ambao unatakiwa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swalii la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nami naomba kuuliza Wizara ya Mawasiliano swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa vijiji vitatu katika Kata ya Ziginiali, Kisawasawa na Kiberege havina mawasiliano ya simu kabisa. Je, ni lini Serikali itawasaidia wananchi hawa huduma ya mawasiliano ya simu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nilijibu katika majibu yangu ya msingi, ni kwamba Serikali iko katika mpango wa kufanya tathmini katika Kata nyingine 1,392 ambazo zimebak Tanzania Bara ili tuweze kuona namna gani tutaziingiza katika Mpango wa Utekelezaji katika Bajeti ya 2020/2021. Hivyo namhakikisha Mheshimiwa Mbunge, sambamba na hilo tutahakikisha kwamba tunawasiliana naye kwa ukaribu sana ili kuja changamoto ziko katika maeneo gani ili tuhakikishe kwamba mawasiliano katika Kata hizo yanafika kwa ukamilifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Tatizo liliopo katika Jimbo la Mbulu Vijijini ni sawa kabisa na changamoto iliyoko katika Jimbo la Kalenga. Kata ya Kihanga, Ulanga, Ifunda katika Vijiji vya Mibikimitali na Kata ya Mgama iliyoko katika Vijiji vya Lupembewasenga, kuna changamoto ya mawasiliano.

Je, ni lini sasa Serikali itahakikisha wananchi hao wanapata huduma hiyo ya mawasiliano ili waweze kufanya shughuli zao za kawaida?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto tuliyonayo kwa sasa, labda nitoe maelezo kidogo. Ni kwamba kuna baadhi ya sehemu ambazo mawasiliano au minara ilipelekwa ambapo uhitaji wake inawezekana walikuwa watu 5,000 ambaao walikuwa wanaweza kutumia huduma hiyo. Kwa sababu ya ongezeko la watu katika eneo husika, kwa hiyo, ile minara yetu inashindwa kuwa na uwezo wa kuhudumia watu wengi zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, kwa kugundua hilo, tumeagiza *mobile operator* wote wafanye tathmini, wafanye *research* za kutosha ili waongeze uwekezaji katika maeneo hayo, aidha kwa kuongeza minara au kwa kuongeza *capacity* katika minara ambayo tayari ipo katika maeneo husika ili kuhakikisha kwamba wananchi wote wanafikiwa na mawasiliano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana nami, Naibu Waziri amejibu maswali mengi na leo ni siku yake ya kwanza kabisa kusimama hapa. Kwa hiyo, tumpongeze, amefanya kazi nzuri. (*Makofii*)

Tuendelee na Wizara ya Viwanda na biashara, Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 93

**Kufufua Viwanda vya Kubangua Korosho Mtwara**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafufua viwanda vyote vya kubangua Korosho vilivyopo Manispaa ya Mtwara Mikindani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Kigahe Exaud Silaoneka.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa **Tunza Issa Malapo**, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kabla ya zoezi la Ubinafsishaji, Serikali ilikuwa na jumla ya viwanda 12 vya kubangua korosho nchini. Kati ya viwanda hivyo viwanda viwili vilikuwa katika Manispaa ya Mtwara. Hiki ni kile kilichokuwa kinajullikana kama *Likombe Cashew Factory* na hivi sasa ni *Micronics Systems Company Limited*; na kile kilichokuwa kinaitwa *Mtwara Cashew Company Limited*, sasa hivi ni *Cashew Company (2005) Limited*.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda hivi vyote viwili vinafanya kazi. Kiwanda cha *Micronics Systems Company Limited* kina uwezo uliosimikwa wa kubangua korosho tani 5,000 kwa mwaka. Hata, hivyo kutookana na changamoto ya malighafi kiwanda hicho kinabangua wastani wa tani 2,000 kwa mwaka. Pia Kiwanda cha *Mtwara Cashew Company Limited* kinaendelea na uzalishaji katika kutoa huduma za kupanga madaraja (*grading*) na kufungasha (*packaging*) kwa korosho zinazobanguliwa na viwanda vidogo vilivyopo katika maeneo hayo ambavyo havina mitambo ya *grading* na *packaging*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuvutia uwekezaji na kuwezesha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vipyaa na kufufua viwanda vilivyopo vya kubangua korosho hapa nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, swalii la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba viwanda hivyo viwili anavyovisema, kimoja kinabangua tani 2,000 badala ya tani 5,000 na kingine hakibangui kabisa, kinafanya kufunga. Swali la kwanza; je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha viwanda hivi vinabangua kwa ule uwezo wake? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; katika Manispaa ya Mtwara Mikindani kuna kiwanda kikubwa cha kubangua korosho kinachomilikiwa na Kampuni ya OLAM. Kiwanda hicho kimefungwa. Kiwanda kile kilikuwa kinaajiri wafanyakazi wasiopungua 6,000 wakiwemo wanawake karibu 5,000. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha wanakaa na mwekezaji yule, kiwanda kile kiweze kufanya kazi ili wanawake wa Jimbo la Mtwara Mjini waweze kupata ajira wajikwamue kiuchumi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kabisa kwamba, kama nilivyosema katika jibu la msingi, kuna changamoto ya malighali kwa maana ya korosho ambazo zinahitajika katika viwanda vyetu mbalimbali nya kubangua korosho hapa nchini. Hivyo, kutokana na changamoto hiyo, Serikali kuititia Bodi ya Korosho, tumeandaa mwongozo ambao kwanza tunawapa kipaumbele wabanguaji wa korosho hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuanzia msimu wa 2021 mwongozo huo unataka malighafi zinazopatikana katika mnada wa awali kuititia soko la awali la korosho, viwanda vyote nya ndani ambavyo vinabangua korosho, kwanza vipate korosho, vikishajitosheleza ndiyo sasa tunafungua ule mnada wa pili ambao sasa utahusisha wafanyabiashara

wote ambao wako katika soko la korosho. Hii itapelekea kuhakikisha kwamba viwanda vyote vinavyobangua korosho vinapata malighafi kulingana na mahitaji yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusu Kiwanda cha *OLAM*, ni kweli kiwanda hiki ambacho kilikuwa ni sehemu ya uwekezaji katika Manispaa ya Mikindani, changamoto kubwa iliyosababisha kufungwa kiwanda kile ilikuwa ni kutokana na kukosa malighafi ambazo zilitokana na ushindani wa wanunuzi wa korosho katika minada ambayo inafanyika kwenye maeneo hayo. Ndiyo maana tunapeleka mwongozo huu ambao sasa utahakikisha kwamba viwanda vya kubangua korosho vinapata malighafi kwanza, halafu sasa zile zinazobaki ndiyo zitaingizwa kwenye mnada ambao utajumuisha wafanyabiashara wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali tayari imeshaanza mawasiliano na Kampuni ya *OLAM* ambao waling'oa mitambo ile na kuipeleka nchi jirani Msumbiji ambako wao walikuwa na utaratibu mzuri wa kuhakikisha viwanda vinapata malighafi. Kwa hiyo, sasa tunataka warudi nyumbani kwa sababu nasi tayari tumeshaweka mwongozo huo ambao unawahakikishia malighafi viwanda vyote ambavyo vinabangua korosho hapa nchini. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu unakimbia, maswali ni mengi hapa mbele. Mheshimiwa pale nyuma, tafadhali jitambulisse. Ni Mheshimiwa Mpakate ama! Aah, Mheshimiwa Daimu Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Tunduru tuna Kiwanda cha Kubangua Korosho kilichojengwa miaka ya 1980 ambacho alipewa mwekezaji kwa muda mrefu na mwekezaji yule alikuwa anaendelea kubangua korosho bila kufikisha lengo la makubaliano na Serikali. Kufikilia mwezi Agosti, 2020, kubangua korosho wamesimama kabisa na korosho za Tunduru zinalazimika kununuliwa na kupelekwa nje. Je, kwa nini Serikali haioni haja ya kumnyang'anya mwekezaji yule Kiwanda cha Tunduru

cha Korosho na kupewa mtu mwingine ili uzalishaji wa korosho uendelee? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mpakate kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali ni kuhamasisha uwekezaji wa viwanda mbalimbali hapa nchini ikiwemo viwanda yya kubangua korosho. Ni kweli kiwanda cha kubangua korosho cha Tunduru (*Tunduru Cashew Factory*) ambacho kilinunuliwa na Kampuni ya *Micronics* ambaye amewekeza katika maeneo mengi, bado kuna changamoto kidogo katika ufanyaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyo sema, lengo la Serikali ni kuona tunaendelea kuhamasisha uwekezaji katika viwanda. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mpakate kwamba tutakaa na mwekezaji huyu, tuweze kujadiliana naye, tuone ni changamoto gani ambazo alizipata katika uendeshaji wa kiwanda hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, suala la kumnyang'anya kiwanda litakuwa baada ya kujihakikishia kwamba kweli ameshindwa kutekeleza kuwekeza katika kiwanda hicho halafu tuweze kuona namna bora ya kupata mwekezaji mwingine. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Mheshimiwa Augustine Vuma Holle, Mbunge wa Kasulu Vijijini sasa aulize swalii lake.

Na. 94

**Mgogoro wa Ardhi Kambi ya Jeshi Mtabila**

**MHE. VUMA A. HOLLE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua mgogoro wa ardhi kati ya Kijiji cha Mgombe na Kambi ya Jeshi Mtabila?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu swal, kwa ruhusa yako naomba nimshukuru Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge lako. Vile vile namshukuru sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Amirijeshi Mkuu wa Majeshi yetu kwa kuniamini na kunithea kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Ushetu, wapiga kura wangu kwa kuniamini na kunipitisha bila kupingwa na kwa kura nyingi ambazo walizitoa kwa Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe pamoja na Spika kwa ushindi mkubwa na kuaminiwa na Bunge hili. Vile vile nawapongeza Wabunge wote kwa kuchaguliwa na wananchi kuwa Wabunge wa Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kujibu swal la Mheshimiwa August Vuma Holle, Mbunge wa Kasulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Jeshi ya Mtabila – 825/KJ ipo Wilayani Kasulu, Mkoani Kigoma. Eneo husika lina ukubwa wa ekari 12,206.05 ambalo awali lilitumiwa kama Kambi ya wakimbizi. Aidha, mwaka 2012 eneo hili lilikabidhiwa kwa Jeshi na kuwa Kiteule na mwaka 2014 kiliundwa Kikosi cha Jeshi Mtabila.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa ardhi ulianza baada ya wananchi wa Vijiji vya Mgombe na Katonga

kuvamia eneo hilo kwa shughuli za kilimo na hatimaye kuweka makazi. Kwa sasa wananchi waliokuwa wamevamia eneo hilo wameondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeanza kuutatua mgogoro uliopo kwa kufanya vikao na uongozi wa Wilaya. Tarehe 11 na 12 Januari, 2021 Viongozi wa Kikosi cha Jeshi Mtabila walikutana na Uongozi wa Wilaya ya Kasulu na kuamua kuihamisha barabara inayokuwa inapita katikati ya kambi kuelekea Kijiji cha Shunga hadi Nchi ya Burundi ipite mpakani mwa eneo la Kambi. Pia, *TANROADS* wameweka alama za barabara tarehe 13 Januari, 2021 ikiwa ni hatua ya kuitambua barabara hiyo na kuiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itatuma timu ya wataalam kukutana na uongozi wa Mkoa, Wilaya na Vijiji husika kwa lengo la kutatua mgogoro huo. Nawaomba wananchi wawe na subira wakati Serikali inalifanya kazi suala hili na kulipatia ufumbuzi. Aidha, Wizara inawasihi Viongozi wa ngazi zote kuwaelimisha na kuwasisitiza wananchi katika maeneo yao kutovamia maeneo ya Jeshi. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Augustine Holle Vuma, swalii nyongeza.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Waziri, naomba kuuliza swalii nyongeza. Kwa kuwa inafahamika wazi kwamba baada ya Kambi ya Wakimbizi kuondoka, Serikali ilifanya *expansion*, yaani illongeza mipaka ya Kambi ile ikamega Vijiji vya Katonga, Mgombe, Nyamusanzu na Buhoro bila kufuata taratibu. Bahati mbaya wakawa wamekabidhiwa Jeshi; na kumekuwepo na jitihada za Ofisi ya Mkuu wa Wilaya wakishirikiana na Jeshi kutaka kuwarudishia wananchi maeneo. Sema walitaka kuwarudishia kipande kidogo, wananchi wakawa wamegoma.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kufanya jambo hili kwa haraka ili wananchi wale waweze kupata haki

yao ya mashamba hayo ambayo yamechukuliwa kwa muda mrefu, aidha kwa fidia ya maeneo au fidia ya fedha? (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Vuma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza uniruhusu nimpongeze tu Mheshimiwa Vuma, kwa juhudii zake anazozifanya kuhakikisha kwamba mgogoro ambao ulijitokeza tunaweza kuumaliza. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wafahamu kwamba Jeshi ni la kwao. Hili ni Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Watambue kwamba uwepo wa Jeshi ni kwa manufaa yetu sote. Kwa hiyo, tumekuwa na maeneo makubwa katika maeneo yetu, lakini lengo lake ni kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanatumika kwa ajili ya shughuli za Jeshi na vifaa vya Jeshi. Kwa hiyo, wananchi wakitambua hivyo, nawaomba tu wawe na ushirikiano. Nafahamu ipo migogoro kadhaa lakini nafahamu pia juhudii imefanyika kuhakikisha migogoro mingi tumeweza kuimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namhakikisha Mheshimiwa Vuma kwamba suala la kumaliza mgogoro tunamaliza kwa kuwa kuna hatua nzuri tumezifikia. Vikao vya awali kama nilivyosema, vimeshafanyika, lakini sasa vikao ambavyo vitakuja kuendelezwaa ni kuhakikisha kwamba tunamaliza mgogoro huu. Zipo Sheria za Ardhi na Sheria za Vijiji zitatumika ili kuhakikisha wananchi hawa wanapata haki zao.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, lakini naomba tuendelee kushirikiana; na wananchi wavute subira, tuko kwenye hatua nzuri ya kumaliza mgogoro huu. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Matatizo yaliyoko Kasulu Vijiji yanafanana na matatizo yaliyoko kwenye Jimbo langu la Mbozi katika Kijiji cha Sasenga na Itewe, kuna mgogoro kati ya wananchi na Kambi ya Jeshi. Napenda kumuuliza Waziri wa Ulinzi. Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua huo mgogoro ambao umekuwa ni wa muda mrefu kati ya hivyo vijiji na Kambi ya Jeshi 845KJ. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwenisongole kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba katika Kambi ya Itaka kuna shida hiyo ya mgogoro. Niseme kwamba migogoro hii imesababishwa na mambo mengi ikiwemo lile suala tu la uzalendo, majeshi yetu, pale ambapo tulikuwa tunawaruhusu wananchi kufanya shughuli zao; na walipozoea kufanya shughuli zao wakaamua kuhamia katika maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, kwamba tunafanya utaratibu maeneo yote na tumeshatambua maeneo yote yenye mgogoro na kwa hiyo, tumejipanga kwa ajili ya kuitatua. Tumeanzisha kitengo maalum cha miliki kuhakikisha kwamba migogoro yote tunaimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Mwenisongole kwamba tunafahamu shida ya Itaka na kuna hatua zinachukuliwa, tunakwenda kutatua shida ambayo iko kwa wananchi. Vilevile nawasihi sana wanasiasa na viongozi mbalimbali, kwamba kuna wakati mwingine tumetafuta kura Waheshimiwa Wabunge tukiahidi kwamba tutawasaidia

wananchi kupata maeneo ambayo ni ya Jeshi. Niwahakikishie tu kwamba tutafuata taratibu kuhakikisha kwamba haki inatendeka, wananchi wanapata haki zao na Jeshi linaendelea kufanya shughuli zake bila kikwazo chochote. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi, swalii la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Matatizo yaliyojitekeza huko Kigoma, ndiyo hali ilivyo katika eneo la Kampuni Mpanda Mjini.

Je, ni lini Serikali itakuja kutatua mgogoro wa wananchi na Jeshi katika eneo la Kampuni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu la nyongeza la Mheshimiwa Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua mgogoro uliopo na nikipongeze Chama Cha Mapinduzi kwa sababu mlezi wa Chama katika Mkoa ameliwasilisha suala hili mezani kwangu na mimi nimeshachukua hatua. Nimetoa maelekezo ili uchambuzi wa kina juu ya mgogoro huu niupate.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Kapufu asiwe na wasiwasi na tutakwenda kwa kasi kubwa kuhakikisha kwamba wananchi katika Jimbo hili la Mpanda wanakaa vizuri, waendelee na shughuli zao na Jeshi nalo liendelee na shughuli zake. Kwa hiyo, taratibu zinaenda vizuri Mheshimiwa Kapufu naomba avute Subira tu kidogo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swalii la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Wananchi wa Mtaa wa Kenyambi na Bugosi katika Mji wa Tarime wana mgogoro wa muda mrefu na Jeshi la Wananchi na Serikali imeshafikia hatua nzuri tu ya kufanya tathmini na ikarudia tena kufanya tathmini bado imebakiza malipo. Napenda kujua ni lini wananchi wale wataenda kulipwa fidia yao ili waweze kuondoka maeneo yale na kuwaachia Jeshi la Wananchi wa Tanzania? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru kwa kutambua kwamba tunaendelea kuwajali wananchi wetu wa Tanzania na niseme tu kwamba migogoro hii ilikuwepo kadhaa lakini niseme kwamba kati ya migogoro hiyo, zaidi ya asilimia 50 ya migogoro tumeshaitatua. Yako maeneo ambayo tumeyatambua kwa ajili ya fidia na wananchi wameshalipwa, yapo maeneo mengi ambayo tayari tumeshalipa. Hii inaonesha tunao mwendelezo mzuri wa kuendelea kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wananchi hawa wa Tarime wavute subira kwa sababu tunatafuta fedha. Tukipata fedha kwa maeneo yote ambayo tumeyatambua yanahitaji fidia kwa wananchi wetu tutakwenda kuwafanya malipo. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge kuvuta Subira na wakati mwingine tunaweza tukaonana ili nimueleze kwa kinagaubaga namna tunavyokwenda kutatua matatizo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Tutaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu, sasa aulize swali lake.

Na. 95

**Hitaji la Umeme Vijiji vya Wilaya ya Kakonko**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza:-

(a) Je, ni kwa nini vijiji vyote vya Wilaya ya Kakonko havijapata umeme?

(b) Je, ni lini vijiji hivyo vitapata umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Buyungu lina jumla ya vijiji 44, vijiji 40 tayari vinapatiwa umeme kuititia awamu ya pili na ya tatu ya utekelezaji wa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini. Kazi inayoendelea sasa ni kuunganisha umeme katika vijiji 22 kwa wateja ambavyo vilipata umeme tayari ili kukamilisha mpango kazi aliopewa mkandarasi katika eneo hilo. Kazi hiyo, inatarajia kukamilika ifikapo mwezi Aprili, 2021.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa usambazaji wa umeme vijijini umekuwa unafanyika kwa awamu, vijiji vinne vilivyobaki ambavyo ni Kijiji vya Rumashi, Nyamtukuza, Nyabibuye na Kinyinya viko katika mpango wa *REA* awamu ya tatu mzunguko wa pili utakaoanza mwezi Februari 2021 na kukamilika Septemba, 2022.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, swali la nyongeza.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kupeleka huduma kwa wananchi. Tatizo lilloljitokeza hapa ni baadhi ya vitongoji hasa katika Mji wa Kakonko kurukwa. Mfano, vitongoji vya Itumbiko, Mbizi, Kizinda, Cheraburo zikiwemo taasisi kama shule za makanisa. Kwa nini taasisi na vitongoji hivi vinarukwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, lini sasa haya maeneo ambayo yamerukwa yatapewa huduma hiyo ya umeme? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aloyce Kamamba, Mbunge wa Kakonko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vitongoji vya Jimbo la Kakonko havijarukwa isipokuwa Serikali inaendelea kupeleka umeme katika vijiji na vitongoji vyetu kwa awamu. Kwa hiyo, kadri ya upatikanaji wa fedha vitongoji vimekuwa vikipatiwa umeme kulingana na mazingira yalivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari umeme umepelekwa katika vijiji 40 vya Jimbo la Kakonko na wakati tunapeleka umeme katika vijiji hivyo baadhi ya vitongoji vilifikiwa katika awamu ya pili ya REA na awamu ya tatu mzunguko wa kwanza. Sasa awamu ya tatu mzunguko wa pili itapeleka umeme katika vijiji lakini na baadhi ya vitongoji pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Kakonko lipo katika awamu ya pili (b) ya mraji jazilizi wa umeme katika vitongoji. Jumla ya vitongoji 49 vitapatiwa umeme katika Jimbo la Kakonko na mradi huu wa jazilizi unaanza kuanzia mwezi Aprili. Kwa hiyo, kadri ya upatikanaji wa fedha, vitongoji vya Jimbo

la Kakonko lakini na vitongoji vingine vingi nchini vitaendelea kupelekewa umeme taratibu ikiwa ni pamoja na taasisi za umma. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jerry Silaa, swali la nyongeza.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani kwa Serikali kwa kufungua wilaya ya TANESCO pale Chanika na kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nishati kwa kufanya ziara kwenye Jimbo la Ukonga, je, Serikali inawaeleza nini wananchi wa Jimbo la Ukonga ambao mpaka sasa miradi yao ya REA hajakamilika kwenye Kata za Chanika, Zingiziwa, Msongola, Majohé na Kivule? Serikali inatoa tarehe gani wananchi wategemee mradi huu kukamilika? (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jerry, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali kwamba miradi ya umeme ya REA awamu ya tatu mzunguko wa pili itaanza mwezi huu wa pili na itakamilika kufikia Septemba, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwa ujumla kwamba miradi yote ya kupeleka umeme vijiji kwa vijiji 2,150 vilivyokuwa vimebakia havijapata umeme, vyote vitapatiwa umeme katika awamu hii ya tatu mzunguko wa pili ya REA. Baada ya hapo hatutarajii kuwa na kijiji chochote ambacho kitakuwa hakina umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwasihî Waheshimiwa Wabunge waendelee kuwa watulivu na

wajiandae kupokea mradi mkubwa wa kupeleka umeme vijiji ambao utakuwa unakmilisha vijiji vyote ambavyo vilikuwa havijapata umeme.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 96

### **Ununuzi wa Kokoa Kyela na Rungwe**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Serikali imezuia kampuni binafsi kununua kokoa katika Wilaya za Kyela na Rungwe kwa msimu huu na Vyama vya Ushirika havina uwezo wa kununua kokoa hizo kwa wananchi:-

Je, ni lini Serikali itaruhusu tena kampuni binafsi kuendelea kununua kokoa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijazuia kampuni binafsi kununua kokoa kwa wakulima bali imezuia mfumo wa ununuzi wa ulanguzi maarufu kama "njemke" ambao umekua ukimlalia mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuitia mfumo wa Vyama vya Ushirika imekuwa ikikusanya na kuuza mazao hayo kuitia minada ya wazi katika kusaidia kutambua bei za mazao hayo (*price discovery*). Kwa kutumia utaratibu wa

ushirika wakulima waliouza kokoa kwa mfumo wa stakadhi za ghalani bei ya kokoa ilipanda kutoka Sh.3,000 mpaka kufika kiasi cha Sh.5,000 katika msimu wa 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mfumo huo wakulima hupeleka kokoa katika Vyama vya Msingi na kupata asilimia 60 ya bei ya soko. Baada ya mnada kufanyika hupewa kiasi kilichobaki ili kufikia bei ya mnada kwa kuzingatia gharama za usafiri, uhifadhi, ushirika na ushuru. Bei hii iko juu ukilinganisha na bei ya ununuzi binafsi kabla ya ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia faida inayopatikana kuititia kuuza mazao katika ushirika, Serikali haitoruhusu makampuni binafsi kununua kokoa kwa wakulima kwa kununua kuyafuata shambani. Aidha, Serikali kuititia Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaendelea kuimarisha na kujenga uwezo wa Vyama vya Msingi ili viweze kukusanya, kununua kokoa yote kwa wakulima na kuwasaidia wakulima kupata pembejeo sambamba na kuwa na nguvu ya pamoja katika kusimamia bei.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na jibu la Mheshimiwa Waziri, je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa Vyama vya Ushirika ili waweze kuwalipa wakulima wa kokoa Wilaya ya Rungwe na Wilaya ya Kyela kwa wakati kwa maana mpaka sasa wanadai madeni yao? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Serikali inatambua kwamba kokoa ya Kyela na Rungwe ni kokoa bora baada ya kokoa ya Ghana.

Ni nini Serikali itafanya kuwawezesha wakulima hawa na kuwasimamia bei yao iongezeke maana hiyo uliyosema Mheshimiwa Waziri ya shilingi 5,000 bado ni ndogo, haitoshi kwa wakulima maana wao ndiyo wawekezaji wakubwa na wenye kazi kubwa katika ukulima wao? Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakagenda maswali yake mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kulipa wakulima kwa wakati, kwa utaratibu na mwongozo ambao Wizara ya Kilimo imeutoa, baada ya mnada, mkulima anatakiwa awe amepata fedha zake ndani ya saa 72. Huu ndiyo utaratibu ambao tumeuweka. Kwenye minada ya kokoa tumejenga utaratibu ambapo mkulima anapewa malipo ya awali kabla ya mnada na baada ya mnada hupewa fedha ambayo ni *difference* kati ya fedha ya awali na fedha ambayo mnada umefikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hatua tunazochukua sasa hivi ni kuvizezesha Vyama vyा Ushirika kupitia *Tanzania Agricultural Development Bank* kupata fedha kwa gharama nafuu ili waweze kuwa na uwezo wa kukusanya mazao kwa wakati na kuyapeleka mnadani na pale ambapo mnada unakuwa bei yake haivutii, wakulima waweze kusubiri mnada uweze kuwa na bei nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Vyama vyा Ushirika vyा Kokoa vilivyoko katika Mkoa wa Mbeya sasa hivi vina maongezi na *Tanzania Agricultural Development Bank* na sisi Wizara ni sehemu ya majadiliano hayo. Bado hatujaruhusu wachukue fedha kwa sababu riba ambayo iko mezani ni kubwa kwa kiwango cha asilimia 9. Kwa hiyo, tunaendelea na majadiliano na hili tutalirekebisha. Tumhakikishie tu kwamba tunaendelea kuboresha mfumo wa stakabadhi ghalani ili kupunguza *gap* kati ya mnada na fedha kumfikia mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubora, ni kweli na ndiyo maana bei ya kokoa ya Tanzania imepanda kutoka Sh.3,000 mwaka 2017 na sasa imefika wastani wa Sh.5,000

kwa kilo. Bado sisi kama Wizara tunaamini kwamba kokoa yetu ni bora. Sasa hivi hatua tunazochukua, tumeanza utaratibu wa *certification* ili kuweza ku-meet *International Standard* ili na sisi tuwe na zile *competitive advantage* ambazo zinakubalika katika soko la dunia. Ni lazima bidhaa ile ithibitike kupitia kitu kinaitwa *Global Gap Certification* kwamba bidhaa hii ni *organic*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hizi ndiyo hatua tunachukua na mwaka jana tulipitisha sheria ya *TAFA* hapa na sasa *TAFA* wanaanza kazi ya ku-certify mashamba ili yaweze kupata hiyo hadhi. Kwa hiyo, tunaomba mtupe muda tuko kwenye hatua nzuri tunaamini tunafika, *Inshaallah*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya zao la kokoa iliyoko kule Mbeya ni sawasawa kabisa na changamoto ambayo zao la korosho kwenye Wilaya ya Liwale inakumbana nayo. Kwenye msimu uliopita 2018/2019 mikorosho yenye ilikuwa inakauka bila kujua sababu ni nini. Kwenye msimu huu uliopita kwa nje zinaonekana korosho ni nzima lakini ukizipasua kwa ndani zimeoza.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutuletea wataalam kwenye Wilaya ya Liwale waje kufanya tathmini au utafiti kujua ni nini changamoto za korosho Wilaya ya Liwale zinazosababisha wananchi wale wapate bei isiyoridhisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kuchauka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi tu siyo tuko tayari, timu ya Wizara ya Kilimo leo ina wiki mbili ikishirikiana na watu wa *TAF*A na Naliendele. Timu hii wako Mkoa wa Mtwara na wengine wako Ruvuma kuangalia athari zilizojitokeza katika msimu uliopita ili tuwe tuna majibu sahihi ni athari za kimazingira ama kuna *attack* kwenye mimea yetu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ali Anyigulile Mlaghila, Mbunge wa Kyela sasa aulize swali lake.

Na. 97

### **Mfumo wa Stakabadhi Ghalani**

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA** aliuliza:-

Mfumo wa Stakabadhi Ghalani kwa zao la kokoa haujamnufaisha mkulima:-

Je, ni lini sasa mfumo huo utabatidilishwa ili kukidhi lengo la ushirika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Anyigulile Mlaghila, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani ni utaratibu unaowezesha biashara kufanyika kwa kutumia bidhaa ambazo zinakuwa zimehifadhiwa katika ghalalililopewa leseni kwa mujibu wa sheria kifungu cha 5(a) cha sheria ya mwaka 2005 na marekebisho ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mfumo huu, mmiliki wa bidhaa anapewa stakabadhi ambayo inathibitisha ubora, uzito, idadi ya vifungashio na umiliki mahsusii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani kwa zao la kokoa umesaidia kuimarisha bei ya zao la kokoa kutoka wastani wa Sh.3,000 kwa kilo katika msimu wa 2017 hadi kufikia Sh.5,011 katika msimu wa 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani umesaidia kuimarisha na kuweza kugundua bei halisi na hivyo kumpa mkulima bei nzuri za zao hilo. Pia mfumo huu umeimarisha upatikanaji wa takwimu za uzalishaji na umesaidia ukusanyaji wa ushuru halali kwa Halmashauri za Kyela, Rungwe na Busokelo unaotokana na zao la kokoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika msimu wa 2018/2019 jumla ya tani 7,532 ziliuzwa ambapo jumla ya Sh.33,697,643,289.75 zilipatikana na kulipwa kwa wakulima na Sh.1,033,098,535.20 zilipatikana ikiwa ni ushuru kwa Halmashauri zote tatu. Katika msimu 2019/2020 jumla ya tani 9,483 ziliuzwa na wakulima kupata jumla ya Sh.45.721 na Halmashauri kujipatia jumla ya shilingi bilioni 1.367. Hadi kufikia tarehe 21 Januari 2021, jumla ya kokoa zilizouzwa ni tani 7,000 na kiasi cha shilingi bilioni 33 zimelipwa kwa wakulima na Halmashauri ya Rungwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kusimamia ubora wa kokoa kuititia Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani na hivyo ubora wa zao la kokoa umeongezeka kwa kuwa katika mfumo huu kokoa inaandaliwa kwa kuzingatia viwango vya ubora na matakwa ya walaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa mfumo huu wa Stakabadhi Ghalani umewafanya wananchi

na wakulima wa kokoa wasipate pesa papo kwa papo kama ambavyo Serikali leo imejibu; na kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Waziri ni tofauti kabisa na uhalisia ulioko kule *field*, je, anachukua hatua gani kwa watu ambao wametoa taarifa ambazo sio sahihi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa zao la kokoa linalimwa na watu kwenye nyumba/kaya zao na siyo mashamba makubwa na wanatumia muda mwangi kukusanya hizo kokoa kidogo kidogo na pesa zinazolipwa zinachukua muda mrefu na kwamba makampuni yanayonunua yanaanza kwanza kukubaliana wao kwa wao pamoja na makato makubwa, je, Serikali inachukua hatua gani kudhibiti haya matatizo yaliyopo kwa wakulima? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza anaposema taarifa tulizotoa sio sahihi; taarifa tulizotoa ni sahihi, wakulima wamelipwa kutokana na takwimu tulizonazo na uthibitisho tulionao. Kwa hiyo, kama ana kesi maalum ya mkulima ama wakulima ambao hawajalipwa atuletee hiyo kesi na tutaishughulikia kwa wakati na inavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba kupitia Bunge lako Wabunge wanapoinuka na kusema kwamba, kuna mkulima X hajalipwa na sisi Wizara tunapoomba kwamba, tuleteeni uthibitisho, tunaomba mtuletee uthibitisho, mjadala huu usiishie humu ndani. Mtuletee uthibitisho, ili tuweze ku-*resolve* tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, taarifa tulizotoa ni sahihi. Hoja iliyoko ya kwamba, mkulima anapovuna, anapokausha, anapopeleka kwenye chama cha msingi

mpaka inapoenda kwenye chama kikuu ni vizuri tukaelewa kwamba, *cocoa* inakusanywa kidogokidogo; mkulima atavuna kilo moja, baada ya siku chache atavuna kilo kadhaa, baada ya siku chache atavuna kilo kadhaa atapeleka kwenye chama cha msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna hoja kwamba, tujadiliane kupunguza muda wa kutoka kwenye chama cha msingi kwenda kwenye mnada, lakini hatuwezi kurudisha mfumo ambaao ni maarufu kama *njemke* ambaao wakulima walikuwa wanafuatwa majumbani na wanakusanyiwa *cocoa* yao na wanapewa bei ndogo na walanguzi hao ndio wanapeleka kwenye mnada, hatutaruhusu huo mfumo. Kama kuna changamoto kwenye mfumo wa malipo, tuujadili huo mfumo wa malipo na kama Waheshimiwa wana maoni watuletee, lakini Wizara sasa hivi tunatengeneza utaratibu wa kuondoa mfumo wa kuhifadhi mazao ya *cocoa* kwenye maghala binafsi na yatatumika maghala ya Serikali. Tutaanza pia kuuzia katika *AMCOS*, badala ya kuleta kwenye chama kikuu cha ushirika, ili tuweze kupunguza *time* kati ya mnada na malipo ya mkulima. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, sasa aulize swali lake.

Na. 98

**Kujenga kwa Lami Barabara ya Lushoto – Mlalo**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, ni lini ahadi ya Serikali ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Lushoto – Muyanta hadi Mlalo itaanza kutekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

## **NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Lushoto – Mlalo yenyeye urefu wa kilometra 41.93 ni sehemu ya Barabara ya Lushoto – Mlalo – Umba *junction* yenyeye urefu wa kilometra 66.23 ambapo katika hilo, kilometra tisa ni za lami na kilometra 32.93 ni za changarawe. Katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 kiasi cha milioni 420 zimetengwa kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa mita 400 za barabara hii kwa kiwango cha lami. Ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu zilizobaki utaendelea kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Barabara ya Lushoto – Mlalo – Umba *Junction* kiuchumi, kiulinzi na kiutalii na hivyo wakati ujenzi kwa kiwango cha lami kwa awamu ukiendelea, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo mbalimbali kila mwaka. Katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 jumla ya Shilingi milioni 475.5 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ili kuhakikisha kuwa barabara hiyo inapitika majira yote ya mwaka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Swali la kwanza; barabara hii ni muhimu sana kwa shughuli za uchumi wa wananchi wa Lushoto, hasa ukizingatia kwamba, mazao tunayozalisha kule ni mbogamboga na matunda ambayo ni rahisi kuharibika. Kulikuwa na ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, angalau sasa barabara hii ijengwe japo kwa kiwango cha kilometra 10 kwa mwaka. Je, tunapoelekea kutengeneza bajeti Serikali haioni ni muhimu kutenga kiwango hicho cha kilometra 10 kwa kila mwaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili; kwa kuwa barabara hii imeendelea kutia hasara wananchi wa Mlalo, hasa nyakati za mvua. Je, Serikali sasa iko tayari kuwalipa fidia mara ambapo wananchi wanapata hasara ya mazao yao kuoza barabarani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara hii ambako kunazalishwa sana matunda na mbogamboga. Kwa kutambua umuhimu huo ndio maana Serikali tayari imeshakuwa na mpango wa kujenga hii barabara. Tunatambua pia kwamba, Serikali ilitoa ahadi kwamba, itaendela kujenga hii barabara walao kwa kilometra 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, ameuliza kama kwenye bajeti ijayo je, tutajenga. Itategemea pia na upatikanaji wa fedha na kama itapatikana si tu kilometra 10 balii inawezekana ikawa ni kukamilisha kabisa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili; endapo kama tutatoa fidia kwa wale wanaopata matatizo hasa pale ambapo mazao yao yanaharibika. Tumeshaongea na Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Tanga, ili badala ya kuendelea kutengeneza kile kipande wanachokiendezea, basi atengeneze yale maeneo ambayo ni korofi, ili yaweze kuimarika na kusitokee tatizo kama hilo. Kama kuna changamoto nyingine basi namwomba Mheshimiwa Shangazi, Mbunge wa Mlalo, anipatie. Nimwahidi Mheshimiwa kwamba, nitafika kuona hito changamoto ambazo anazisema. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swalii la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona, nilitaka kunyosha mikono miwili. Naomba niulize swalii moja. Kwa vile Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alipokuwa kwenye kampanye kule Vunjo aliahidi kujenga barabara ya Kilema *a.k.a* barabara ya Nyerere ambayo ni kilometra tisa; barabara ya Uchira kwenda Kisomachi kilometra nane tu na Mabogini – Kahe na Chekereni ambayo na yenyewe ni kilometra 22 tu kwa kiwango cha lami. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akatuhakikishia kwamba, barabara hizo zimeingizwa kwenye mpango wa 2021/2022? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Kime, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi alizosema ni ahadi za Rais na ni ahadi katika kipindi cha uchaguzi wa 2020. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Kime avute subira kwa sababu, bajeti ndio inaenda kwa hiyo, tutaangalia. Siwezi nikasema kwa sasa kwa sababu, hiyo bajeti bado haijapitishwa, lakini kama ni ahadi ya Rais, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kime kwamba, ahadi za Rais zitazingatiwa katika kutekelezwa kwa bajeti zinazokua kuanzia 2021/2022. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa muda wetu umekwenda, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto. Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 99

**Upungufu wa Watumishi wa Afya Nchini**

**MHE. MWANTUMU M. ZODO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na upungufu wa Watumishi wapatao 16,000 kwenye Sekta ya Afya nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantum Mzamili Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Tanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya upungufu wa watumishi katika sekta ya afya ambayo kwa kiasi kikubwa hivi sasa imetokana na mahitaji mapya yanayotokana na ujenzi na upanuzi wa hospitali za rufaa za kanda, mikoa, ujenzi wa hospitali za Halmashauri, ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali inachukua hatua mbalimbali kukabiliana na changamoto ya uhaba wa watumishi ambapo katika kipindi cha miaka mitano iliyopita 2015 hadi 2020 Serikali illajiri watumishi wapatao 14,479 na zaidi ya watumishi 565 walipatiwa ajira za mkataba kwa kugharamiwa na makusanyo ya vituo vya kutolea huduma za afya. Pia katika mwaka wa fedha 2020/2021 sekta ya afya inatarajia kuajiri jumla ya watumishi wapya 12,476.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwantum Mzamili Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo. Swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani

wa kupeleka watumishi wengi zaidi katika Mkoa wa Tanga, hasa ikizingatiwa kuwa Mkoa wa Tanga ndio mkoa wenyewe halmashauri nyingi zaidi nchini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; utoaji wa huduma za afya kwa vituo vyta Serikali unakabiliwa na changamoto nyingi tukilinganisha na vituo binafsi. Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha huduma zinaboreshwani kwenye vituo vyta Serikali ili kuongeza mapato ya Serikali? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjilbu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ajira 12,476, Serikali inaenda kuelekeza kwenye maeneo kama aliyoyataja ndio kipaumbele kitakuwa, ukiangalia Mikoa kama Kigoma, Mtwara, Songwe na mingine ambayo kwa kweli ni mikubwa, lakini kuna upungufu mkubwa zaidi, itakuwa ndio *priority* ya Serikali. Kwa hiyo, tunachukua ushauri wake na utaenda kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilivile swali lake la pili ameuliza kwamba, alitumia neno mapato kwenye eneo upande wa Serikali. Ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba, ukiangalia kwenye vituo vyetu vyta Serikali, hasa ukiangalia kwenye eneo la bima tu, ukiangalia kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge utaona. Tukichukua hata zahanati tu, tuliwahi kuchukua moja, kwenye zahanati tu ya kawaida ambayo wanalipwa bima kidogo ukilinganisha na mkoani, unakuta wanaingiza milioni 84 kwa mwaka, lakini Serikalini wanaingiza 420, lakini ukigawa kwa idadi ya watumishi Serikalini tulijua walikuwa 187 huku kwenye *private* walikuwa 17, lakini utakuta kwa mwaka wanaingiza shilingi 5,300,000/=, lakini huku serikalini tena mkoani wanaolipwa zaidi wanaingiza shilingi 2,000,000=

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunafikiri kuna umuhimu wa kwenda kufanya kazi kuhakikisha *productivity* ya watu wetu inaongezeka. Tukiongeza kwenye eneo la *productivity* maana yake hata kuna mahali ambapo *productivity* ndio inasababisha ione kane kwamba kuna upungufu, lakini upungufu sio halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna eneo la watumishi; tutaenda kuchukua *modal* ya Wizara ya elimu. Wizara ya elimu wameshirikiana vizuri sana na *private sector* kwamba, *private sector*wana shule, lakini na Serikali ina shule, lakini wamekuwa wanashirikiana vizuri sana bila kuwepo anayenyonya upande huu. Hivyo, kwenye afya tutaenda kudhibiti hasa kwenye eneo la kwamba, unakuta kuna watumishi wakati wa kufanya kazi Serikalini wako eneo la *private sector*wakati wameajiriwa ndani ya Serikali. Nalo hilo litaenda kufanyiwa kazi kwa nguvu na litatusaidia sana kuweka mambo sawa. Ahsante. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Rungwe, sasa aulize swalii lake.

Na. 100

### **Ukarabati wa Miundombinu ya Maji – Tukuyu**

**MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza:-

Serikali ilifanya upembizi yakinifu na kubaini kuwa jumla ya shilingi Bilioni 21 zinahitajika ili kukarabati miundombinu ya maji Mji wa Tukuyu:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha na kuanza ukarabati wa miundombinu hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Albert Anton Mwantona, Mbunge wa Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha wananchi wa Mji wa Tukuyu wanapata huduma ya maji safi na salama ya kutosha, Serikali imeendelea na mikakati ya muda mfupi na mrefu. Mkakati wa muda mfupi ulihusisha uboreshaji wa chanzo cha maji cha Masalala, ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 200,000 pamoja na ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa mita 750. Kazi hizo zimesaidia kuimarisha huduma ya maji kwa wakazi wa Mji wa Katumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mkakati wa muda mrefu wa kuboresha hali ya upatikanaji wa maji safi katika Mji wa Tukuyu, Serikali kwa kutumia wataalam wa ndani wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira za Mbeya na Tukuyu inafanya mapitio ya usanifu wa mahitaji kwa ajili ya uboreshaji wa huduma ya maji katika Mji wa Tukuyu kwa kutumia chanzo cha Mto Mbaka. Kulingana na usanifu kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mradi huu ni pamoja na ujenzi wa bomba kuu la kilometra 15.5, ujenzi wa bomba la usambazaji maji kilometra 20, ujenzi wa tenki lenye ujazo wa lita 2,000,000. Mradi huu utatengewa fedha katika mwaka wa fedha 2021/2022 na utekelezaji wake unatarajia kuanza mwezi Julai, 2021.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, swali la nyongeza.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Wizara ya Maji. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwenye Mradi wa Maji Tukuyu nimeridhika, lakini kuna mradi mwingine ambao unaendelea katika Mji wa Ushirika, Kata ya Mpuguso. Tenki tayari limeshajengwa, mabomba tayari yameshafika kwenye tenki, usambazaji wa maji bado kwa wananchi kwa muda mrefu. Naomba Wizara ituambie wananchi wa Rungwe lini itaanza kusambaza maji kwa wananchi wa Rungwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili; tuna Kituo cha Afya cha Ikuti ambacho kina matatizo makubwa sana ya maji. Nilikuwa naomba Wizara iwaambie wananchi wa Ikuti, Jimbo la Rungwe, ni lini maji yatasambazwa hasa baada ya upembuzi yakinifu wa mradi ule kuonekana kwamba, ni milioni 100 tu ambayo itapeleka maji kutoka kwenye chanzo cha maji mpaka kwenye Kituo cha Afya cha Ikuti? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge, Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Nailbu Spika, mradi unaoendelea pale miundombinu yake imeshakamilika, imebaki tu usambazaji wa maji. Mheshimiwa Mbunge mradi ule unakwenda kukamilika wiki chache zijazo na maji yatafika mabombani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Kituo cha Afya cha Ikuti kupata maji, Mheshimiwa Mbunge Serikali tutalifanyia kazi na namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, ndani ya muda mfupi utekelezaji wake utakuja kufanyaika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Amar, swalii la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi niulize swalii dogo la nyongeza. Kwanza nimpongeze Naibu Waziri wa Maji pamoja na Waziri wake kwa kuufuutilia Mradi wa Nyanghwale na hivi karibuni unaenda kukamilika, nawapongeza sana. Swalii langu ni kwamba, kwa kuwa mradi huu unaenda kukamilika. Je, bajeti ijayo Serikali imejipanga vipi kwenda kuweka mpango wa kusambaza maji kwenye kata zifuatazo: Kata ya Busolwa, Nyanghwale, Ijundu, Kakola, Shabaka na Mwingilo. Je, Wizara imejipanga vipi kwenda kusambaza maji hayo kwenye bajeti ijayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Hussein Amar, Mbunge wa Nyanghwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuweka mipango mahususi kuhakikisha mradii ule ambao tayari upo kwenye utekelezaji kwenye hatua za mwisho unakwenda kukamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, swalii la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Suala la maji la Tukuyu linalingana kabisa na matatizo ya maji katika Jimbo la Makambako. Mambo ya upembuzi yakinifu yalishafanyika. Je, Serikali ina mpango gani kupeleka maji au kutatua tatizo la maji katika Mji wa Makambako kwa sababu, tumekuwa tukiwaahidi watu kwa muda mrefu, ni lini sasa mradii ambao tumekuwa tukiwaambia wananchi utaanza kutekelezwa? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Makambako ni moja ya miji 28 ambayo inakwenda kunufaika na mradii ule mkubwa ambao tumeshapata fedha kutoka Benki ya Exim. Hivyo, Serikali inakwenda kuanza kutekeleza miradi hii yote ndani ya miji 28 ifikapo mwezi Aprili. Mheshimiwa Deo Sanga mradii wa maji Makambako nao ni sehemu ya miradi ya miji 28 hivyo kufikia mwezi Aprili wataalam wetu pamoja na wakandarasi watafika *site* kuanza kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza niishukuru sana Wizara ya Maji kwa sababu Jimbo letu la Temeke maji yamefika karibu kila kata. Tatizo letu kubwa ni kwamba bomba lile kubwa limepita katika barabara kubwa lakini kuvuta maji kwenda ndani ya nyumba zetu ambapo miundombinu siyo mizuri sana kwenye Kata za Buza na Kilakala na nyumba ziko mbali. Niombe Wizara ya Maji tunapoomba kuvutiwa maji ndani ya nyumba zetu, fedha ile ambayo tunatakiwa kuilipa kidogo ni kubwa, sasa mfikirie tuweze kuvuta kwa nusu ya bei halafu muendelee kutudai ndani ya malipo ya kila mwezi kama vile tunavyofanya luku ili tuweze kuona kila mmoja sasa anapata maji ndani ya nyumba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Hilo ni ombi nadhani utakuwa umeliandika Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea na Mheshimiwa *Engineer Ezra John Chiwelesa*, Mbunge wa Biharamulo Magharibi.

Na. 101

#### **Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Victoria Kwenda Biharamulo**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa mradi wa kutoa maji toka Ziwa Victoria kuyapeleka Biharamulo kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi hapo tarehe 16/09/2020 alipokuwa Biharamulo katika Kampeni za Uchaguzi Mkuu, 2020?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto za upatikanaji huduma ya maji katika Wilaya ya Biharamulo. Hivyo, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali inatekeleza mradi wa upanuzi wa mtandao wa maji wenyewe urefu wa km 10.9 katika maeneo ya Ng'ambo, Kalebezo, Nyakatuntu, Rubondo Chuoni na Rukagarata na kuchimba kisima katika eneo la Rukagarata. Thamani ya mradi huu ni shilingi milioni 178.9 na utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto ya uhaba wa maji katika Mji wa Biharamulo, Serikali ilihamua chanzo cha uhakika cha maji kiwe Ziwa Victoria badala ya bwawa na chemichemi vinavyotumika kwa sasa. Hivyo mradi wa usambazaji maji katika Mji wa Biharamulo ambao utatoa maji katika Ziwa Victoria umefikia katika hatua ya kuandaa makabrasha ya zabuni (*tender documents*). Utekelezaji utaanza katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Aidha, kupitia Mradi wa Maziwa Makuu, Wilaya ya Biharamulo itanufaika kupitia chanzo cha Ziwa Victoria ambapo jumla ya vijiji 12 vya Rwekubo, Rusese, Kabindi, Runazi, Rukora, Kikomakoma, Kagoma, Songambele, Kasozibakaya, Nyamigogo, Chebitoke na Nyabusozitapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya maji kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer Ezra John Chiwelesa*, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Nitoe shukrani kwa Serikali

kwa majibu mazuri kabisa ya kuridhisha kwa ajili ya wananchi wa Biharamulo lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa Miji ya Nyakanazi, Nyakahura na Nyanza ni miongoni mwa sehemu ambazo zinapanuka kwa kasi katika Wilaya ya Biharamulo lakini bado zina ukosefu wa maji. Naomba kujua au kusikia kauli ya Serikali jinsi gani hawa wananchi wataweza kupatiwa huduma ya maji katika mwaka huu wa fedha au mwaka ujao ili tuweze kuondoa kero hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, Kata ya Kaniha na Nyantakala zinabeba shule mbili kubwa za *boarding* pale Biharamulo na shule zile zina uhaba mkubwa wa maji. Naomba kupata kauli ya Serikali ni lini wataweza hata kuchimbiwa visima viwili virefu katika shule zile ili watoto hao waweze kuondokana na adha ya kupata maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa *Engineer Ezra John Chiwelesa*, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua vema tatizo la maji lililopo pale Biharamulo. Hivi karibuni Mheshimiwa Waziri alikuwa katika Kata ya Nyakahura kwenye ziara yake ya kikazi. Kwa sasa maji toka Bwawa la Nyakahura ambapo vijiji vinne vinapata maji, tunatambua utekelezaji wake unakwenda vizuri kwa vijiji vile vinne.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tunafahamu kuna ushirikiano mzuri kati ya RUWASA pamoja na *BWSSA*. Tayari Serikali inafahamu chanzo kile bado hakitoshelezi kwa sababu ya ongezeko la watu. Tayari Serikali kuitia *EWURA* imeshatenga fedha za usanifu wa maji kutoka kwenye Mto Myovozi. Lengo ni kuona kwamba eneo lote la Nyakahura

linakwenda kupata maji safi na salama ya kutosheleza hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye kwenye Kata ya Nyanza usanifu unaendelea. Pia tutahakikisha maji ya kutosha yanakwenda kupatikana. Tayari kuna chanzo chenye uwezo wa lita 50,000 kwa saa ambapo maji haya yatasaidia sana mpaka kwenye Kata ya Nyanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali inatambua umuhimu wa maji mashulenii. Tayari kwenye Shule ya Mbaba kuna kisima kirefu pale kimechimbwa na maji yanapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Nyantakara, mradi umetekelizwa. Pale tuna mradi mkubwa tu ambapo fedha zaidi ya shilingi milioni 300 zimeelekezwa na maji yatafika mabombani muda sio mrefu, haitazidi wiki tatu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumalizie swalii la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo.

Na. 102

### **Kufikisha Maji ya Ziwa Victoria Urambo**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Serikali iliahidi kufikisha Urambo maji ya Ziwa Victoria na kwa sasa yameshafika Tabora:-

(a) Je, ni hatua zippi zimechukuliwa katika kutekeleza azma hiyo?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa katika mwaka huu wa fedha na ni lini maji yatafikishwa Urambo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Jimbo la Urambo lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepata mkopo kutoka Serikali ya India kuititia Benki ya Exim ya India ambapo jumla ya Dola za Marekani milioni 500 zitatumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika miji 28 Tanzania Bara na Zanzibar. Kuititia mkopo huo, Mji wa Urambo ni kati ya maeneo yatakayonufaika na mkopo huo. Kwa sasa utekelezaji wa mradi huo upo katika hatua za manunuzi ya wakandarasi wanaotarajiwa kuwepo eneo la miradi ifikapo Mei, 2021 na utekelezaji wake ni muda wa miezi 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imetenga jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 1.89 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika Halmashauri ya Urambo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swalii la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naipongeza Serikali kwa majibu mazuri lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake aliyoitoa tarehe 30 Mjini Tabora ambayo ilituhakikishia kwamba tutapata maji na baadaye pia kuongezewa zaidi na Mheshimiwa Waziri wa Maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, je, Serikali haioni kwamba changamoto kubwa ya maji sasa inakaribia kupata ufumbuzi baada ya kuhakikishiwa kwamba mradi utafika huko, Mheshimiwa Waziri anaweza kuja Urambo kwa sasa hivi akaangalia hali halisi na huenda akaongezea hata maeneo yatakayonufaika na mradi huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tumuandalie mkutano wa hadhara arudishie maneno hayahaya ili wananchi wa Urambo waendelee kuishi kwa matumaini na kushukuru Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa kwa sababu amekuwa ni mfuatiliaji mzuri sana. Kwa kuwa ahadi ya Mheshimiwa Rais lazima tuitekeleze kwa nguvu zetu zote na Urambo inakwenda kunufaika, niseme niko tayari kuja Urambo na mkutano wa hadhara hapa ndiyo mahala pake. Nitahakikisha naelekeza vema jamii ya Urambo na watamuelewa Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa matatizo ya maji yanakwenda kufikia ukingoni.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kingu, swali la nyongeza

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Naomba na mimi niulize swali moja tu, ni lini Serikali ya Chama cha Mapinduzi itakwenda kutekeleza miradi ya visima 10 vilivyochimbwa Jimbo la Singida Magharibi katika vijiji vya Minyuge, Mpeta, Kaugeri, Mduguyu pamoja na Vijihi vya Mnang'ana, Munyu na Irisya ukizingatia Jimbo la Singida Magharibi ni mionganoni mwa Majimbo ambayo yana changamoto kubwa sana ya maji? Naomba nipate jibu *serious* kutoka kwenye Serikali *serious*. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kingu kutoka Singida Magharibi, kama ifuatavyo:-

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Siyo daktari.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Nimekutunuku au siyo. Wanasema dalili nje huonekana asubuhi, daktari rudi shule ukapate hiyo *profession.* (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali ni maeneo yote ambayo yalishafanyiwa usanifu tunakuja kuhakikisha kazi zinafanyika ndani ya wakati. Hiiyo visima vyote vitachimbwa kadiri ambavyo vipo kwenye bajeti na maji tutahakikisha hayaishii kwenye kisima bali yanatembea kwenye bomba kuu na kuwafikia wananchi kwenye mabomba yao katika makazi lakini vilevile katika vituo vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote yanakwenda kutekelezwa kwa kipindi hiki kilichobaki cha mwaka wa fedha na mwaka wa fedha 2021/2022. Isitoshe nitafika kuona eneo husika na kuleta chachu zaidi kwa watendaji wetu, japo tayari tuna watendaji wazuri katika Wizara na wanafanya kazi vizuri sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu hiki cha maswali, nitaleta kwenu matangazo.

Kwanza ni matangazo yahusuyo wageni waliopo hapa Bungeni. Tutaanza na wageni walioko jukwaa la Mheshimiwa Spika, nao ni wageni wangu watano kutoka Chuo cha Biashara (CBE), Profesa Emmanuel Mjema ambaye ni Mkuu wa Chuo cha CBE, karibu sana. Ameongozana na Dkt. Emmanuel Munishi ambaye ni Naibu Mkuu wa Chuo, Mipango, Fedha na Utawala, CBE, karibu sana. (*Makofi*)

Pia yupo Ndugu Tumaini Jeremiah ambaye ni Mkuu wa Chuo cha CBE *campus* ya Mbeya, karibu sana. Yupo pia Ndugu Arnold Dominick ambaye ni Mwenyekiti wa CBE

*Alumni, karibu sana. Yupo pia Ndugu Ally Nchahaga ambaye ni CBE Alumni, karibuni sana. (Makofi)*

Tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge. Tutaanza na wageni 34 wa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria na hawa ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Kampasi Kuu ya Morogoro wakiongozwa na Ndugu Salum Kova. Karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi ambaye ni Naibu Waziri wa Maji ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Mbeya wakiongozwa na kaka yake Ndugu Constantine Mahundi. Karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni saba wa Mheshimiwa George Mwenisongole ambao ni Maafisa Elimu na Wakuu wa Shule kutoka Mbozi, Mkoa wa Songwe, wakiongozwa na Afisa Elimu Wilaya, Ndugu Abihudi Fungamtama. Karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni 60 wa Mheshimiwa Eng. Kundo Andrea ambao ni Makatibu Kata na wapiga kura kutoka Bariadi, Mkoa wa Simiyu wakiongozwa na Katibu wa Mbunge, Ndugu Mabula Mvanga. Karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Hawa Chakoma ambao ni rafiki zake kutoka Kibaha, Mkoa wa Pwani na hawa ni Ndugu Siza Lyimbo na Ndugu Janefrida Mfikwa. Sijui wamekaa upande gani hawa, karibuni sana. (Makofi)

Pia wapo wageni 23 wa Mheshimiwa Jumanne Sagini ambao ni Madiwani kutoka Butiama, Mkoa wa Mara wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri, Mheshimiwa Peter Nyerere. Karibuni sana. (Makofi)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambaye ni shemeji yake kutoka Jijini Dar es Salaam, huyu ni Ndugu Nisile Mwakasala. Karibu sana. (Makofi)

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Eric Shigongo James ambaye ni mdogo wake kutoka Buchosa, Mkoa wa Mwanza, huyu ni Ndugu Martin Kaswahili. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Vedastus Manyinyi ambaao ni wapiga kura wake kutoka Musoma, Mkoa wa Mara na hawa ni Mwenyekiti wa CCM, Kata ya Nyasho, Ndugu Fidelice Manyerere na Ndugu Makunja John. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 11 wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke ambaao ni wafanyabiashara kutoka Kariakoo, Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Abdallah Mwinyi. Karibuni sana. (*Makofi*)

Pia tunao wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanachuo 100 kutoka Chuo cha Mipango kilichopo Jijini Dodoma. Wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunayo pia matangazo mengine mawili. Tangazo la kwanza linatoka kwa Katibu wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba Ofisi ya Mheshimiwa Spika imepokea vitabu vya orodha ya namba za simu za viongozi wa Serikali na vitabu vya orodha ya tozo, ada na kodi zilizofutwa na Serikali katika sekta ya kilimo nchini. Kila Mheshimiwa Mbunge atapatiwa nakala ya vitabu hivyo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, vitabu hivi ni muhimu sana hasa wale tunaotoka maeneo ya watu ambaao wanajishughulisha na kilimo ni muhimu sana kuangalia ni tozo, ada na kodi gani ambazo zimeondolewa. Kwa hiyo, tuwape moyo wananchi wetu wanaojishughulisha na kilimo. Kwa hiyo, kabla hamjaenda Majimboni mchukue vitabu hivyo ili mkawaelimishe wananchi huko.

Waheshimiwa Wabunge, pia liko tangazo la ibada ya Misa Takatifu ya shukrani na hili linatoka kwa Mwenyekiti wa Jumuiya hapa Bunge, Mheshimiwa Shally Josepha

Raymond, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wanajumuia na wageni wote kuwa leo kutakuwepo na ibada ya misa takatifu ya shukrani itakayoanza saa saba kamili mchana mara tu baada ya kusitisha shughuli za Bunge. Ibada hiyo itafanyika katika Kanisa la Bunge (*Chapel*) katika ukumbi wa Msekwa. Mnakaribishwa nyote kushiriki pamoja ili kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa matendo makuu aliyatutendea na anayoendelea kututendea katika maisha yetu.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndio mwisho wa matangazo tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu!

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nasimama kwa kanuni ya 68(7), sitaisoma kutokana na muda.

**NAIBU SPIKA:** Kanuni ya 68(7) inasemaje Mheshimiwa Sophia Mwakagenda?

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisilisome kwa sababu teknolojia imenishinda hapa, lakini naomba niendelee kwa maana kwamba...

**NAIBU SPIKA:** Kanuni zimebadilika Mheshimiwa, Mwongozo haupo Kanuni ya 68, lakini endelea.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu. Nilikuwa na swali namba 96 nililoiliza Serikali juu ya zao la *cocoa* katika Wilaya ya Rungwe na Wilaya ya Kyela. Majibu ya Serikali jinsi nilivyojibiwa kwenye Bunge lako lakini pia kwenye *tablet* yangu, inaonesha Serikali haiwajakataza wanunuzi binafsi kununua *cocoa*. Pia Mheshimiwa Waziri amesema kwamba asilimia 60 ya mapato baada ya mkulima kuuza kwenye mnada wanapewa kabla

wale wakulima. Naomba kujua Serikali kama ilitoa taarifa hiyo kwa wakulima wale wa Wilaya ya Rungwe na Wilaya ya Kyela, kwa maana tunavyojuu ni vyama ushirika ndio vinanunua *cocoa* na wakati mwingine kwa muda mrefu mapato ya wale wakulima yanachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Mwongozo wako kama Waziri amepewa majibu ambayo si sahihi labda yeeye mwenyewe hajafahamu, wataalam wake warudi kuangalia kama kweli kule chini hayo aliyojasema huwa yanafanyika; naomba Mwongozo wako ili watu wetu wawze kupata haki yao ya kimsingi hususan malipo kwa wakati kwenye zao la *cocoa*. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda amesimama akiomba Mwongozo kuhusu majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri wa Kilimo kwa swali lake Na. 96 liliokuwa linhusu ununuvi wa *cocoa* Kyela na Rungwe. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda anaomba Mwongozo kuhusu majibu yaliyotolewa hapa na ameleeza mahususi kwamba majibu ya Serikali yanaonesha kwamba wanunuvi binafsi hawajakatazwa lakini pia je, wakulima wameambiwa kuhusu hii asilimia 60 wanayolipwa *cocoa* ikinunuliwa na hivyo vyama msingi.

Waheshimiwa Wabunge majibu hayo ya swali Na. 96 niko nayo hapa, lakini pia Mheshimiwa Naibu Waziri alivyojibu maswali, swali hili la msingi lakini pia maswali ya nyongeza nimemsikia hapa majibu ya msingi ambayo na Mheshimiwa Sophia atakuwa nayo yako wazi, Mheshimiwa Waziri ameyasoma hayo. Lakini sehemu ya mwisho inasema hivi: "Mheshimiwa Spika, kufuatia faida iliyopatikana kuititia kuuza mazao katika ushirika, Serikali haitoruhusu makampuni binafsi kununua *cocoa* kwa wakulima kwa kuwa hununua kwa bei ndogo ambayo haitakuwa na uwiano wa bei sawa baina ya wakulima."

Waheshimiwa Wabunge kwa muktadha huo, utagundua kwamba hii sehemu ya mwisho inasema Serikali

haitaruhusu wanunuzi binafsi kwa kuwa wanaondoa uwiano kwa wale wakulima ndio jibu linavyosema hapa, jibu la msingi. Amesema pia jambo la kwamba je, wakulima wanafahamu kama hiyo asilimia 60 inalipwa na je, pia Wizara imeshafika kule chini kujiridhisha? Nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri amesema hivi, kama iko changamoto, kwa sababu taarifa ilizonazo Serikali ni kwamba fedha zimelipwa; kama kuna wakulima ambao hawajalipwa fedha, Naibu Waziri amesema apewe hizo taarifa ili Wizara izifanyie kazi kwa wakati.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda Mwongozo kuhusu jambo hili nafikiri ufuate kile alichokisema Naibu Waziri, mpeleke hao wakulima ambao hawajalipwa ili sasa kama hawajalipwa katika kipindi kwa sababu yeye kasema watalifuatilia kwa haraka na Bunge letu linaisha Ijumaa, ukiweza kupata hizo taarifa leo mpelekee, ili kama sasa kama hawatalipwa basi utarudi kwamba hawa wakulima hawajalipwa hiyo asilimia sitini yao kwa sababu ndicho alichokijibu hapa. Kwa hiyo, Mwongozo wa maswali aliyouliza Mheshimiwa Sophia Mwakagenda na majibu yaliyotolewa yote yako sawasawa mpaka atakapopeleka taarifa tofauti na hayo majibu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. (Makof)

Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa  
wa Miaka Mitano 2021/2022 hadi 2025/2026 na  
Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka  
2021/2022 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa  
Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali  
kwa Mwaka 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Tunaendelea na majadiliano, majina nimeshaletewa hapa na vyama vyenye uwakilishi hapa Bungeni, tutaanza na Mheshimiwa Jumanne Sagini, atafuatiwa na Mheshimiwa Humphrey Polepole na Mheshimiwa Oliver Semuguruka ajiandae.

**MHE. JUMANNE A. SAGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda wa dakika tano, naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye kuchangia. Mpango ulioandaliwa na Serikali kwa ujumla wake ni mzuri hasa huu wa miaka mitano. Kwanza niwapongeze Wizara ya Fedha kwa namna walivyochambua zile changamoto, maana yake wameainisha ni vitu gani vilisababisha Mipango miwili iliyopita na hususan Mpango wa Pili kushindwa kutekelezeka kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ninayoiona tu ni ile mikakati inayowekwa ya kushughulikia hizo changamoto ili mpango wa ili uweze kutekelezwa kwa ufanisi. Ushauri kwenye eneo hilo waichambue vizuri ile mikakati ya utekelezaji katika ku-deal na zile changamoto kwa kuwa kuainisha nani anafanya nini, wakati gani, kinahitaji rasilimali kiasi gani ili changamoto kama hizo zisije zikajitokeza kwenye utekelezaji wa Mpango wa Tatoo, kinyume chake tunaweza tukaingiza *statement* tutafanya hivi ukajikuta hizo *statement* hazijachambuliwa vizuri, changamoto hizo zikaendelea kuathiri utekelezaji wa Mpango unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuzungumza ni juu ya ile mikakati ya utekelezaji wa Mpango. Changamoto kubwa ninayoiona hapa ni kuainisha Mipango ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Serikali za Mitaa, Mikoa na Kadhalika. Serikali ni pana kweli, ukizungumza kwa ujumla tu kuainisha mipango ya MDAs na Mpango Mkuu wa Serikali, kumbukumbu zangu wakati niko

Serikalini kuna *tendencyya ku-cut na paste*, mtu atakwambia Mpango huu umezingatia MKUKUTA, *Vision 2020 – 2025*, sijui *SP* ya Wizara, lakini ukienda kuangalia mambo yaliyozungumzwa huoni moja kwa moja kama yana-*linkage* zozote na hiyo mikakati mikubwa ya kitaifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ushauri wangu kwamba Wizara ya yenye dhamana na fedha ifanye kama ilivyowahi kufanya huko nyuma, kutaka hizi *MDAs* zichambue unaposema umezingatia MKUKUTA, *Vision 2020 – 2025*, Mpango wa Miaka Mitano, awamu ya tatu, aoneshe kindakindaki nini kiko wapi na eneo gani. Kwa kufanya hivyo Mpango unaweza ukajikuta unatekelezwa, lakini vinginevyo inaweza kuwa ni *wishful statements* ambazo utekelezaji wake unaweza kuwa na changamoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa takwimu; imetajwa kama ilikuwa changamoto. Ningetamani waainishe sababu zilizosababisha kuwe na changamoto ya upatikanaji wa hizi takwimu na sasa tumejipangaje hizi takwimu ziweze kupatikana hasa kutoka kwenye *private sector*. Kama pamekuwa na changamoto na hatujaijua itakuwa ngumu awamu ijayo pia kuzipata hizo takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye muundo wa utekelezaji ambapo Wizara, Tawala za Mikoa na Halmashauri na *private sector* zinaingizwa, tuonyeshe *details* kama nilivyosema mwanzo kwani wakati mwingine unaweza kukuta hakuna *link* kati ya vinavyotokea kwenye Serikali za Mitaa na hivi vinavyokuja kuzungumzwa ngazi ya Serikali Kuu. Ili mpango uwe jumuishi ni vizuri hizo *linkage* zionekane bayana, badala ya kuwa na jedwali tunaloonesha *local government* lakini huioni vizuri kama ina *match* na yale matakwa ya kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sekta ya Kilimo, nataka nishauri jambo; kwenye vijihi, kwenye kata ndiko shughuli za kilimo zinakofanyika, lakini Maafisa Ugani, wataalam wa kilimo kule ni wachache sana. Kuna kata moja

Mheshimiwa mmoja alizungumza hapa ina barabara ya umbali zaidi ya kilomita 250, kata moja ina vijiji 16, hivi kweli kama una Afisa Ugani mmoja anawezaje kuwa *effective* kutekeleza shughuli za ugani kwenye kata kubwa kama hii? Ni ushauri wetu kweli kama tunataka kilimo kileté tija tuwe na vijana wanaojua eneo lao la kilimo, lakini tuwapeleke kule kilimo kinakotekelezwa hasa vijijini vinginevyo tutakuwa bado tuna changamoto tukidhani tutaongeza tija kwenye kilimo, lakini kisifanye hivyo kwa sababu ya uhaba wa wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ugharamiaji wa Mpango, nadhani wadau wanaotajwa na Serikali ni wengi sana, lakini utaona kuna *future* tutafanya hivi, litatokea hivi, nilidhani kwa vile Mpango unaanza 2021/2022 mpaka 2025/2026 hizi *engagement* zote zimeshafika, vinginevyo itafika Julai tutatumia muda mrefu sana ku-*engage* hawa wadau wote, halafu utekelezaji sjui utakuja kuanza lini. Kwa vile kuna dalili za kuchelewa, ni ushauri kwamba sasa Serikali ifanye haraka ku-*engage* na hizi Taasisi za Serikali, Taasisi Zisizo za Kiserikali, Wadau wa Maendeleo na kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwenye kuianisha mifumo ya Serikali na ya sekta binafsi; unajua kwenye Serikali kuna urasimu, kuna *junior officer* anaanda dokezo *senior officer* analipokea, Mkurugenzi Msaidizi anaweka *comments*, Mkurugenzi halafu liende kwa Katibu Mkuu, wakati mwingine inaweza ikachukua hata mwezi kufikia uamuzi, lakini kwenye sekta binafsi vitu vinaenda haraka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni maoni yangu kwamba pengine katika usimamizi wa Mpango huu kuwe na mfumo wa tofauti, tukifuata huu mfumo wa Serikali wa madokezo kupita kwa watu saba kabla ya uamuzi, tunaweza tukajikuta tumechelewa kutekeleza Mpango wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, kengele imeshagonga.

**MHE. JUMANNE A. SAGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Humphrey Polepole, atafuatiwa na Mheshimiwa Oliver Semuguruka na Mheshimiwa Jesca Kishoa ajiandae.

**MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuungana na wenzangu kuchangia Mpango huu Maendeleo kwa Miaka Mitano kwa kuanza na kuainisha kazi nzuri ambayo imefanyika katika Mpango wa Pili chini ya uongozi wa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi na ningetamka mambo mawili muhimu, kazi kubwa imefanyika katika Mpango wa Pili katika kuimarishe uchumi mkubwa na umadhubuti wake (*Macro level economy performance*) ambayo ukifanya vizuri hapo inakwenda kwenye uchumi mdogo unaohusisha watu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kimoja cha kipekee kimefanyika hapa Tanzania ni kufanya haya mambo yote kwa wakati mmoja na nitatoa viashiria vichache kuonesha kwamba katika uchumi mkubwa kazi kubwa sana imefanyika katika Mpango wa Pili na tuna kila sababu ya kuendeleza mafanikio hayo katika Mpango wa Tatu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kiashiria kimoja cha ukuaji wa uchumi na katika uchumi mkubwa na ufanisi wake ni ujenzi; tumefanya ujenzi wa bandari kubwa na ndogo, tumefanya ujenzi wa viwanja vyatundege, tumefanya ujenzi wa barabara kote nchini Tanzania, tumefanya ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa, lakini ukiacha ujenzi imefanyika kazi kubwa sana ya kudhibiti mfumuko wa bei kutoka asilimia tano mpaka asilimia tatu kwa maana ya mfumuko wa bei wa jumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine kubwa imefanyika katika kuimarishe uchumi mkubwa ni kuweka nafuu ya kikodi kwa watumishi katika Pay As You Earn kutoka

12% mpaka 9%. Pia kumepunguzwa kwa kiasi kikubwa sana kwa tozo zenyе kichefuchefu katika eneo la kilimo na madini na hapa ni makumi ya tozo ambazo zimefutwa. Kubwa kuliko yote ni uzalishaji wa umeme usafirishaji na usambazaji na hapa kazi kubwa imefanyika kufikia vijiji vyote na tumbakiza kama 2,000. Hoja ninayojaribu kuisema hapa ni kwamba umeme ambao tumezalisha mpaka sasa hivi tuna ziada, tulianza na *megawatt* 1,300 na sasa tuna 1,600 na hiyo ni ziada ya matumizi ambayo tunayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kwamba, uchumi mkubwa unakwenda sambamba na uwekezaji na katika sekta binafsi na hapa utagundua kwamba mazingira wezeshi tumeyaweka katika kodi ya makampuni (*corporate tax*) ambayo tumeipunguza kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 20 kwa viwanda vinavyohusika na kutengeneza madawa. Hii itawezesha viwanda hapa Tanzania kuanza kutengeneza dawa na kupunguza changamoto ya upatikanaji wa dawa kama ambavyo imepatikana wakati mwininge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tulinde viwanda vya ndani kwa kuweka sera ambazo zitahakikisha kwamba bidhaa zinazoweza kuzalishwa ndani haziagizwi kutoka nje. Hapa napenda kupongeza uamuzi wa Serikali kuongeza kodi katika kuingiza sukari kutoka asilimia 25 mpaka 35 ili viwanda vya ndani viweze kuzalisha na kuuza sukari hapa nchini. Katika uchumi mkubwa pia utaangalia mzunguko wa fedha, wako watu wanapotisha wakati mwininge, lakini ukweli ni kwamba nikitoa kiashiria kimoja tu ya fedha tu zilizowekeza katika mawakala wa benki kutoka mwaka 2013 mpaka mwaka 2019, mzunguko wa fedha ambazo ameziweka mle ndani ziliikuwa bilioni 28 tu, lakini mwaka 2019, zimefika triliioni tano, hili ni ongezeko kubwa kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa nijielekeze katika ushauri; rai yangu kwa Serikali ni kwamba, tufanye itakavyowezekana, miradi ya uzalishaji wa nishati tuikamilishe kabla Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli hajaenda. Sasa hivi tunatengeneza *Stigler's pale bwawa* la Mwalimu Nyerere, *megawatt* 2,115, hiyo inakwenda tayari. Kwenye hotuba ya

Mheshimiwa Rais ameeleza miradi mingine karibu kumi ambayo itazalisha umeme na kuongeza uzalishaji wa umeme nchini kifani na kwa sababu tunazungumzia *a competitive industry economy*, yaani uchumi shindani wa viwanda, umeme ni kigezo muhimu sana cha kufanikiwa kwa viwanda nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilipokuwa nikisoma Mpango, nimeangalia katika ukurasa wa 129, kiashiria cha Serikali hapa kinasema tunataka tuongeze umeme kutoka 1,600 ya sasa mpaka 4,900. Nikizitoa hapa tutabaki na 3,000 nikitoa 2,100 za *Stigler's* tutabaki na 1,000, aah jamani! Mheshimiwa Rais ameeleza hapa Ruhuji *megawatt* 358, Rumakali *megawatt* 222, Kikonge *megawatt* 300, Mtwara gesi *megawatt* 300, Kinyerezi III na IV *megawatt* 600 na 300 mtawalia; na Somanga Fungu kwa gesi *megawatt* 330. Naishauri Serikali itazame ile miradi *strategic* ya kuzalisha umeme katika hii ambayo Rais ameelekeza ili tusije tukafika 2025 tumechukua ile ambayo kwa hakika haitaweza kutuvusha kwa maana hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nieleze tu katika viwanda na kilimo tujikite kwenye eneo moja kubwa, kutehamisha uunganishaji wa wakulima na masoko. Siku hizi *Alibaba* ni tajiri kwa sababu mtandaoni mtu unaweza kuuza korosho, mahindi na vitu kama hivyo. Nashauri, siku hizi simu hizi za kupangusa kila mtu anazo, lakini pia matumizi ya *USSD code*, inawezekana mkulima akawa na nyanya Ilula, asihangaike kuchukua lori zima kulipeleka Dar es Salaam, akatazama mle ndani akaona kuna soko, Dodoma au Morogoro... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kengele imegonga, basi nitaleta mchango wangu kwa maandishi. Naomba kuunga hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Oliver Semuguruka atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Kishoa na Mheshimiwa Ask. Josephat Gwajima ajiandae.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyezekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, kwanza kabisa, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kusimama tena katika Bunge lako Tukufu. Pili, niwashukuru wa kina mama wa Mkoa wa Kagera kwa kunipigia kura nydingi za kishindo. Tatu, nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa kunipitisha tena kuingia tena Bunge lako Tukufu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, nampongeza Rais wetu wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri anazozidi kuzifanya katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Pia nampongeza Waziri wa Fedha na Mpango kwa kutuwasilishia Mpango ili tuweze kuujadili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, naomba sasa nijielekeze moja kwa moja katika mchango wangu. Nitachangia kuhusu vituo vyta afya na elimu kidogo. Vituo vyetu vyta afya viliivyojengwa sasa hivi ni vyta kisasa kabisa, vina *maternity ward, theatre, maabara, mortuary* na nyumba ya daktarin. Hata hivyo, changamoto iliyopo hakuna wodi ya wanaume wala wanawake. Kwa hiyo, naomba Serikali Tukufu waweze kujenga wodi za kina baba na kina mama kwa ajili ya kusaidia wale wananchi wa hali ya chini ili wakifika pale waweze kupata *first aid*, labda wanawenza kupata *drip* wakapumzishwa pale kabla hawajaenda kwenye vituo vikubwa vyta afya. Kwa hiyo, naomba Serikali yangu Tukufu iweke mpango mzuri wa kujenga hizo wodi za kina baba na kina mama. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, moja kwa moja nijielekeze katika suala zima la elimu. Nashukuru Serikali yangu Tukufu imetelekeza vizuri Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa suala la elimu, kuanzia darasa la kwanza hadi *form four* elimu ni bure. Hata hivyo, mwanafunzi wa hali ya chini akimaliza

*form four, form five na six* kama amefaulu vizuri hawezi kwenda shule. Kwa hiyo, naomba Serikali yetu Tukufu kwa sababu imeshajitoa yaani hapo imekula ng'ombe mzima bado mkia, iweze kuangalia watoto wetu waweze kufika mpaka *form six* kwa elimu bure kwa sababu akishaingia chuo kikuu anapata mkopo. Kwa hiyo, naomba Serikali yangu Tukufu iliangularie hilo kwa ajili ya kuokoa kizazi chetu na watoto maskini kama Rais wetu wa wanyonge anavyosaidia. Kwa hiyo, naomba aendelee kusaidia hawa watoto waweze kusoma vizuri mpaka *form six* ili waweze kuingia chuo kikuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze pia kwenye miundombinu ya barabara. Kule kijjini kwetu miundombinu siyo mizuri, unakuta hakuna barabara, mkulima ameshalima mazao yake ili aweze kuyafikisha kwenye soko barabara ni changamoto kubwa sana. Kwa hiyo, naomba Serikali yangu Tukufu isiangalie barabara kuu tu iangalie na Kisingimbi kwetu kule vijjini waweze kuweka barabara Rafiki, mkulima akimaliza mazao yake mazuri aweze kufika katika masoko kuuza mazao yake ili kujkwamua kiuchumi aweze kusaidia na familia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa ni hayo, nashukuru san ana naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca Kishoa atafuatiwa na Mheshimiwa Ask. Josephat Gwajima, Mheshimiwa Agness Hokororo ajiandae.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Natambua tunajadili Mpango huu wakati dunia inapita kwenye mtikisiko mkubwa wa *COVID-19*. Nimeangalia ripoti ya *World Bank*, ukuaji wa kibashara kidunia ulikuwa umeshakua mpaka kufikia asilimia 64 lakini baada ya *COVID-19*, biashara ya dunia ime-*drop* mpaka asilimia 37 ya pato la dunia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema haya, nataka niiombe Serikali, kwa sababu wataalam wa kiuchumi wamefananisha anguko hili na lilitotokea wakati wa Vita ya

Pili ya Dunia, nataka tunapojadili hotuba hii ya Mpango basi tuonyeshe *reflection* kubwa sana na gonywa hili la *COVID-19* ili tuweze kuchangia ndani ya changamoto hii tusiwe tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kutekeleza Mpango tunahitaji fedha ya kutosha. Nimeona Mheshimiwa Mpango na baadhi ya Wabunge wakitoa malalamiko kwa namna ambavyo kumekuwa na malalamiko makubwa sana kwenye ukusanyaji wa kodi, tunahitaji fedha ili kuweza kutekeleza Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujiulize ni kwa nini tunakusanya kiasi kidogo cha kodi ukilinganisha na nchi nyingine nyingi lakini pia kuna kilio kikubwa kuhusu mzigo wa kodi. Tanzania tunakusanya kodi asilimia 13 ya pato la Taifa. Nimefanya *research* kidogo Lesotho wanakusanya asilimia 29 ya pato la Taifa; Kenya wanakusanya asilimia 20 ya pato la Taifa; *South Africa* wanakusanya asilimia 28 ya pato la Taifa; ukienda Burkina Faso wanakusanya asilimia 18 ya pato la Taifa; Namibia asilimia 30; Zimbabwe asilimia 21.1; Mozambique asilimia 23 na Zambia asilimia 15.2. Tanzania tunakusanya asilimia 13 ya pato la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini sababu? Hii inathibitisha kuna udhaifu mkubwa sana kwenye sayansi ya kukusanya kodi. Namwomba Mheshimiwa Mpango anapokuja kuhitimisha hapa atuambie ni kwa nini kuna malalamiko na kelele nyingi kwenye ukusanyaji wa kodi na wakati tunakusanya asilimia 13 tu ya pato la Taifa ukilinganisha na nchi nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa njielekeze kwenye hoja yangu ya msingi kabisa ya zao la alizeti. Kuhusiana na kilimo cha zao la alizeti kama nchi tunatia kichefuchefu. Naomba niseme hivi, kuna mtu mmoja aliwahi kusema Afrika miujiza haitakuja kufika mwisho na mimi ninaungana naye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia zaidi ya asilimia 60 ya ardhi inayofaa kwa kilimo duniani inapatikana Afrika

lakini kila mwaka Afrika tunatoa zaidi ya dola bilioni 27 tunaangiza vyakula kutoka nje. Kwenye muujiza huu, Tanzania hatuko nyuma, kila mwaka nchi ya Tanzania tunaagiza mafuta zaidi ya dola milioni 280. Tunatumia wastani wa dola milioni 280 kuagiza mafuta ya kula kwa pesa za kigeni badala ya pesa za kigeni kuingia ndani kupitia zao la alizeti kwa kuuza mafuta, tunatumia fedha za kigeni kuagiza mafuta kutoka nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya *study* ndogo sana kwenye zao la alizeti ambalo limekuwa *recognized* na *WHO* kwamba ni zao linalotoa mafuta bora kabisa, inaonyesha kwamba karibu nusu ya eneo la Tanzania linafaa kwa ajili ya zao la alizeti. Mfano, Simiyu, Shinyanga, Singida, Iringa, Morogoro na kwingineko wanaweza kulima alizeti. Cha ajabu tunazalisha tani laki nane peke yake kwenye zao la alizeti, kiasi hiki hakifiki hata 0.1 *percent* ya kiasi cha mbegu za alizeti kinachozaliwa dunia nzima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka nitoe mfano wa nchi kama Ukraine, nchi ambayo inaongoza kwa kilimo cha alizeti na uzalishaji wa mafuta. Nchi ya Ukraine inazalisha takribani tani millioni 16.5 kwa mwaka lakini wanalima kwenye *square meter* za mraba 20,000. Ukisema *square meter* za mraba 20,000 ni sawasawa na nusu ya Mkoa wa Singida maana Mkoa wa Singida ni *square meter* za mraba 48,000. Sisi Tanzania tunauza mafuta, kahawa, chai, almasi, tunapata dola bilioni 5 kwa mwaka na wakati Ukraine hiyo dola bilioni tano wameipata kwa kuuza mafuta ya alizeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka nimalizie, kama Ukraine wanafanikiwa, kama Ukraine wanaweza kulima zao hili na kupata manufaa sisi tunashindwa nini? Namwomba Waziri wa Viwanda na Biashara, Waziri wa Uwekezaji, Waziri wa Kilimo hebu wakae chini na kutafakari, umizeni vichwa acheni kumbwelambwela.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia galoni ya lita tano ya mafuta ya kula inauzwa Sh.28,000, wananchi wanalia, wananchi wanateseka. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kidogo niwape *solution*, nataka niwasaidie hawa...

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha, ahsante sana Mheshimiwa Jesca Kishoa. (*Makofii*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Josephat Gwajima atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mheshimiwa Muhamamy Mkenge ajiandae.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pasipo kifani kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao umewakilishwa na Waziri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa mama Kilango Malecela leo alikuwa anachangia nikamwomba aniazime dakika zake tano na akakubali. Sasa kama wewe itakupendeza basi niunganishe dakika tano za Mheshimiwa mama Malecela na za kwangu nipate dakika kumi ili niweze kutoa nilichonacho. Nimezungumza naye akasema anachangia na akaniruhusu lakini nikasema nikipata ruhusa yako na hekima yako itapendeza sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gwajima, hiyo hairusiwi, Wabunge huwa hawapeani muda lakini muda wako sasa unazidi kwenda kwa hayo maombi ambayo yamechukua muda kidogo, tafadhali anza kuchangia. (*Makofii/Kicheko*)

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno machache sana kwa sababu ya muda wangu, kuna hoja zinazungumzwa hapa kuonyesha kana kwamba awamu ya Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli hajafanya jambo lolote. Mtu yejote ambaye haoni kwamba miaka mitano ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli hajafanya chochote basi anaweza kuwa na ugonjwa hatari sana ambao hauwezi kutibika hapa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua fika kwamba kuanzia mwaka 1976 mpaka 1981, Tanzania ilikuwa na ndege *almost* 11 na mpaka tunafika kwenye ubinafsishaji tulikuwa na ndege 9 na mpaka Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli anaingia madarakani tukawa hatuna ndege. Hata hivyo, tangu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ameingia madarakani tuna ndege zinaelekea 12 sasa. Asiyeona hayo ana ugonjwa *special*/unahitaji daktari *special*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unakumbuka vizuri Shirika la *TANESCO*, kabla ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli hajaingia madarakani lilikuwa linaendeshwa kwa kupewa ruzuku shilingi bilioni 438 kila mwaka, lakini tangu 2015 Shirika la *TANESCO* linajientesha kwa fedha yake lenyewe na linafanya vizuri sana. Asiyeona ana ugonjwa maalum unahitaji daktari maalum. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hivyo tu, mwaka 2015 Tanzania yote ilikuwa na vijiji 2,018 vilivyokuwa na umeme lakini leo ndani ya miaka mitano vijiji 10,263 vina umeme katika nchi ya Tanzania. Kwa taarifa ya asiyeona ni kwamba vimebaki vijiji 2,005 tu Tanzania yote iwe na umeme. Pamoja na mambo mengine yote lakini mwenye macho ni muhimu aone kitu gani kimefanyika na wapi tunaelekea kwa sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanassema msiongelee sana *Stigler's Gorge* ni ileile, sikiliza nikwambie

tangu Tanzania ianze ina *megawatt* za umeme 1,602, hii ni tangu Mwalimu Nyerere, Mheshimiwa Mwinyi, Mheshimiwa Mkapa na Mheshimiwa JK Kikwete, utaachaje kuongelea *Stigler's Gorge* ambao ni mradi mmoja wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ambao umetupa megawatt 2,115. Lazima akili iwe likizo au ina matatizo maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hebu tuseme ukweli, mimi nimekuwa Japan, wao wana treni inakwenda kwa *speed 250* na wana nyngine ambayo watazindua mwaka ujao inayotembea chini ya ardhi inayokwenda kilomita 500 kwa saa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Tanzania kwa Afrika Mashariki tumekuwa nchi ya kwanza kutekeleza mradi wa treni yenye uwezo wa kwenda kilomita 160 kwa saa. Utasemaje Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli hajafanya vitu vyake? Unahitaji dawa maalum na daktari maalum kusema hivyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haitoshi, hebu tuangalie ukweli, wakati Mheshimiwa Dkt. Pombe Magufuli anaingia madarakani tunaambiwa tembo wa Tanzania walikuwa wamebaki 15,000, leo kwa taarifa ya Wizara ya Maliasili tuna tembo 60,000. Kwa utawala wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli mpaka tembo wanaanza kuzaana bila utaratibu. Huwezi kusema Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli hajafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa mfano afya, nagusia kila mahali kwa sababu muda wangu haunitoshi, tangu Uhuru tumekuwa na Hospitali za Wilaya 77 lakini miaka mitano ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli tumejenga Hospitali zingine za Wilaya 102. Utabezaje hizo juhud? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haraka haraka tulikuwa na Hospitali za Rufaa za Mikoa 18 tu tangu Uhuru ndani ya miaka tano zimejengwa mpya 10. Asiyeona ana ugonjwa unaitwa *Schizophrenia*.

## **T A R I F A**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gwajima, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namsubiri. (*Kicheko*)

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda tu nimpe taarifa anayenisubiri, kwanza hapa tunachangia Mpango kushauri Serikali, tunavyosema Mpango haujatekelezeka hatumaanishi kwamba Mheshimiwa Dkt. Magufuli wa Awamu ya Tano hajafanya kitu. Mfano kwenye umeme alipotaja *target* tuliojiwekea mpaka 2021 ilikuwa tufikie *megawatt* 4,915 lakini mpaka sasa hivi tuna *megawatt* 1,601 wakati mwaka 2014/2015 ilikuwa ni *megawatt* 1,501. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukisema kwamba wanaweka *target* na hazifikiwi siyo kwamba tunasema hakijafanyika kitu lakini wanavyoweka viashiria basi viweze kufikiwa angalua kwa asilimia 80. Asipambe bali ashauri ili Serikali ifanyie kazi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Matiko. Mheshimiwa kabla sijakuuliza kama unapokea taarifa, nadhani tuwe tunaelewana vizuri, mtu anayegoma kutambua kilichofanyika na mtu anayetambua kilichofanyika lakini anatoa ushauri wa nini kifanyike zaidi kuna tofauti kati ya hayo mambo mawili. Mheshimiwa Gwajima unapokea taarifa hiyo? (*Makofii*)

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimwambie msomi ye yeyote kabla hajaenda mbele ana-referkwanza kule alipotoka. Mimi nime-referkwanza alipotoka Mheshimiwa Dkt. Magufuli na Mpango uliowekwa na Waziri wa Magufuli Mheshimiwa Dkt. Mpango wa kule tunapoelekea. Kwa hiyo, taarifa yake haina maana yoyote kwangu, naomba niendele Mheshimiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye vituo vya afya tangu Uhuru tulikuwa na vituo vya afya 535 lakini ndani ya miaka mitano tumejenga vituo vya afya 487. Kama hiyo haitoshi tangu uhuru tulikuwa na zahanati 4,554 lakini ndani ya miaka mitano tumejenga zahanati mpya 1,998.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme jambo moja kwamba haya yote niliyoyasema hayamaanishi kwamba tusitekeleze Mpango mpya uliowekwa mbele yetu. Nataka kila mtu afahamu kuna ugonjwa wa *COVID-19* amba ni ugonjwa umetikisa dunia na nchi yetu imechukuwa msimamo tofauti na nchi nyingine zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge nataka kutumia nafasi hii kuwatia moyo; msilogope. Msilogope mnapoambiwa kwamba kuna *phase* ya pili ya *COVID-19*. Kilicho na nguvu nyuma ya *COVID-19* ni woga ultiotengenezwa juu ya *COVID-19; the fear over COVID-19 is even more powerful than COVID-19 itself.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wote na watu wote tushinde woga, tusiogope, tumeshinda, tusonge mbele. Msimamo wetu wa kutokuchanjwa na msimamo wetu wa kutokufanya *social distancing* ni msimamo sahihi na utatufikisha mahali sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha mwisho, watu wengi wanazungumza kusahau tulikotoka wakifikiri historia *when you don't remember where you are coming from, you are bound to make mistakes where you are going thinking you are doing development, but you may do the same because you don't know where you are coming from.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu kule nyuma ilikuwa na miradi ya wachimba madini. Tulikuwa tunapewa *royalties* peke yake, nchi yetu ilikuwa inapata *royalties* peke yake ya makampuni ya madini. Sasa hivi Mheshimiwa Rais amesukuma tunapata *almost* asilimia 50 na Tanzania ni wamiliki wenza wa madini yanayochimbwa na kampuni za madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Shukrani sana. Mheshimiwa Agnes Hokororo, atafuatiwa na Mheshimiwa Muharamy Mkenge na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota ajiandae.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa ni mara ya kwanza nianze kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia uzima. Pili, nitumie fursa hii kuwashukuru sana akina mama wa Mkoa wa Mtwara ambao wameniwezesha kurudi katika Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais wetu mpendwa, jemedari bingwa, Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa katika maeneo yote; miundombinu, maji, elimu, afya na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa. Mojawapo ya nguzo ya mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa kama ilivyoainishwa kwenye Mpango huo ni ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu.

Naiomba sana Serikali yetu Tukufu, ili kuwajumuisha wananchi wa Kanda ya Kusini, ni muhimu sana Mpango huu wa miaka mitano ukaingiza ujenzi wa reli ya Kusini. Kwa nini naiomba hii? Ujenzi wa reli ya Kusini ulitokana na Mradi wa *Mtwara Corridor* na mradi huu ulisainiwa na nchi nne; Tanzania, Msumbiji, Malawi na Zambia. Ulisainiwa mwaka 2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muasisi wake ni hayati mpendwa wetu Rais Mkapa. Lengo lake lilikuwa kuiwezesha Bandari ya Mtwara. Bandari ya Mtwara imejengwa kwa bilioni 157 lakini juzi swali liliulizwa hapa na Waziri alikiri kwamba Bandari ya Mtwara kwa sasa inafanya kazi chini ya kiwango.

Kumbe mradi huu wa Reli ya Kusini ukitekelezwa ina maana Bandari ya Mtwara itafanya kazi ile iliyokusudiwa kwenye huu mradi na miradi ya *EPZA* ambayo kwa sasa bado haijaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naiomba sana Serikali, kwenye huu Mpango wa miaka mitano ioneshe waziwazi ni lini mradi wa ujenzi wa reli ya Kusini utaanza na kukamilika ili kuwajumuisha wananchi wa Mikoa ya Ukanda wa Kusini katika ukuaji wa uchumi na maendeleo yao. Vinginevyo tutakuwa tu tunaendelea kushangilia lakini wananchi wa Ukanda wa Kusini kama maeneo haya muhimu katika ukuzaji wa nchi yetu hayatajumuishwa na wao watakuwa wanaendelea kushuhudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kabisa kwamba Serikali imeanza kutekeleza sehemu ya Mradi wa *Mtwara Corridor*, kama vile ujenzi wa barabara ya kutoka Mtwara mpaka Mbambabay umetekeliza, lakini pamoja na huo ujenzi wa bandari, pamoja na upanuzi wa uwanja wa ndege, lakini pia pamoja na ujenzi wa Daraja la Umoja lile linalounganisha Tanzania na Msumbiji, lile Daraja la Mtambaswala. Sasa mambo haya yote ambayo Serikali ya Awamu ya Tano na zile zingine imeyatekeleza, hii miradi itaendelea kulala kwa sababu shughuli za kiuchumi zinategemea kwa kiasi kikubwa ujenzi wa mradi wa reli ya Kusini. Naamini Serikali yetu Tukufu itaweza kujumuisha Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kusini ili na sisi tuweze kushiriki kikamilifu katika ile dhana ya uchumi jumuishi, uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nijielekeze katika eneo la kilimo. Kama ambavyo mpango umeainisha kwamba asilimia 65 ya Watanzania wanapata riziki yao kwa kutegemea shughuli za kilimo. Lakini tunaona shughuli za kilimo zinachangia asilimia 27 tu ya *GDP* na asilimia 24 ya *total export*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kinahitajika katika eneo hili; kwa kuwa wananchi wa Mikoa ya Kusini, hasa Mtwara, asilimia 98 ni wakulima, ili tujumuike pia katika ujenzi wa uchumi huu ambao wote tunauhitaji, naomba sana tujikite

katika mapinduzi ya kiteknolojia. Wakulima wetu kwa sasa wanatumia jembe la mkono; kwa nini? Trekta ziko bei juu, milioni 45 mpaka milioni 60. Akinamama ambaao wanashiriki kwa asilimia 75 kule mashambani na katika shughuli za kilimo hawawezi kununua trekta, mikopo yetu ya vikundi vyatya halmashauri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Kengele imeshagonga.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Shukrani sana. Mheshimiwa Muhamramy Mkenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Chikota na Mheshimiwa Rehema Migilla ajiandae.

**MHE. MUHAMRAMY S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kupata nafasi hii. Napenda pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema hadi kufikia siku ya leo. Napenda pia niwashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Bagamoyo kwa kunipa heshima kubwa ya kuwa hapa leo. Pia napenda niwashukuru familia yangu, ndugu zangu na jamaa zangu kwa kuni-*support* hadi nimefikia hatua hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika Mpango. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango amewasilisha Mpango wake; kwa kweli kabisa ni mpango mmoja ambaao ni mzuri sana, kama jina lake liliivo Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niguse katika suala zima la kilimo. Katika mpango nataka nijikite zaidi katika kilimo cha umwagiliaji. Serikali katika hotuba yake ya Mpango imezungumza kwamba hekta za umwagiliaji ziko 461,378 na ina mpango wa kuongeza hekta hizo hadi kufikia 694,715.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze; pale kwetu Bagamoyo tuna kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Mto Ruvu. Kilimo hiki kinawasaidia watu wengi sana. Si Mto Ruvu pekee, tuna Mto Wami ambao una nafasi kubwa sana katika kuisaidia nchi katika kilimo hiki cha umwagiliaji, kwa sababu mwaka 1966 mwezi Oktoba kulifanyika *study* na kampuni moja ya watu wa Sweden ambayo ilikuwa inafanya kazi ya kufanya utafiti wa mradi wa umeme pamoja na bwawa kubwa sana la umwagiliaji katika Mto Wami ambalo lilitakiwa liwe pale Mandera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali, bwawa hili likitumika katika kilimo cha umwagiliaji maeneo mengi sana ya Bagamoyo pamoja na Mkoa wa Pwani, Kibaha, yanaweza yakapata maji mengi sana kupitia mradi huu kwa sababu ni bwawa ambalo limefanyiwa *studyn* na makaratasni yake yapo, naflkiri hata Wizara inalitambua hilli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nirudi katika suala la wavuvi. Bagamoyo kwetu sisi tunashughulika na uvuvi na kwa bahati nzuri Serikali mwaka huu kupitia jemedari wake, Rais Dkt. John Pombe Magufuli, wameamua kununua meli nane za uvuvi. Nina imani katika meli hizo Bagamoyo inaweza ikapatiwa meli moja; sina shaka na hilo kwa sababu Chuo cha Uvuvi Mbegani ambacho kina wataalam wengi sana wanaojua masuala ya uvuvi tuko nacho pale. Niwashauri ndugu zangu, suala hili la uvuvi tukilishikilia linaweza likatuingizia pesa nyngi sana katika nchi yetu. Kwa sababu mwaka 2015/2016 mauzo yalikuwa dola bilioni 379, mwaka 2019/2020, mauzo yanaonesha yalikuwa dola bilioni 506,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri; pale Bagamoyo pana mradi mmoja wa kufuga jongoo bahari. Hawa jongoo bahari bei yake ni kubwa sana duniani. Hata Waheshimiwa Wabunge mki-google katika hizo *tablets zenu sea cucumber, world price market* ni shilingi ngapi, mtaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri alitembelea pale tulikwenda sehemu ambako wanafugia yale madude. Kilo moja ya jongoo bahari ni

Sh.65,000. Sasa tukielekeza katika miradi kama hii Serikali inaweza ikatupatia pesa nydingi sana na kuhakikisha mipango yetu ya maendeleo itakuwa sawa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, muda umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. MUHARAMY S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mengi, lakini naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, atafuatiwa na Mheshimiwa Rehema Migilla na Mheshimiwa Janejelly James ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu kuhusu hoja ambazo zipo Mezani. Kabla sijaanza kuchangia, nitumie nafasi hii, kwa moyo wa dhati, kuipongeza Serikali yangu ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri ambayo imeifanya katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa nchi yetu. Kwa kweli kazi kubwa imefanyika, miradi mingi imetengenezwa, mingi tumeiona katika maeneo yetu. Changamoto iliyopo kwa pale ambapo haikutekelezwa ndiyo taratibu za mipango. Imeingizwa kwenye Mpango huu wa Tatu ili itafutiwe fedha iendelee kutekelezwa. Kwa hiyo naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu unajikita katika maeneo mawili. Sehemu ya kwanza ni sehemu ya kilimo na hapa nitashauri namna gani ya kupata fedha ili tuendelee kutengeneza miradi mingine na itahusu kuongeza thamani kwenye mazao ya biashara na hususan zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ubanguaji ndiyo njia pekee ya kuhakikisha kwamba korosho yetu inapata bei nzuri

kwenye soko la dunia. Kubangua korosho ni mkakati ambao tulishauanza hapo nyuma. Lengo la kuweka *export levy* ilikuwa ni kuwazuia wanunuzi wasisafirishe korosho ghafi, lakini mpango huo naona kama una dosari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wetu wa kubangua korosho kwa viwanda tulivyonavyo ni kama tani 70,000 na sasa hivi tunazalisha mpaka tani 220,000. Kwa hiyo korosho nyingi tunaziwa zikiwa ghafi. Nashauri kwamba tukose fedha kidogo leo ili tupate fedha nyingi baadaye na hii itawezekana kwa kufanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuondoe tozo na kodi zilizopo wakati wa uingizaji wa mashine za kubangua korosho. Wawekezaji wanalamika kwamba kodi ni kubwa kwa hiyo tuondoe hizo kodi ili mashine nyingi ziweze kuingizwa.

Pili, nashauri, tuweke vivutio maalum kwa wawekezaji wapya wa viwanda vya korosho. Ushauri wangu wa tatu, tuondoe kodi na tozo kwenye vifungashio. Wale ambao wana viwanda sasa hivi wanalamika kwamba vifungashio vina kodi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo faida yake hapa ni nini? Faida ya kwanza ni kwamba tutapunguza gharama za uwekezaji, kwa hiyo tutapata wawekezaji wengi; Pili, tutawapata wawekezaji wa ndani badala ya kuwategemea wawekezaji wa nje tu; na tatu, tutapata wawekezaji au wabanguaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kidogo cha korosho unaweza ukatumia mtaji wa milioni 60. Kwa hiyo kwa sababu sasa hivi korosho inalimwa na zaidi ya mikoa 12, tunaweza tukatumia halmashauri zetu badala ya kutoa zile fedha za Mfuko wa Vijana kwa vijana mmoja mmoja, tunaweza tukaamua waanzishe viwanda vidogo vidogo vya kubangua korosho. Hapo tutaongeza ajira kwa vijana wetu, tutaongeza ajira kwa wanawake na utakuta thamani ya fedha ile tutakuwa tunaiona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Vietnam na India wanatumia sana korosho yetu kuongeza ajira kwao. Mipango hii wakiisiklia wenzetu watakuwa na hofu sana kwa sababu korosho ghafi hazitakwenda kwao.

Kwa hiyo muda ni sasa tuwekeze katika ubanguaji ili tuongeze ajira. Naona kabisa tukiwekeza kwenye korosho hizi ajira milioni nane ambazo tumeahidi kwenye llani ya chama chetu karibu robo yake zitatoka kwenye viwanda vya kubangua korosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili, niungane na Mheshimiwa Hokororo kuhusu Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na ule wa Chuma Liganga. Ukiangalia Mipango yetu yote mitatu ile inaendelea kutajwa. Wakati umefika sasa tuweke fedha za kutosha ili miradi hii iende kutekelezwa. Mradi huu unakwenda sambamba na ujenzi wa relli kutoka Mtwara – Mbambabay na ile pacha ya Mchuchuma na Liganga. Tuwekeze katika miradi hii sasa ili tuweze kupata fedha za kutosha. Tukiwekeza kwenye reli hii ya Kusini basi Bandari ya Mtwara itatumika ipasavyo na siyo kama malalamiko yaliyopo sasa hivi kwamba inategemea zao la korosho, tutasafirisha tumbaku kutoka kwa wenzetu Songea lakini Malawi, Zambia na DRC Kongo wanatumia bandari yetu na hivyo tutapata kodi nyngi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rehema Migilla, atafuatiwa na Mheshimiwa Janejelly James na Mheshimiwa Joseph Tadayo ajiandae.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi nami nichangie Mpango ulioko mbele yetu. Kwanza, niungane na waliotangulia kuchangia Mpango huu wa maendeleo ambao dhima yake kubwa ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wowote hauwezi kufanikiwa endapo maeneo fulani hayatapewa kipaumbele. Nitaanza na eneo la kilimo. Asilimia kubwa ya wananchi wa Tanzania wanashiriki kwa kiasi kikubwa katika shughuli za kilimo lakini kilimo hiki sasa hivi badala ya kuwa uti wa mgongo kinakuwa ni kiua mgongo cha wananchi walio wengi, hasa wa maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu, kilimo sasa hivi hakina tija kwa wakulima wetu badala yake kimekuwa kinaleta dhiki kwa hawa wakulima wetu na hatimaye kuwasababishia kukata tamaa. Hivyo, niiombe na kuishauri Serikali, kama kweli tuna nia ya dhati ya kufikia malengo yaliyokusudiwa katika mpango huu, basi Sekta hii ya Kilimo ipewe kipaumbele hasa kwa kuiongezea bajeti. Pia masoko kwa ajili ya bidhaa za wakulima wetu yapatikane na yawe na bei elekezi illi hawa wananchi wetu waweze kuwa na uhakika wa kuza mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la bima ya kilimo; suala hili kama halitapewa kipaumbele wananchi wetu watakuwa na uhakika hata kama yatatokea mabadiliko ya hali ya hewa, basi watakuwa na uhakika wa kufidiwa endapo matatizo ya kijigrafia yanaweza yanatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kwenye kilimo ni suala la kuanzisha hizi *block farming* ambazo kwa kiasi kikubwa zitakuwa zina tija kwa hawa wananchi wetu kwani asilimia kubwa ya maeneo yaliyopo Tanzania hayalimwi kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, kama tutaanzisha hizi *block farming*, nina uhakika kabisa wananchi watalima kwa eneo kubwa na pia watakuwa na uhakika wa masoko ya mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni uhakika wa pembejeo kufika kwa wakati na kuwezesha mazao ambayo yako kwenye ushindani katika Soko la Dunia. Mfano kwenye maeneo yetu, mazao kama tumbaku, chikichi na korosho, ni mazao ambayo yanaweza yakahimili udongo kwenye maeneo yetu. Hivyo, naomba mazao haya sasa yawekewe

umuhimu mkubwa na wananchi waweze kuelimishwa juu ya kulima mazao haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala lingine la *TARURA*. Hatuwezi kuwa na uchumi wa viwanda endapo tu uhakika wa kusafirisha mazao yetu hautakuwepo kutokana na barabara nyingi kuwa mbovu. Barabara nyingi sana ambazo ndiyo zinalisha barabara kubwa ni mbovu na hazipitiki. Hivi mfano ninavyoongea mimi barabara yangu ya kutoka Mnange - Uliyanhulu, Urambo - Uliyanhulu, Uliyanhulu – Tabora ambazo zinapitisha bidhaa nyingi sana, ni mbovu na hazipitiki. Naomba *TARURA* iongezewe bajeti kwani bajeti inayowekwa ni ndogo sana ukilinganisha na mtandao wa barabara unaohudumiwa na *TARURA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naziomba Halmashauri na ikiwezekana zilazimishwe, ziweze kuwa na vitendea kazi; mitambo ya kutendea kazi kama *excavator*, magreda na kadhalika. Vifaa hivi vikiwepo Halmashauri zetu zitakuwa na uwezo wa kufanya matengenezo ya barabara zetu pindi inapotokea uharibifu wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, nafikiria kuna haja sasa ya kufanya mabadiliko kwenye bajeti ya *TARURA* ya *TANROADS*. Haiwezekani kila mwaka tutegemee bajeti hiyo hiyo ya *TARURA* ya asilimia 30 na *TANROADS* asilimia 70. Naomba kama kutakuwa na *demand* na kwa wakati huo, basi pawepo na mabadiliko. Kama *demand* itakuwa ni kubwa kwa wakati huo, *TARURA* iweze kuongezewa bajeti kuliko mtindo uliopo sasa hivi wa kutegemea bajeti hiyo hiyo tu kila mwaka bila kuangalia kwamba mahitaji yanabadilika kulingana na wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la ukusanyaji wa mapato. Katika Mpango huu kilicholeta mtafaruku mpaka changamoto hizi zitokee na Mpango usifanikiwe inavyotakiwa ni kukosekana kwa mapato kwa wakati na yanayotosheleza. Hivyo, naomba sasa Halmashauri na Serikali ziweze kubuni vyanzo vingine vya mapato ambavyo ni vikubwa kuliko kutegemea vyanzo vidogo vidogo. Leo Serikali

inategemea vyanzo vidogo vya mapato hali ambavyo inasababisha mapato yasipatikane. Pia ni kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa kutumia watu wenyewe utaalami kuliko *task force*, kazi yao ni ku-force tu watu na kusababisha utoroshaji wa mapato kwa njia ambazo siyo stahiki.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Haya, shukurani. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Janejelly James, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Tadayo na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ajiandae.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uweza wa kusimama hapa. Nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alivyojipambanua kwamba yeye maendeleo kwake hayana itikadi za kivyma. Kama angefuata itikadi za vyama maendeleo tunayoyasema Dar es Salaam yasingekuwepo. Dar es Salaam tunajua fika ilikuwa ni ngome ya wapinzani lakini amefanya maendeleo ya barabara, maji, elimu iliyopelekea wananchi wa Dar es Salaam sasa nao kumlipa fadhila ya kuifanya Dar es Saalaam ya kijani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru na nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mpango, amekuja na Mpango kwelikweli kama jina lake. Hata hivyo, Mpango huu wanaohusika ni wataalam wake ambao ni rasilimali watu. Mimi nijikite kwenye rasilimali watu. Haya yote tunayoongea humu, yote tunayojadili humu, wanaoenda kuyatekeleza ni rasilimali watu, ni watumishi wetu, lakini kuna sehemu hawa watumishi hawatoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Waheshimiwa Wabunge wamesema kuhusu kilimo, lakini ukiangalia nchi ina *shortage* ya Maafisa Ugani 6,000 badala ya 12,000. Sasa hawa 6,000 hawawezi kutumika kwa nchi kumfikia kila mkulima, suala hili tuliangalie kwa makini. Hata hao waliopo vitendea kazi walivyonyayo ni vichache sana. Tumesikia kuna Kata zina vijiji 15, lakini Afisa Ugani huyu hata baiskeli hana, atamfikiaje huyu mkulima? Kama kweli tunataka kilimo kiwe ni uti wa mgongo, tuwaangalie hawa Maafisa Wagani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajivunia *GePG* ambapo mtandao uliotengenezwa na watumishi wetu wa Serikali. Hii ni *software* tungkuwa tunainunua kwa wataalam wengine ingetumia bilioni za fedha. Kwa hiyo, tuwaendeleze hawa watumishi wetu kielimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi imefikia wakati watumishi wanaogopa kwenda kusoma kwa sababu ya nyaraka zinazotoka utumishi. Mtumishi sasa hivi akienda kusoma, anaambiwa muda wake alioenda shule hautahesabiwa kwenye *promotion* yake. Sasa tunaenda kuzalisha wale walioenda kusoma na aliyebakika akaendelea na ule muundo anakuwa mwandamizi, yule aliyetoka na elimu yake anakuwa *junior* kwake. Sasa hii inapunguza utendaji kazi ndani ya Serikali. Huyu mwenye elimu kubwa angemshauri huyu lakini sasa huyu ni mwandamizi kwake, atamshaurije na huyu ni *senior* wake? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utumishi niwaombe, tuangalie hizi nyaraka. Kuna sheria za kiutumishi, lakini nyaraka ndani ya sheria za kiutumishi zimekuwa nydingi mno, zinaleta mkanganyiko. Sasa hivi mtumishi ukimwambia nenda kasome ataleta sababu zisizo na msingi, lakini ukimfikia kwa karibu anakwambia ngoja kwanza nipande kwenye huu muundo nifikie daraja la uandamizi ndiyo nitaenda kusoma lakini sasa wanadumaa na utaalam unabadiilika kila wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuiangalia hii miundo, tutabaki tunawalaumu wataalam hawafanyi kazi lakini kumbe kuna kitu kimewakwamisha. Naomba tuliangalie hili

kwa umakini. Tuna vijana ambao ni wazalendo wa kweli. Mfano ni hii Wizara ya Fedha ambayo imekuja na huu Mpango, wanakesha, wanaumiza vichwa kuja na Mpango kama huu, lakini sasa miundo inawakamata. Tuliangalie suala hili na kama tunataka nchi hii iendelee, tuwekeze kwenye rasilimali watu. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ana utashi kabisa wa kuwekeza kwenye rasilimali watu. Ukiangalia llani ya Uchaguzi imesema hivyo; ukiangalia hotuba yake hapa imesema hivyo; Mpango umekuja unasema hivyo, lakini je, tuatekeleza sisi tunaomsaidia? Nizidi kuiomba Menejimenti ya Utumishi wa Umma, hebu angalieni nyaraka zenu za kiutumishi, zimekwamisha kabisa haya maendeleo na huu Mpango wanaoenda kuutekeleza ni rasilimali watu hii hii. Tukiyafanya hayo, Tanzania inaenda kubadilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Tadayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa na Mheshimiwa Neema Lugangira ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia Mpango huu. Nianze kwanza kuipongeza Serikali yetu chini ya Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa ajili ya kutuletea Mpango huu mzuri. Naipongeza pia Wizara kwa kazi nzuri ambayo wamefanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nilikuwa nasoma *journal* moja ambayo imeandikwa na *Royal Irish Academy* ikizungumzia juu ya vyama vikongwe kubakia madarakani. Walifanya uchambuzi mzuri sana, walipofika kwenye CCM wakaeleza kwamba CCM ipo madarakani na ina uwezo wa kuendelea kuwa madarakani kwa sababu baada ya uchaguzi huwa wana-stick kwenye kutekeleza llani, hawafanyi *manipulations* na kufanya mambo mengine mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nasoma Mpango huu, kikubwa nilichokuwa najaribu kukitazama ni hicho kwamba umeendana vipi na llani yetu? Mimi nimeridhika kabisa kwamba Mpango ulioletwa uko sambamba na llani na kwa hiyo, kama ilivyo kawaida kwamba kwenye Mfumo wa Vyama Vingi, chama kinachoshinda kwenye uchaguzi llani yake inageuka kuwa sera, basi tuungane kwa pamoja tutekeleze Mpango huu, tuutungie sheria, bajeti ikija tupitishe mafungu tukatekeleze kwa pamoja na kwa umoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri tu mambo machache. Suala la kwanza ni elimu. Endapo kweli tutataka kama ambavyo tunataka kwamba vijana wetu washiriki katika uchumi wa viwanda na waweweza kufaidi matunda ya nchi kufikia katika uchumi wa kati, basi suala la *VETA* ni lazima tulitilie mkazo sana kama ambavyo imezungumzwa kwenye Mpango. Vipo Vyuo vya *VETA* ambavyo villanzishwa na wananchi kwa kushirikiana na marafiki na wafadhili mbalimbali; kwenye Jimbo langu viko viwili; kuna kimoja kiko Tarafa ya Usangi na kingine kiko Tarafa ya Ugweno, ni muhimu hivi vikafufuliwa viweze kufanya kazi kwa sababu huduma yake bado inahitajika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunahitaji Vyuo vya *VETA* katika kila wilaya ambavyo vitaendena na uchumi wa eneo husika. Kwa mfano, Kanda ya Kaskazini tuko kwenye utalii na madini; basi Vyuo vyetu vya *VETA* viendane na kutengeneza vijana watakaoshiriki kwenye uchumi huo. Halikadhalika, Kanda ya Ziwa kama kuna uvuvi na madini, basi twende hivyo hivyo ili tuhakikishe kweli vyuo vyetu vinawafaidisha vijana wa maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunahitaji kuendelea kutilia mkazo elimu ya juu. Dhana kwamba kwa sasa hivi elimu ya juu imeanza kuwa *irrelevant*, hiyo mimi sikubaliani nayo kabisa, kwa sababu mbili. Kwanza, huwezi kupigana vita ukawa na Askari wa chini peke yao bila Majenerali. Halikadhalika, liko suala kwamba dunia imekuwa kijiji, tunahitaji *ku-export* hata *grains*. Kama tunavyopeleka wachezaji akina Mbwana Samatta wakacheze nje huko, pia

tunahitaji wasomi wetu waende wakafanye kazi za kibingwa huko nje. Wako wengi mpaka sasa hivi ambao wanafanya kazi hiyo, hata waliotoka kwenye Jimbo langu, lakini tunahitaji *succession plan* kwamba hawa wanapostaafu, wapatikane wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutilie mkazo pia elimu ya juu, kwenye Jimbo langu tuna ardhi kubwa sana, kwa hiyo, ninaalika kabisa Serikali ije kuwekeza hata kwenye vyuo vikuu. Tuna ardhi ya kutosha, tufanye kazi hiyo, pamoja na Vyuo vya VETA lakini pia tuendelee kutengeneza akili kubwa kwa ajili ya kuingia kwenye Soko la Dunia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotakiwa ni kwamba wataalam wetu wa elimu watutengenezee mitaala ambayo itawafanya wahitimu wasiabudu vyeti. Kuna nchi jirani tu hapa, kuna kijana ame-*graduate International Relations and Diplomacy* lakini akaenda kuanzisha *car wash*. Sasa ye ye kwa sababu amefikia *level* hiyo, anaenda kwa Mabalozi na Mashirika ya Kimataifa, anasaini mikataba ya kuwaoshea magari, analipwa dola. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijana mwingine atakuja akuambie naomba mtaji wa kuanzisha *car wash* shilingi milioni tano, sijui nitanunua *hooverna* hiki na hiki; akishaanzisha *car wash* anakaa hapo anasubiri wateja wamfuate, ye ye anaongea habari ya Arsenal na nini akisubiri wateja waje, badala ya kwenda kuwagongea mlango. Bora hata angezungumza Simba na Yanga maana ni za kwetu. Kwa upande wa elimu napenda nisema hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo, naungana na wote ambao wamesema kabisa kwamba kilimo ni moja ya vitu ambavyo vitatutoa kiuchumi, lakini lazima twende kwenye kilimo cha umwagililaji. Nchi yetu ina vyanzo vingi sana vya umwagililaji kiasi ambacho hata suala la *greenhouse* linaweza likaja kama *second option*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa sababu kengele imelia, ipo miradi kwa mfano kwenye Jimbo langu, naishukuru Serikali kwamba...

*(Hapa kengele ya pili illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Lugangira na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate ajiandae.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia kwenye Bunge hili la Kumi na Mbili, nianze kwa kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Rufiji kwa kunichagua kwa kishindo na kukomboa Kata zote 13 na kupata ushindi ambao haujapata kutokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango tunaoujadili leo, una mambo makuu matatu. Jambo kubwa la kwanza ni utawala bora; ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu; na uchapa kazi kufikia malengo ya Mpango uliokusudiwa. Hizi siyo ndoto pekee za Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, hizi ziliikuwa ni ndoto za Mwasisi wa Taifa hili, Rais wetu wa Awamu ya Kwanza, ambapo ye ye katika fikra zake aliamua kuziweka fikra zake katika Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiisoma Ibara ya 9 ya Katiba, inazungumza misingi ya kwenda kuwasaidia Watanzania; kumsaidia mwananchi mmoja mmoja na kuondoa umasikini, ujinga na maradhi. Kwa hiyo, haya yote yanayozungumzwa leo na Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli,

yana msingi wake katika Serikali ya Awamu ya Kwanza ya Mwasisi wetu wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Ibara ya 9(e) inazungumzia Watanzania kwenda kufanya kazi. Hili ndiyo jambo kubwa ambalo Mheshimiwa Rais analisisitiza leo kuwataka Watanzania kufanya kazi ili kwenda kutimiza ndoto za Mpango wa Maendeleo ambao tunaukusudia. Haya pia siyo mageni. Mambo haya tayari yana msingi wake, yalianzishwa na Mwalimu Baba wa Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Mpango wa Taifa wa Maendeleo baada ya uhuru uliotolewa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwaka 1964 mpaka mwaka 1969 na Mpango wa Pili wa Maendeleo uliosomwa mwaka 1969 mpaka mwaka 1974, haya yote yalidhamiria kwenda kukomboa Watanzania. Ujenzi wa miundombinu ya barabara, viwanda na mambo mengi makubwa, Mwalimu Nyerere dhamira yake ilikuwa ni kuhakikisha Tanzania yote inafikika. Wakati ule nchi yetu miundombinu ilikuwa ni *square* kilometra 86,000, wakati huo Tanzania ilikuwa na watu milioni 9 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tujulize, changamoto zilizopelekeea ni kwa nini tulishindwa kufikia malengo ambayo Mwalimu aliyakusudia? Hapa tunajikita katika Watafiti wa kiuchumi wanavyosema. Tunaye mtafiti mmoja anaitwa Daron Acemoglu pamoja na James Robinson, katika kitabu chao cha tafiti kilichokuwa kinazungumza ni kwa nini mataifa yanashindwa kuijendeleza, waliwahi kusema: "Mataifa mengi yanashindwa kwa sababu hayana *strong institutions and vigilance*. Hayana taasisi zilizo imara, lakini siyo taasisi kuwa imara peke yake, taasisi ambazo zinaweza kujua changamoto tulizonazo na kesho tutafikia wapi? Kama tutashindwa katikati, njambo gani tutafanya ili tuweze kufika kule tunakotaka kufika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndipo tunapoiangalia bajeti ya Serikali na tunagundua kwamba Bajeti ya Serikali ya 2019/2020 tulikusanya asilimia 92.8, lakini mwaka 2020/2021

makusanyo ni asilimia 88. Ziko sababu nyingi ambazo wachumi wetu, tungekuwa na taasisi imara wangeweza kuntuambia, ni kwa nini tumeshindwa kufikia malengo yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo lilijadiliwa na Bwana Acemoglu, alisema: “*The quality of political and economic institutions.*” Ni lazima tuwe na taasisi za kisiasa zinazozingatia uchumi, lakini pia tuwe na taasisi za kiuchumi ambazo ni imara, zinaweza ku-focus na kujua Tanzania tunataka kwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote lazima tuangalie, bajeti yetu leo hii, dhamira yetu ni kukusanya shilingi trilioni 26, je, Taifa letu tutaweza kukusanya shilingi trilioni 13? Kwa sababu tayari tumepanga shilingi trilioni 10 itumike katika miradi ya maendeleo na fedha hizi lazima zitokane na makusanyo ya ndani, tunawezaje kufika huko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimekuwepo kelele nyingi sana kuhusu chombo chetu cha *TRA* namna kinavyokusanya na namna kinavyoshindwa kuwa imara na kutumia taasisi nyingine. Ili tuweze kufanikiwa yapo mambo mawili lazima tuyafanye. Jambo la kwanza, ni lazima tuzipe *immunity institutions* zetu ili ziweze kujitosheleza, ziwe imara na ziweze kufanya maamuzi kwa niaba ya Watanzania ili tuifikie Tanzania mpya tunayoitaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo Bunge linaweza kufanya ni kuitaka Serikali kuleta mbele ya Bunge lako Tukufu vipaumbele vya Taifa vikionyesha *flagship projects*. Zile *project* zote ambazo ni kubwa na za kimkakati, basi Bunge liiagize Serikali na litoe Azimio la Kibunge ambapo hatatokea mtu yejote kuweza kubadilisha Maazimio ya Bunge ili tuweze kuainisha miradi ya kimkakati, vipaumbele vya Taifa letu na ni wapi tunataka kwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli amefanya vizuri sana, amekuwa na mpango mzuri sana wa kuipeleka Tanzania mbele, lakini hatujui kesho atakuja nani? Kama Bunge likitoa

Azimio na likitungwa mkono na Wabunge zaidi ya robo tatu, kwamba tunataka miradi ya maji ikamilike, tunataka miradi ya mwendokasi wa treni ikamilike, hakuna kiongozi mwingine atakayeweza kuja kubadilisha haya kwa sababu tayari Bunge limeshatoa Azimio. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja hii, lakini tuiombe Serikali kama siyo Bunge hili, Bunge linalokuja, ilete ndani ya Bunge vipaumbele, miradi ya kimkakati ili Bunge tuamue robo tatu ya Wabunge kuikubali. Asije Kiongozi yejote baada ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli kwenda kuipinga miradi hii ya kimkakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MHE. TOUFIQ SALIM TURKY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala* kwa kunijalia kufika hapa, lakini pia kumtakia Rehema mzee wangu aliyeqwishakutangulia mbele ya haki Mheshimiwa Salim Turkey, *Mr. White*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nichukue fursa hii nikishukuru chama changu, Chama cha Mapinduzi kwa kuona ninafaa na kuweza kuwakilisha wananchi wetu wa Jimbo la Mpandae. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nianze na kuunga mkono hoja, kwa kweli Mpango huu ni mpango kazi. Kusema kweli nchi yetu inavyoelekea imetuletea hamasa kubwa mno ndani ya miaka mitano hii. Mheshimiwa Rais wetu kafanya makubwa sana, ile hamasa imekuja mpaka Visiwani. Kwa mara ya kwanza katika historia CCM kushinda kwa asilimia 74 Zanzibar, imeonesha kwa namna gani Awamu ya Tano ilivyofanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la uchumi, nataka kuongelea masuala mawili tu, hatuwezi kuongelea uchumi kama hatuongelei mtaji. Mtaji tukisema inaingia

katika masuala ya ajira, lakini muhimu sana namna gani unaweza kuipata ile *capital*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la ajira tunatafuta ajira milioni 8, namna gani tutazipata hizi ajira? Ni kwa kupitia *private sector* lakini pia watu kuweza kujajiri wenyewe. Tukitizama mabenki yetu wanawapatia mtaji matajiri zaidi kuliko wanyonge, sasa namna gani wale wanyonge wanaweza kupata mtaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuitazame katika taswira mbili; uchumi wa pande hizi mbili uko tofauti, tukifuata uchumi wa Bara uko tofauti na wa Zanzibar. Zanzibar kitu gani tunaweza tukafanya ambacho kinaweza kusaidia kwa pande zote mbili, kupitia Benki Kuu (*Bank of Tanzania*), tunaweza tukaongeza wigo wa kuanzisha *offshore banking*. Hii *off shore banking* itasaidia vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia visiwa vyote vilivyoendelea duniani, mfano Singapore, Dubai, Hongkong, Mauritius, Panama masuala yote wanayofanya ni *offshore banking*, wanahakikisha watu wanaleta fedha ndani ya nchi zao. Sasa zikipatikana zile hela ndipo yale mabenki wanakuwa na *excess funds* za kuweza kuwapatia wajasiriamali wadogowadogo watakuwa na *appetite*. Sasa kwa kwa nini tusianzishe *offshore banking* katika kusaidia uchumi wa Zanzibar lakini BoTikawa ni msimamizi mkuu kupitia *Bank of Tanzania branch* ya Zanzibar? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusu Zanzibar kuendelea katika *real estate*. Uchumi wa visiwa ni fedha na *real estate*, hiyo ndio ukitizama karibu visiwa vyote vilivyoendelea. Sasa tukitizama katika suala la *real estate* kuna changamoto moja kubwa nayo ni suala la *immigration*. Dubai leo ukitaka kununua nyumba zaidi ya milioni 1 Dirham, sawasawa na Dola 270,000 unapatiwa *resident permit* ya miaka mitatu. Leo kuna nyumba ya Dola 600,000 imejengwa pale na Mzee Bahresa, wako wengine wamejenga hata *resident permit* ya mwaka mmoja hupati. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukitizama ule mradi wametumia tayari *almost 150 million dollars*, lakini hauwezi ku-*take off*. Miradi ya namna ile iko mingi sana Zanzibar. Zanzibar kuendelea ni suala zima la *tourism* na *real estate*, sasa ni namna gani tunaweza kusaidia? Tunaweza kutizama katika wigo huo, namna gani *immigration* kupitia Zanzibar ikawa na wigo fulani sasa wa kuwawezesha Wazanzibar kule katika uwekezaji wao. Tutaweka *cealing*, mtu aki-*invest* dola laki tatu anaweza kupata *resident permit*, pengine inamruhusu kubakia Zanzibar au akitaka kuja mpaka Bara kuwe na namna fulani ya kuweza kuwekeza watu wasiweze kutumia vibaya ile mianya ya uwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni muhimu sana tufanye hivyo kama kweli tunataka maendeleo yafanyike, hususan kwa uchumi wa Zanzibar. Tukitizama rasilimali zetu sisi zaldi ya uchumi wa *blue* ambapo tunaongelea bahari ni mdogo mno tofauti na Bara; kuna rasilimali watu, rasilimali nguvu na *minerals*. Kwa hivyo, naombeni sana tulitizame suala hili na muhimu suala la *BoT* kwenda *offshore* na *immigration* hususan katika masuala ya *resident permit*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Makoa, muda wetu kama utaturuhusu tutamalizia na Mheshimiwa Judith Kapinga.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehema mwenye kurehemu, ambaye ametujalia kuwepo katika nyumba hii Tukufu. Pia nikushukuru wewe kunipa nafasi hii ya kuchangia huu Mpango ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nijikite sana katika Mpango huu hususan niende katika Wizara yetu mama

ambayo iko katika Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo ni ya Muungano pamoja na Mazingira. Kama tunavyo jua Tanzania ni pamoja na Zanzibar, bila Zanzibar hakuna Tanzania. Sote sisi ni waumini wa Muungano na mimi ni muumini wa Muungano wa haki na wa usawa. Kwa hivyo, napenda Muungano huu udumu katika mfumo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi jambo ambalo tuna shida kule katika visiwa ni kuhusu mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko ya tabianchi yametukumba sana katika Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba na visiwa vidogovidogo ambavyo vimeizunguka Zanzibar. Wizara inayohusika nahisi kwa upande wangu hajafanya vya kutosha, leo ukiangalia visiwa vinavamiwa na maji ya bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoa mfano kuna visiwa vidogovidogo kama Kisiwa Panza, Pemba kuna Kisiwa kinaitwa Kisiwa Panza. Kisiwa kile kimevamiwa mpaka sehemu ya kuzikia makaburi yamezolewa na maji, wakati mwininge unaweza ukaenda ukakutana na mafuvu ya vichwa ya maiti. Kadhalika kuna Kisiwa cha Mtambwe Mkuu, Mtambwe Mkuu ni katika jimbo langu ambacho ni kisiwa cha historia kilichokaliwa na Wareno katika karne ya 18 ambacho kinatishia amani, wananchi wake wanakaribia kuhama kwa sababu maji ya bahari yamevamia kisiwa kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viko visiwa vingine vingi kwa mfano Misali ni kisiwa vilevile cha utalii, lakini nacho kimevamiwa na maji, lakini bado Serikali kupitia ofisi yetu hii haina jitihada yoyote ya makusudi ambayo inaifanya na mpango endelevu kuweza kushughulika na mambo haya ili kukinga maji yale yasiweze kuvamia makazi ya watu. Kwa hivyo, hofu yangu baada ya karne si nyingi zinazokuja tunaweza tukavipoteza visiwa hivi, kwa hivyo, yale matamanio na utashi tuliokuwanao wa kuwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikaondoka kwa sababu visiwa vile vimeondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ni mfano ambao uko hai kabisa. Sisi wazee wetu ambao wameishi katika miaka

sitini, sabini siku za nyuma wanatueleza tunapita katika bahari ya kina sasa hivi lakini miaka sitini iliyopita ilikuwa watu ni mashamba wakilima mipunga katika maeneo yale, lakini kwa sababu hakuna jitihada maalum kwa hivyo, bahari inapanda juu kila uchao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Ofisi, Wizara kattika Ofisi ya Makamu wa Rais kwa makusudi kabisa ifanye bidii tuje tuvitembelee visiwa. Awamu iliyopita ya Bunge tulifanya jitihada kubwa kuonana na Mawaziri lakini haikuwezekana, hawakupata nafasi ya kuja kuvikagua na kuweza kupata ufumbuzi. Kwa hivyo, huo ni msisitizo wangu mkubwa ambao napenda kuutoa kwenye Mpango huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari hii kwa kweli inaanza kuonekana. Hata hizi mvua ambazo hazina misimu, unakuta mvua zinanyesha wakati mwingine, mafuriko yanatokea wakati wa kiangazi, lakini wakati wa misimu wa mvua yenye we mvua haipatikani. Ndio maana wakati mwingine tunapata hii *collision* katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nilitaka niliseme kwa ufupi ni kuhusu huu Mfuko wa Kunusuru Kaya Masikini ambao unajulikana kwa TASAF. Mfuko huo kwa kiasi kikubwa nikiri umeleta manufaa makubwa katika kaya zile ambazo ni masikini. Familia zile za kaya masikini zimemudu kuwapeleka watoto wao shule, kupata *uniform*, kupata chakula, kupata ada za shule na wakati mwingine kupata pesa za matibabu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, ni jambo zuri, lakini tatizo linakuja, uteuzi wa hawa wanufaika unakuwaje? Wakati mwingine unaweza kuona watu ambao wanastahiki hasa kuingizwa katika mpango huu wameachwa, lakini wale ambao wana uwezo kidogo ndiyo ambao wamechukuliwa. Hii inatokea wakati mwingine utashi wa viongozi wa Shehia, kama mnaendana pamoja na kiongozi wa Shehia, Sheha, basi anaweza kukiingiza katika listi.

## T A A R I F A

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusema kwamba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khalifa kuna Taarifa.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe Taarifa mzungumzaji...

**MWENYEKITI:** Jitambulisse tafadhali.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina naitwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Jimbo la Wingwi, Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe Taarifa mzungumzaji kuhusu utaratibu unaotumika kuwapata wanufaika wa kaya maskini kule Pemba. Kunafanyika kikao cha jamii ambapo wanajamii hawa wanachagua watu wa kuratibu na kuorodhesha wanufaika wa kaya masikini ambao wanaitwa *CMC* si Sheha.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Sheha hashiki daftari kuandika wanufaika wa kaya masikini, ni wananchi wenyewe ndiyo wanaoandika kupitia wajumbe wanaowachagua wao wenyewe ambao wanaitwa *CMC*, asipotoshe umma. Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khalifa, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tuendelee, asijejua maana haambiwi maana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusema kuwa upande wa pili miradi hii, hasa ule mradi wa kutoa ajira ya muda, tatizo liliopo pia ni ule uteuzi wa ile miradi. Wakati mwingine miradi inateuliwa au inawekwa lakini haiangaliwi *sustainability* yake, nini uendelevu wake na nini tija yake mwisho? Kwa hivyo, unaweza kuanzisha mradi lakini baadaye ukawa haukufika mwisho, tija yake inakosekana. Pia wakati mwingi mradi ule unakosa ile *value for money*. Utakuta mradi umefanywa lakini *value for money* haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi kuna mradi wa tuta la kuzuia maji ya bahari ambao umefanywa katika kipindi fulani, ukiangalia umechukua muda mrefu, lakini tija yake haikuonekana kwa sababu leo tuta lile limevurugika, maji yanaendelea kuingia katika mashamba ya watu kwa hivyo, ile *sustainability* inakosekana. Hata ukiangalia tuta lile labda lingejengwa na watu kwa kulipwa shilingi milioni mbili, milioni tatu, lakini limegharimu zaidi ya shilingi milioni 10, lakini tija yake haikupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi tunasikitika Wabunge katika maeneo ya miradi hatushirikishwi. Mimi kipindi kile nilikuwepo, mradi huo uko karibu tu, umo katika kata au shehia yangu, lakini mimi sikushirikishwa vyovoyote ili kuweza kutoa ushauri wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, yangu ni hayo niliyosema kwa ufupi, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Shukrani sana. Mheshimiwa Ali Makoa, tutamalizia na Mheshimiwa Judith Kapinga.

**MHE. ALI J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nikushukuru wewe kwa kuni pa nafasi ya kuchangia Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niishukuru Serikali ya Awamu ya Tano, chini ya Dokta John Joseph Pombe Magufuli, Mama Samia na Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa. Pia nitoe shukrani kwa Mawaziri wa Awamu iliyopita kwa kazi

kubwa waliyomsaidia Rais wa nchi katika kutekeleza shughuli mbalimbali katika nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mazuri yaliyofanyika awamu iliyopita, pia mimi mchango wangu katika mpango huu ni kama ifuatavyo, moja nitagusa sehemu ya kilimo. Kama tunataka tufikie malengo ya kilimo katika nchi yetu ni lazima kwanza mambo yafuatayo yafanyike. Moja, tuhakikishe ile migogoro mikubwa ya mashamba kati ya wananchi na taasisi za Serikali inamalizwa mapema ili kutoa nafasi kwa wananchi kuendelea kufanya kilimo. Iko migogoro kati ya wananchi na Jeshi la Magereza kuhusiana na mashamba na imechukua muda mrefu kiasi ambacho imekuwa ikisimamisha shughuli za kilimo kwa wananchi hasa maeneo ya Kingale kwa kule kwetu Kondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tujikite katika mbegu. Soko la jana nilikwenda katika maduka ya mbegu, mfuko wa kilo mbili wa alizeti unauzwa kati ya Sh.15,000 mpaka Sh.16,000. Kwa hiyo, Mpango ungejiwekeza katika maeneo ya uandaaji wa mbegu ili kurahisisha upatikanaji wa mbegu kwa bei nafuu kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kuhusu viwanda. Tumekuwa na viwanda vingi sana katika nchi hii. Nimekuwa Mkoa wa Pwani, tumekuwa tukiuita Mkoa wa Viwanda kwa sababu viko viwanda ambavyo vinaonekana, ni kazi kubwa iliyofanyika katika Serikali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne, Mpango huu unatakiwa uendane sambamba na kuweka tahadhari ya kuilinda miundombinu pamoja na mali za wenye viwanda. Nimewahi kushuhudia kiwanda kinaungua moto mpaka kinamalizika hakuna zimamoto. Kwa hiyo, nashauri kwenye Mpango huu wakati tunaandaa mipango ya viwanda tujaribu na Wizara nydingine ziwe zinashirikiana katika kufanya ulinzi. Kiwanda cha Mafuta ya Alizeti Kondoa kiliungua mpaka kikamalizika hakuna zimamoto. Walipofanya juhudhi ya kutafuta zimamoto Babati, Manyara, zimamoto linapatikana kiwanda kimeungua mpaka kimeisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia wawekezaji wa mabasi, muda mfupi badaye basi la abiria pia likaungua mpaka linamalizika, hakuna zimamoto. Kwa hiyo, tunaomba katika Mpango huu pia, Wizara ya Ulinzi iangalie maeneo yale ambayo yanakosa zimamoto yatufanyie mpango wa kupata zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano, Mpango huu tunaomba uimarishe uwajibikaji, uadilifu na uaminifu katika sekta zote ambazo watu wamepewa majukumu ya kumsaidia Mheshimiwa Rais ikiwepo kwenye eneo la *TRA*. Bado kuna mianya mingi sana ya kodi kupotea na yako maeneo mengi kabisa kodi hazlipwi. Kwa hiyo, Mpango huu uendelee kuweka mkakati kwa ajili ya kuhakikisha kodi ya Serikali inaingia hasa kwa kutumia zaidi TEHAMA katika ukusanyaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Judith Kapinga.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, napenda kuipongeza Serikali kwa *commitment* kubwa inayofanya katika sekta ya habari, mawasiliano na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza kuzungumzia namna tunaweza tukaboresha mifumo ya kutumia huduma za fedha kwa njia za kimtandao. Kama tunavyofahamu, kutokana na changamoto kubwa ya ajira vijana wengi wamejielekeza katika kufanya ujasiriamali wa kimtandao ambao kwa kiasi kikubwa unatumia huduma za fedha za kimtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za fedha za kimtandao zimekekwa pamoja na sababu nyingine, ili ziweze kumrahishishia huduma mfanyakia shara. Nafahamu hizi huduma za kifedha za kimtandao zinahusisha tozo ambazo zina kodi ambayo ni muhimu sana katika utekelezaji wa miradi

ya maendeleo ya Serikali. Pamoja na dhamira hizo ambazo ni njema sana tozo kwa ajili ya kutumia huduma za kifedha kwa mitandao ni kubwa mno na hivyo inasababisha vijana wengi wasiweze kuwa na mazingira mazuri ya kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano. Leo hii ukiwa unatuma pesa shilingi 5,000/= tu kwa mtandao wa simu gharama yake ni shilingi 750/=, unaweza ukaona ni ndogo lakini ni 15% ya pesa ya mtu. Anayetoa shilingi 50,000/= anakatwa shilingi 2,700/= ni 5.4%; anayetoa shilingi 200,000/= anakatwa shilingi 3,700/= ni 1.9%. Kwanza unaona yule ambaye ni maskini kabisa wa chini ametoa shilingi 5,000/= anakatwa 15% ya pesa yake, yule ambaye anatoa shilingi 300,000/= anakatwa 1.9% ya pesa yake. Sasa hawa vijana ambao wanaanza biashara wataweza vipi kupambana katika soko hilli la kimitandao? Hawana ajira, wanaamua kujajiri kwenye mitandao na gharama zinakuwa kubwa kiasi hiki? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiamua kwa mfano leo unaamua kutuma ada kutoka *Tigo Pesa* kwenda *NMB* gharama yake kwa Sh.140,000/= anakatwa Sh.6,000/=. Kama una watoto watatu gharama yake ni Sh.18,000/=, kwa uchumi upi wa Mtanzania? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ni kubwa mno, kijana anafanya kazi kwenye mtandao ili apate faida ya shilingi 10,000/= na shilingi 20,000/= lakini yote inaliwa kwenye tozo za huduma za fedha za kimtandao. Naomba Serikali iangalie upya hizi tozo ili ziweze kuleta unafuu kwa vijana ambao wanapambana kwenye mitandao ili kuweza kupata kula yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye huduma za *internet*, natambua tafiti zinaonesha Tanzania ndiyo ina tozo ndogo kabisa kwenye *data*, katika ukanda wote wa *East Africa*, lakini tatizo lipo kwenye upandishaji holela wa huduma za *data* (*internet*). Wiki moja iliyopita ukitoa shilingi 8,000/= kwa *Tigo* ulikuwa unapata *GB 16*, yaani kesho asubuhi

watu wameamka wameweka 8,000/= wanunue *GB* 16 wanapewa *GB* tatu, hawajapewa taarifa kwamba huduma gharama yake zinaongezeka. Halafu sasa *MB* 300 unapata kwa Sh.1,000/= yaani kwa mfanyakishara uki-*post post* mbili, hela imekwisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi 3,000/= unapata *GB* moja wakati shilingi 3,000/= ulikuwa unapata mpaka *GB* 5. Watanzania hawakupewa taarifa ya upandishaji wa gharama hizi yaani kampuni ya mawasiliano anaamka anaamua kupandisha gharama za mitandao kama anavyopenda. Pato la mtu mmoja-mmoja ni shilingi elfu moja na kitu, lakini unamfanya Mtanzania atumie gharama ya shilingi 3,000/= kwa siku kwenye huduma ya mawasiliano, sio sahihi. Naomba Serikali iangalie upya ili inusuri vijana hawa ambao wanatumia mitandao ya kijamii kujipatia kipato chao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni la pili kutoka mwisho, sisi tunapolipa huduma, tunaweza kulipa huduma kupitia *Master Card Visa* pamoja na *PayPal* kulipia malipo nje ya nchi. Leo mimi kijana wa Kitanzania nikiamua kufungua *website* kutaka kutangaza bidhaa watu wa nje ya nchi waweze kununua kwenye *website* yangu hawawezi kulipa kupitia *Master Card*, *PayPal*, *Visa* au *Credit Card* hela iingie moja kwa moja kwenye benki yangu, lakini mimi nina uwezo wa kuwalipa wale wa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vijana tunawahimiza ubunifu, lakini ubunifu wao hauwezi kuwasaidia kwa sababu watu wa nje hawawezikuwalipa kwenye akaunti zao za benki. Naomba *BoTna* Wizara ya Fedha iangalie suala hili kumhusuru kijana huyu wa Kitanzania na kumwekea mazingira mazuri ya biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, naamini mmeielewa vizuri hiyo hoja. Kweli hayo ni malalamiko

ya vijana wengi, wanashindwa kulipwa kwa kazi waliyofanya, yaani inabidi watumie watu ambao wako nje ya nchi yetu hii kama Kenya ama Uganda walipwe wale halafu ndiyo wawalipe Watanzania, kwa hiyo, gharama zinazidi kuwa kubwa. (*Makofi*)

Tunaendelea, Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Mipango kwa sasa imekamilisha kazi zake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji ambao hawakupata fursa ya kuchangia asubuhi watapata nafasi tutakaporejea mchana.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 Jioni.

*(Saa 07.06 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali  
wa Mwaka 2021 (*The Written Laws (Miscellaneous)  
Amendment Bill, 2021*)**

*(Kusoma Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Katibu hapo ametusomea Muswada kwa mara ya kwanza, naamini tumepata kwenye vishikwambi vyetu orodha ya shughuli za leo, orodha ya nyongeza ambayo inaashiria kwamba kuna jambo linaongezwa katika ratiba yetu ya leo nayo ilikuwa ni kusomwa mara ya kwanza kwa huu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali. Kwa hivyo Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2021 (*The written Laws (Miscellaneous) Amendment Bill, 2021*) umeshasomwa kwa mara ya kwanza hapa Bungeni.

Sasa baada ya hatua hiyo sisi sote tunafahamu chini ya kanuni ya 97(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Mheshimiwa Spika ameagiza kwa mamlaka aliyonayo Muswada huo unapelekwa kwenye Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria ili ufanyiwe kazi. Kwa hivyo tutaanza kufuata sasa ule utaratibu wetu wa kawaida baada ya Muswada huu kusomwa kwa mara ya kwanza.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

### **KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na uchangiaji na kuna Wabunge amba majina yao yako hapa hawakupata fursa ya kuchangia asubuhi kwa hiyo wataanza kuchangia mchana huu. Tunaye Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Miraji Mtaturu atafutiwa na Mheshimiwa Nicholaus Ngassa na Mheshimiwa Steven Kiruswa ajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu Mpango wa Miaka Mitano na ule wa Mwaka Mmoja. Kwa hakika nianze kwa kumshukuru

Mwenyezi Mungu, mwingu wa rehema kutujalia uzima na kuweza kukutana leo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda basi niende moja kwa moja kwenye kuchangia Mpango ulioko mbele yetu. Kwanza nianze kwa kupongeza Mpango ule wa Pili wa Miaka Mitano ambao ulipita, tumeuona tathmini yake na katika muda huu tumeona maendeleo makubwa ya nchi yetu. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, pamoja na Serikali na watumishi wote ambao wameshirikiana katika kutekeleza Mpango ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunapokuja kwenye Mpango huu wa Miaka Mitano na hasa ule wa Mwaka Mmoja tunaona namna ambavyo tumejipanga kwenda mbele na nitachangia sana leo kwenye eneo ambalo limesema kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba Watanzania wengi wanafanya kilimo katika nchi yetu, zaidi ya 70% wanafanya kilimo na kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa yetu. Naomba nikiri wazi kumekuwa na juhudini mbalimbali za kuhakikisha kilimo chetu kinabadilika na kama ambavyo Mheshimiwa Rais amesema katika hotuba yake, kwamba tutaongeza juhudini katika kuwekeza kwenye kilimo na kilimo chenyewe ni kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo tukikifanya vizuri pamoja kuwa kitatusaidia kwenye chakula lakini mapato mengi yanapatikana kwenye kilimo. Leo Halmashauri zetu nyingi zinategemea mapato makubwa kutoka kwenye mazao mbalimbali, kwa hiyo maana yake tukiwekeza kwenye kilimo kutakuwa na mapinduzi makubwa ya kiuchumi na itatusaidia sana kwenda mbele kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hoja yangu ni kwamba ni wazi tumefanya *research*nyingi, ni wazi tumepata maoni mengi, ni wajibu wa Serikali sasa kuyatendea kazi

mawazo yale. Hatuwezi kuwa tunatoa ushauri na ushauri ule tunauacha kwenye makabati. Ombi langu nataka niiombe Wizara ije na mpango mahususi katika kukuza kilimo chetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea kwenye suala dogo sana la ambavyo tunasema Tanzania ya viwanda, lakini viwanda vyetu haviwezi kwenda mbali kama hatujawekeza kwenye kilimo kwa sababu tunahitaji malighafi kwenye viwanda vyetu. Kama leo hatujawekeza vizuri kwenye kilimo chenye pembejeo, mbolea, viatilifu na Maafisa Ugani ambao wanafanya wajibu wao. Naamini huko vijijini wote tunatoka hali ya Maafisa Ugani ni imechoka, hali ni mbaya idara ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii anaweza kwenda kiongozi yejote ukakutana na Afisa Ugani, wewe unaweza kuwa na uelewa mkubwa kullko Afisa Ugani maana yake Afisa Ugani huyu hawezi kumsaidia mkulima. Ombi langu nataka niiombe Serikali hasa Wizara ya Kilimo itusaidie kuongeza nguvu kwenye Maafisa Ugani. Naamini kabisa wao pia ni mashahidi kuna baadhi ya mazao ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo nitaongelea zao moja tu la alizeti, mafuta; leo hii sisi tunaagiza tunatakiwa kwa mwaka kutumia *metric tons* 570,000 za mafuta, lakini uwezo wetu ni 210,000 tu, maana yake ni karibu nusu tunaagiza nje ya nchi. Kwa hiyo maana yake ni kwamba tunatumia fedha za kigeni nyngi kuagiza mafuta ya kula, hili jambo ni vema tukabadilisha mwenendo wetu tuhakikisha kwamba zao la alizeti pamoja na mazao ya mbegu za mafuta, tuchukue hatua kubwa katika kuhakikisha tunawekeza vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatumia karibu bilioni 460 kwa mwaka kuagiza mafuta nje ya nchi, ndiyo maana leo tunakuta kuna upungufu wa mafuta ni kwa sababu hatujawekeza vizuri kwenye eneo hili. Niseme tu kwenye eneo hili tukija na mpango kweli unaosema kwamba wa *block farming* itakuwa ni jibu la tatizo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia mkakati wa Serikali katika kuhakikisha kwamba inakuza kilimo cha umwagiliaji kutoka kwenye heka zile ambazo zimeelezwa 461,000 tutakwenda kuhakikisha kwamba tunaongeza zinakuwa 694,000, bado tuna safari ndefu. Lazima tuwe na mapinduzi ya kweli ya kuhakikisha kwamba tunawekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji, tusiendelee kusubiri mvua ambayo hatuna uhakika nazo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunavyoongea habari ya umwagiliaji, tunasemea habari ya kwamba uhakika wa kilimo chetu tusitegemee mvua, lakini wengine walisema hapa, maji yanayomwagika haya kwenye mito kila mwaka, tunayatumiaje ili kuweza kuhakikisha kilimo chetu kinakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hilo la alizeti, nadhani kuwe na mkakati au msukumo maalum, kama tunaweza kuwa na Bodi ya Korosho, kama tunaweza kuwa na Bodi ya Pamba, kwa nini tusiwe na Bodi ya Alizeti ili kuweza kuweka msukumo mkubwa zaidi. Tumeambiwa hapa kuna zaidi ya mikoa nane inayoweza kulima alizeti. Tukiwa na Bodi hii ya Alizeti tutaweka mkakati maalum wa kuhakikisha kwamba tunalima alizeti kwa wingi, tunawezesha viwanda vyetu na mwisho wa siku tunakuwa na mafuta ya kula ya kutosha. Kwa hiyo ombi langu, naomba kama tunazo hizo nyiningine, basi na hii Bodi ya Alizeti iwe ni jibu la kuhakikisha kwamba tunapata mafuta ya kula ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, naomba nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja, naomba niwaachie changamoto hiyo Wizara ya Kilimo. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nicholaus Ngassa atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt Steven Kiruswa, Mheshimiwa Janet Mahawanga ajiandae.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia

Mpango wa Maendeleo ya Taifa. Wiki iliyopita kwa sisi Wabunge wengi tulioingia Bungeni kwa mara ya kwanza tulitumia nafasi hii pia kushukuru Mungu kwa kuandika historia, lakini pia leo tunaingia katika historia nyingine ya kutoa mawazo kwa ajili ya ujenzi wa Taifa letu kwa sababu tunakwenda kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie eneo moja tu, nafasi ya utumishi wa umma katika kufanikisha Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa. Nimeusoma Mpango vizuri kuanzia ukurasa wa 111 mpaka ukurasa wa 120, umeelezea kuhusu maendeleo ya watu na eneo moja kubwa ambalo limekuwa *interesting* kwangu ni suala la ujuzi. Hotuba ya Waziri na Mpango umeelezea vizuri sana kuhusu ujuzi katika ngazi mbalimbali ambazo namna itakavyotusaidia katika kulisogeza Taifa letu mbele. Hata hivyo, kuna changamoto kubwa sana ambayo Serikali naomba msi-*compromise* na hili ni suala la utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002; tuna Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za 2003 na Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za 2009; vyote katika muundo wake na maelezo yake havitoi nafasi katika suala la ujuzi. Sasa huu Mpango tunaoujadili leo Wabunge, wanaoenda kutekeleza, wanaoenda kusimamia na wanaotakiwa kubuni vyanzo vya mapato ni hao hao watumishi wa umma ambao Mpango haujawatambua vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapolipitisha hili jambo litakwenda na Serikali wasipoliona, matokeo yake baada ya miaka mitano, Waziri ataleta Mpango mwingine utakuja na utakuwa na *table* inayoandika vikwazo na moja ya kikwazo itakuja ni hili suala. Sasa ushauri wangu ni nini? Sisi kama Taifa linaloendelea tunachukulia mfano wa Malaysia, Malaysia walipofanya mabadiliko yote kwenye kilimo na viwanda walikuja na kitu wanakiita *re-energizing civil service*; waliamua kuweka nguvu kwenye kubadilisha mfumo wa utumishi wa umma wakaja na mfumo ambao wanaangalia *knowledge, skills* na *ability* kwa maana ya kwamba maarifa,

uwezo na ubunifu ndiyo vikawa vinampa mtu nafasi ya kufanya maamuzi katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwetu bado tuna mfumo wakwetu tunaita *meritocracy* na ni mfumo wa kizamani na ndiyo maana mfumo wetu wa utumishi wa umma umejengwa vizuri sana, lakini unafanya kazi kizamani, bado tunatumia *model* za akina Max Weber za *seniority*, unapotumia mifumo ya *seniority* maana yake watu wenye uwezo wenye ubunifu wanakosa nafasi za kufanya maamuzi, michango yao inaishia chini, unakuta maamuzi yanaishia kufanywa na Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na Wakuu wa Vitengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kukupa mfano hata huu Mpango tunaoujadili, unaweza kwenda Wizara ya Fedha ukaulizia, ukakuta wanaoufahamu huu Mpango hawafiki watumishi 30, Wizara nzima hawaufahamu. Tuunde mfumo sheria hizi zibadilishwe, kuwe na mfumo wa kubadilisha vikao vyta maamuzi vijumuushe na watumishi wa kawaida ambao wengi wanakuwa na uwelewa mpana.

Kwa hiyo tutapokuwa na mawazo ya wachache matokeo yake kwenye utekelezaji tunakwama na ndiyo maana tunatolea mfano suala la ubunifu wa vyanzo vyta mapato, kila siku vyanzo vinarudi vilevile, utaishia vichungi vyta sigara, utaishia sijui pombe zenye vileo vikali, ukiwaambia watumishi kubuni vyanzo vipyta wale wanaobuni miaka yote ni wale wale, ni *level* ya juu *cluster* watumishi wa chini hawashirikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya wazo ambalo ninalo hata kwa watumishi wa umma, inabidi taasisi na idara zote zinazohusika na makusanyo ya maduhuli na mapato waambwiwe ili tuwaongezee mishahara na motisha watumishi wenu wabuni vyanzo vipyta vyta mapato. Tukifanya hivyo tutakusanya trillioni 40 kwa mwaka hili Taifa, lakini sasa hivi mtu anajua ikifika tarehe 23 tarehe ya Baba Jesca imefika nitapata mshahara, hata nisipofanya kazi hamna litakapofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli tumefanikiwa kujenga nidhamu kwenye utumishi wa umma, lakini nidhamu tullyonayo ni ya watumishi kuingia saa 1.30 anasaini, anasubiri kutoka saa 9.30, hawana ubunifu, wanaishia kuanza kuzunguka maofisini wanaauza vocha, wanaauza mabuyu kwa sababu kutokana na mfumo huu hauwasaidii. Ofisi zinabebwa na watu wachache na mtu anajua kwamba mimi sasa hivi nimeshaajiriwa ni *permanent and pensionable*, nisipokifanya leo na mimi labda siku moja nitakuwa Mkurugenzi nitafanya. Tunataka kila mtu atimize wajibu wake. Namna ya kutimiza wajibu wake ni kubadilisha mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningeshauri Serikali, Wakuu wa Idara kwa maana ya Wakuu wa Taasisi za Umma Wakurugenzi wapewe mamlaka ya kuweza kuteua na kupendekeza watu kwa Katibu Mkuu wa Utumishi wanaoweza kufanya nao kazi kwenye menejimenti. Menejimenti nyingi hazitoi ushirikiano kwa Wakurugenzi walioteuliwa na Mheshimiwa Rais, unakuta Menejimenti ina watu tisa wanaounga mkono Mkurugenzi aliyeteuliwa na Rais ni wanne au watano anashindwa kufanya kazi na wale watu matokeo yake wanabaki wanamkwamisha, ndiyo ile *bureaucracy*, unakuta dokezo linahitaji laki mbili, maamuzi yanatumia tisa kuamuliwa, hatuwezi kusogea kama Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tubadilishe huo mfumo Mkurugenzi anapopewa taasisi ya Serikali anapoona kuna watu anashindwa kufanya nao kazi, apendekeze watu kwa Katibu Mkuu wa Utumishi apeleke majina matatu akiletewa moja naye atakuwa hana sababu ya kusema kwa nini nimekwamishwa, lakini atakwamishwa na mwisho wa siku anajua huyu kapewa, baadaye atatumbuliwa atatuacha, ndiyo kauli zinazoendelea kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jambo lingine ambalo ningependa kupendekeza ni kwenye suala la ubunifu wa vyanzo vya mapato kama nilivyo sema. Tunahitaji fedha za kuweza kusaidia huu Mpango; huu Mpango ni wa miaka mitano na Taifa letu tunahitaji lisogee mbele na tuna miradi

mikubwa ambayo inahitajika ikamilike tunahitaji fedha. Wapewe nafasi watumishi wabuni vyanzo vipyta vya mapato ili kuweza kusaidia Taifa letu kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Naona Mheshimiwa Waziri alikuwa anafurahi hapa kwa kuambiwa vyanzo vya mapato vije vingine jamani, hivi vingine vimeshakaba.

Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa atafuatiwa na Mheshimiwa Janet Mahawanga na Mheshimiwa Santiel Kirumba ajiandae.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia kwenye huu Mpango wetu wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano pamoja na Mpango wa mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijipanga kuchangia katika maeneo yaliyotamkwa na kuelezewa kwa kina kwenye Mpango katika sekta za kilimo, mifugo, maji na madini, lakini kwa kutambua ufinyu wa muda nitaomba nichangie maeneo mengine kwa maandishi ila nijikite katika hoja inayohusu sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Mpango umeweka bayana mikakati sahihi na safi kabisa ya kuijenga sekta ya mifugo kwa kuhakikisha kwamba maeneo ya malisho yanaongezwa, upatikanaji wa maji, upatikanaji wa madawa ya tiba na chanjo na maendeleo mengine ya miundombinu ya mifugo, lakini kuna changamoto nyingine moja kubwa ambayo bado tunakabiliwa nayo kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ni kwenye upande wa masoko; hali halisi ilivyo sasa hivi kwa wafanyabiashara wa mifugo katika nchi yetu ni kwamba hakuna masoko yenye tija ya ndani wala nje. Naomba nichukue mfano na naipongeza sana Serikali yetu kwa

kutengeneza mazingira safi ya wawekezaji kwenye sekta ya bidhaa za mifugo kuja kuwekeza nchini na azma kubwa iliyojitokeza ya ujenzi wa viwanda mbalimbali vya mazao ya mifugo nichukue mfano wa kiwanda kikubwa kilichojengwa katika Wilaya yangu ya Longido Kiwanda cha *Elia Foods Oversees Limited*. Kiwanda kile kimejengwa kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kile kimejengwa kwa gharama kubwa, kina uwezo wa kuchinja mpaka ng'ombe 500 kwa siku na mbuzi pamoja na kondoo 4,000 kwa siku. Baada ya mwekezaji kumaliza kujenga kiwanda kile na akaanza uzalishaji mwezi wa 11 akakutana na changamoto kubwa ambayo hata sisi kama wafugaji na wafanyabiashara wa mifugo tumeona kwamba itakuwa ni kikwazo kikubwa kwa ufanisi wa viwanda vinavyojengwa katika sekta ya mifugo katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utitiri wa kodi ambazo bahati nzuri Mheshimiwa Kingu alishatolea uafanuzi juzi akatoa ulinganifu mzuri kabisa wa jinsi Tanzania tunavyofanya vibaya kwa kuwekeza tozo mbalimbali katika viwanda vyetu kiasi cha kufanya vile viwanda ili viweze kuwa endelevu. Kuna zaidi ya tozo 11 lakini ukiangalia madhara anayopata mwekezaji ya kutoona namna nyingine ya kutengeneza faida, anayahamishia kwa muuzaji ambaye sasa ni mfanyabiashara wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika hiki kiwanda cha mfano tu ambacho nimekitaja cha Longido, mwekezaji huyu amepanga bei ya kununua mbuzi Sh.6,500 kwa kilo na wafugaji ambao wamekuwa wakitegemea soko la nchi ya jirani hawaoni tija kwa sababu hata kama wakilipia ushuru wa Serikali wakifisha mbuzi zao Kenya wanauzu kilo kwa Sh.8,500. Kwa hiyo, kwa ajili ya kodi zilizoko maana nilishafanya kikao kati ya wafanyabiashara wa mifugo wa wilaya yangu na Tanzania kwa ujumla wanaotumia soko la Namanga na mwekezaji tukatafuta chimbuko la shida iko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji akatupa changamoto zake akasema kuna hizi *regulatory fees* ndiyo zinafanya yeye asiweze ku-*competence* masoko ya nchijirani na asiweze kutoa bei yenye tija. Yeye kila akichinja na kuweka *consignment* moja akifisha bandarini asilimia moja ya thamani ya ile *consignment* inachukuliwa na *Meat Board*. Mwekezaji huyu anapopeleka bidhaa yake sasa kuza sokoni, Wizara inachukua Sh.50 kwa kila mbuzi na kondoo kwa kilo na Sh.100 kwa ng'ombe. Mfanyabishara huyuhuyu mwenye kiwanda anachajiwa na BAKWATA kwa ajili ya kukagua nyama shilingi milioni 2 kwa mwaka ambayo sasa hivi wanabishania nao wawe wanalipwa kwa kila kilo ya nyama wanayosafirisha kwenda kuza kwenye masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, akajikuta kwamba hakuna namna anaweza akaongeza bei kwenye bidhaa na yeye akawenza kukiendesha kiwanda kile. Kwa sababu hiyo basi tukajikuta ile adhima iliyotamkwa kwenye Mpango ya kuendesha uchumi wa viwanda na shindani hatuko anywhere karibu na kufanikiwa kwa kuwa washindani katika biashara ya bidhaa mbalimbali zinazotengenezwa na viwanda vya hapa nchini kwetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kuishauri Serikali ili tutoke na wafugaji wetu wasiwe na sababu ya kupeleka mifugo Kenya tukapoteza bidhaa mbalimbali inayotokana na mifugo, ni vizuri sasa kodi hizi ama zifutwe au zifanyiwe marekebisho ili ziweze kutoa tija kwa wafugaji wetu na mwekezaji naye aone kwamba kiwanda chake kinamuletea faida na aweze kukiendeleza.

Pia kama kuna uwezekano kuwe na *tax holiday* ya mpaka mwaka mmoja maana huyu mwekezaji alisema kwamba mkinipunguzia kodi nitatoa bei shindanishi na ya Kenya ili atekete soko wale wafugaji wote wanaopeleka mifugo Kenya walete bidhaa pale pale Longido wauze kwenye kiwanda chetu na ajira ziongeze na faida zingine tunazopata kwa sababu kiwanda kile kinatumia kila kitu mfano kwato, pembe, mifupa na mbolea zinatoka *finished product* ambazo zinaendelea kuingia sokoni. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji huyu akasema kwamba kama Serikali ikimuondolea kodi yuko tayari kushindana. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie suala la kupunguza kodi katika bidhaa mbalimbali zinazozalishwa na viwanda vyetu vya ndani ili tuweze kujenga huo uchumi na biashara shindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa yale mengine ambayo nilitamani kuchangia, nitawasilisha kwa maandishi na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Santieli Kirumba, Mheshimiwa John Sallu ajiandae.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nichukue nafasi hili kumshukuru Mwenyezi Mungu, Chama changu ha Mapinduzi, kina mama wa Mkoa wa Dar es Salaam na familia yangu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nichangie Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Miaka Mitano na Mwaka Mmoja. Katika kuongeza kipato cha Serikali na kuwawezesha wananchi kiuchumi kuititia ile Mifuko 18 ambayo iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, napendekeza ishirikiane kwa karibu na Wizara ya TAMISEMI pamoja na Halmashauri zetu. Pia longeze wigo kwa kuhusisha Madiwani nao kwenye Mpango huu ili itengeneze mfumo mzuri wa ukusanyaji wa hizi pesa pindi wajasiriamali hawa wanapopata hiyo fursa kwani fedha nyingi zinatoka kwenye vikundi lakini pia hazirudi. Kwa hiyo, tatizo kubwa hapa ni mfumo wa ukusanyaji wa hizi hela. Watakapohusishwa pia Madiwani katika utaratibu huu itasaidia kwani vikundi vingi kwenye kata zetu Madiwani ndiyo watu sahihi na wanavijua zaidi vikundi itasaidia ufuatiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika kutoa fursa hizi, Serikali iangalie zaidi kwenye kutoa elimu kwa wajasiriamali hawa kwa sababu fursa zipo, mikopo inatoka lakini wananchi wengi wanakwama kutokana na ukosefu wa elimu. Elimu hizi

zikajikite katika kukuza ujuzi wa kuongeza thamani za bidhaa zao, upatikanaji wa mitaji, utafiti wa masoko na kuzitambua fursa zinazowazunguka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya naomba niongelee usajili wa vikundi. Sheria ya Fedha imetoa mamlaka kwa Benki Kuu ya Tanzania (*BoT*) kukasimu shughuli zote za usajili, usimamizi na ufuutiliaji wa vikundi vya kifedha. Makundi haya ya kifedha yamegawanywa katika sehemu nne, kuna mabenki na *microfinance* ambazo zinapata miongozo moja kwa moja kutoka *BoT*, kuna *SACCOS* ambazo zinapata miongozo katika Vyama Ushirika na kuna vikundi vya kina mama ambavyo ni *VICOBA* wao wanapata miongozo kutoka TAMISEMI. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki Kuu ilitoa muda wa mwaka mmoja vikundi yyote viwe vimesajiliwa kupitia sheria mpya. Ule muda uliisha, akina mama walikuwa wako tayari kusajili lakini miongozo kutoka TAMISEMI ilikuwa hajashuka huku chini. Iliongezwa muda wa miezi sita ambaao unaisha mwezi Aprili mwaka huu, lakini mpaka sasa bado akina mama wakienda kwenye Halmashauri wanakuta bado hakuna utaratibu wowote ambaao umetoka TAMISEMI unaowataka wao wasajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imeleta hofu kubwa kwenye vikundi vya kina mama kwani kuna vikundi ambavyo vimesimama kufanya shughuli zake za ujasiriamali na kuna vingine vinafanya kwa uwoga vikiwa vinasubiri kuangalia miongozo hii ya usajili mpya inataka nini na inasemaje. Kwa hiyo, niiombe Wizara ya TAMISEMI, iijtahidi kutoa miongozo hii basi ili kina mama wafanye huo usajili kwa kutumia hii Sheria mpya ya Fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali iangalie baadhi ya kero kuzifanya kama vyanzo vya mapato yaani fursa. Kwa mfano, Mkoo wa Dar es Salaam kuna kero kubwa sana ya takataka, Wizara ya Viwanda na Uwekezaji ni wakati sasa wa kuangalia ni jinsi gani kiwanda cha kuchakata taka kinaweza kupatikana kwani zaidi ya kuongeza kipato kwenye

nchi yetu itaongeza ajira pamoja na kumaliza hili tatizo la taka, tutapata mbolea na gesi na Serikali itapata pato lake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye ushauri, nashauri Serikali irejeshe mifumo ya kuzisaidia na kuchochea benki nchini yaani *credit guarantee schemes* ambazo zitasaidia wawekezaji kulipa kodi na Serikali itapata pato pia. Vilevile yafanyike marekebisho ya kodi inayohusu ufutaji wa madeni ambayo hayalipiki yaani *bad debts write-off* endane na sera, kanuni na Sheria ya Benki Kuu ili kuweka mazingira ya biashara yanayotabirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali iwe inatoa muda wa kutosha inapofanya marekebisho ya sera zake mbalimbali ili kutoa muda wa wadau kujipanga kutokana na mabadiliko ya sera zinapokuwa zinafanyiwa marekebisho. Pia Serikali iweke mazingira mazuri ya kufanya mabenki binafsi kuachana na sera ya kuanzisha benki ambazo zinakuja kuwa mzigo na hazina tija kwenye Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niombe mamlaka ya kukusanya kodi irekebishe *Tax Administration Regulation* kwa kuondoa utaratibu wa sasa wa kutumia *Urgent Notice* kutoka kwenye mabenki moja kwa moja badala yake iweke utaratibu wa kukubaliana na walipa kodi kulipa kodi kwa muda rafiki. Hii itasaidla sana kwani wafanyabiashara wengi wataweza kuweka hela benki, watakuwa na imani na kuondoa ile hofu kwamba benki siyo sehemu salama sasa hivi ya kuweka hela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakiweka taratibu hizi wafanyabiashara, wajasiriamali wengi watakuwa na imani, itaongeza hamasa, watu wataweka fedha benki, ukizingatia hata Mheshimiwa Rais wakati anahutubia Bunge la Kumi na Mbili alisisitiza kuwa watu wahimizwe kuweka hela benki ili kusaidia benki zetu zifanye biashara na mzunguko uwe imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Santiel Kirumba, atafuatiwa na Mheshimiwa John Sallu, Mheshimiwa Deo Mwanyikita ajilande.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Mwenyezekiti, awali ya yote, napenda kushukuru kwa nafasi hii uliyonipatia. Napenda pia kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi na UWT kwa Mkoa mzima wa Shinyanga kwa kunitua kuwa mwakilishi wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa ushindi wa kimbunga alioupara kwa mwaka huu. Ilikuwa si kazi rahisi lakini kwa matendo makubwa aliyoafanya ameweza kushinda na wananchi wakawenza kumwamini na kumpa nafasi nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, napenda kuchangia jinsi Serikali inapaswa katika mpango mpya huu wa kutengeneza ajira milioni nane na uchumi wetu uweze kupanda kwa asilimia nane. Serikali imejikita sana kwa wafanyakishara ambao kwa sasa hivi tukiangalia kwa hali halisi wako *ICU*, ukiangalia tunawanyonya sana na wakati tuna lengo kubwa la kutengeneza hizi ajira milioni nane ili kufikia asilimia nane.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, cha kwanza, naishauri Serikali iwawezeshe vijana na wanawake kwa kuwapa mitaji ya kutosha kwa sababu hii ndiyo nguvu kazi tuliyonayo. Hawa vijana wakitengenezewa ajira upya, *NEMC* wakitoa masharti ambayo ni nafuu, nina uhakika kila nyumba ina uwezo wa kuwa na viwanda vidogovidogo vya kuchakata vitu mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, kwa mfano kwa Mkoa wangu wa Shinyanga kuna vijana wadogo tu wenye miaka 25 wanatengeneza chaki, kuna kina mama wa kawaida tu wamekopeshwa na Halmashauri matrekti makubwa ya kufanya kazi, mitaji ya milioni 50 wanafanya kazi vizuri. Mheshimiwa Rais aliongelea katika *page* ya 11 kwamba hii mifuko ya ukopeshaji ikichanganywa na kuwa pamoja itawezesha Halmashauri kutoa kiasi cha pesa cha kutosha.

Kwa sasa hivi, hela zimegawanywa katika mifuko mbalimbali, kwa hiyo inafanya kwamba hata zile hela zilizokuwepo kwenye Halmashauri hazitoshi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kama Serikali inaweza ikafuatisha maoni ya Mheshimiwa Rais, hii mifuko ikawa mmoja itasaidia kwa kiasi kikubwa, itaongeza zile asilimia kumi za Halmashauri, itaenda kama ku-*boost*. Katika zile Halmashauri, wataangalia Serikali ina Halmashauri ngapi watazigawanya kama ni kwa *pro rata* au kwa *ratio* ya mikoa au kwa *ratio* ya wananchi ambao wako katika eneo lile ambao ni wanawake, vijana na walemavu. Hawa wakipewa mitaji ya kutosha watasaidia kui-*boost* hii ajira kwa kila mtu na tutakuwa tumepata ajira milioni nane na mapato ya nchi yataongezeka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Serikali hizi *certificate* zinazotolewa na Halmashauri ziweze kutumika kama dhamana, watu wanateseka sana kwenye dhamana. Kama Serikali inatoa hizi *certificate* katika Halmashauri ni wakati sasa hizi *certificate* hata benki wazikubali kwa sababu Halmashauri inazikubali kwa wajasiriamali wadogo wadogo kwa kuwapa mikopo. Ni wakati na benki nazo iviamini hivi vikundi watumie zile *certificate* kuwapa mikopo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kwa huu Mpango mwingine wa miaka mitano, asilimia za mikopo ya wanawake itoke kwenye asilimia 4 iende kwenye asilimia 7. Ninyi mtaona kwa namna ya pekee wanawake tukiwezeshwa tunaweza. Hata kwenye kura mnatutumia sisi, mnatuita wanawake ni jeshi kubwa lakini wanawake sisi ni jeshi mmetupa asilimia 4, sisi wanawake ndio tunaokaa katika jamii tunailinda. Kwa hiyo, naamini kwamba tukitoka kwenye asilimia 4 tukapewa asilimia 7 tuta-*boost* ajira nydingi za wanawake na mapato ya nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Serikali ipokee mchango wangu na naunga mkono hoja na naomba Serikali iunganishe ile mifuko iwe sehemu moja. Ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa John Sallu, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mheshimiwa Tunza Malapo aijandae.

**MHE. JOHN M. SALLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Namshukuru Mwenyezi Mungu, namshukuru Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, nashukuru Chama chetu cha Mapinduzi, nashukuru wananchi wa Handeni Vijijiini na wadau wote walionifanya niwepo hapa ili kuwatumikia wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli napongeza sana juhudzi zilizofanywa katika kuandaa Mpango huu. Namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kuandaa Mpango mkakati utakaotutoa sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Ndugu zangu si dhambi kushukuru na kupongeza juhudzi zilizofanywa katika kuanzisha miradi mikubwa katika nchi hii ambapo ni msingi mkubwa wa maendeleo ya nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache wa muda, nitaanza na bwawa kubwa la *Stigler's Gorge*. Bwawa hili la Mwalimu Nyerere litazalisha umeme wa maji *megawatt* 2,115 ambapo ndio rahisi duniani kote. Kwa hiyo, utachagiza maendeleo makubwa kwa viwanda vyetu vikubwa, vyatani na vidogo. Hivyo, itatusaidia sana sisi wananchi wa Handeni Vijijiini kuongeza thamani ya mazao yetu kwani sisi ni wakulima wazuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kuanzisha viwanda hivyo ambavyo tayari vimeshaanza na tuna mikakati ya kuvutia wawekezaji, vilevile maji na barabara ni muhimu. Ili mazao hayo yaweze kufika kwenye viwanda, ndugu zangu lazima tufanye mpango mkakati bajeti ya *TARURA* iongezeke. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile viwanda vinaendana na maji. Naomba Wizara yetu ya Maji tukitoka hapa tuwe na mpango mkakati ili tuongeze pesa ili wananchi

wetu wa vijjini wapate maji safi na salama na kuweza kuendesha mitambo hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni upanuzi mkubwa wa bandari zetu. Bandari zetu zimepanuliwa sasa lazima tutafute mbinu chochezi ziweze kufanya kazi zituingizie pato. Kwa mfano, wananchi wa Mkoa wa Tanga tumeshuhudia meli kubwa ya mita 200 ambayo ilibeba tani 55,000 za *Clinker* kwa ajili ya kwenda Rwanda. Meli hiyo illondoka pale Tanga ikiwa tupu, sasa lazima tutafute mbinu chochezi ili bandari zetu ziweze kubeba mizigo kuingiza na kutoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ya Madini iweze kusaidia wachimbaji wetu wadogo wa chuma na madini ya viwandani kwani Handeni Vijjini tuna madini ya chuma na madini ya viwandani kwa wingisana. Wachimbaji wadogo wamejitahidi, pale tuna takribani tani zaidi 50,000 imelala pale chini ambapo waliingia mkataba na Dangote lakini kwa bahati mbaya haijachukuliwa. Kama tungeweka mbinu chochezi basi tani hizo zingeondoka na meli hiyo na bandari yetu ingefanya kazi, Halmashauri ingepata siyo chini ya shilingi milioni 600, bandari yenyewe ingepata mapato siyo chini ya dola milioni 150 kwa sababu mzigo huo wa tani takribani 50,000 gharama yake ununuzi (*FOB*) huwa ni dola milioni 4. Kwa hiyo, ndugu zangu naomba tutafute namna chochezi Wizara ya Madini ikitusaidia ili tuweze kuwahudumia wachimbaji wetu hawa wadogo tuweze kuhamasisha uingizaji wa pesa kwa kutumia bandari yetu ya Tanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deodatus Mwanyika atafuatiwa na Mheshimiwa Tunza Malapo na Mheshimiwa Ali King ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze

kuchangia. Kwanza ningependa kutoa mchango wangu kwenye eneo la kilimo na biashara. Mpango huu ni mzuri, lakini unachangamoto hasa kwenye eneo hilo la kilimo na biashara ambalo ni eneo muhimu sana kwa uchumi wa nchi. Nianze kwanza ku-*declare interest* hata mimi ni mkulima wa chai kwa sababu nitachangia kwenye eneo la chai. Mpango huu kwa eneo la kilimo kwa maelezo ya Waziri mwenyewe haujaonyesha mafanikio makubwa kwa eneo la kilimo, ukuaji wa uchumi eneo la kilimo umekuwa mdogo na tunasema mchango wa kilimo kwenye pato la Taifa umekuwa mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo nalionna kwamba linaweza likaleta mabadiliko makubwa ni eneo la chai. Zao la chai kwa ujumla wake na sekta ya kilimo kwa ujumla wake imekuwa chini kwa sababu moja kubwa, uwekezaji katika eneo la chai umekuwa mdogo, uwekezaji upande wa Serikali lakini hata uwekezaji kwa upande wa watu binafsi. Kwa hiyo ipo haja ya kuongeza kwa kiasi kikubwa sana uwekezaji kwa namna nyingi na nitazitaja hata chache tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo kubwa ni kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya wakulima wa maeneo ya chai. Ukiangalia kwa undani kabisa utaona wazi kabisa utaona wazi kabisa wakulima wetu wa chai hasa wadogo wadogo bado wana-*struggle* sana kuzalisha chai yao. Kule kwenye maeneo ya Njombe kuna viwanda vikubwa vyatya chai kama kumi na tisa. Viwanda hivyo vyote vinakuwa *own* na watu wa nje, wakulima wetu bado wanafanya njia za kizamani za kulima na hawawezi kutoa mchango mkubwa. Ni vizuri sasa Serikali ikajikita zaidi huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia eneo ambalo unaliona lazima tuungeze uwekezaji, ni eneo la ugani. Katika *global average* wakulima 400 wanatakiwa wahudumiwe na Mgani mmoja, lakini kwetu sisi hapa ni wakulima 1,100. Ukienda kwenye upande wa miundombinu ya umwagiliaji bado tuko nyuma sana, hatuwezi kwenda na kilimo ambacho tunategemea mvua hasa kwenye mazao ya chai na mazao ya *avocado*. Kwa hiyo tuna kila sababu, Tanzania mpaka

leo kwa eneo lilitolimwa kwa mwaka 2019, karibu hekta 13,000,000 ni asilimia 20 tu ambayo ina umwagiliaji kama hekta laki nane. Tunatakiwa twende juu zaidi na zaidi ili tuweze kuona tija kwenye eneo la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tu fungamanishe hii sekta ya kilimo ya *process* na eneo la Nyanda za Juu Kusini Njombe ikiwemo, ni eneo lenye *potential* kubwa sana ya kuwa *game changer* kwenye kilimo kama tutafanya uwekezaji mkubwa na tutaita uwekezaji. Hata hivyo, tukumbuke tuna wawekezaji kule wana-*struggle* kwa sababu ya tozo nyingi sana ambazo kwa kweli pamoja na jitihada za Serikali na tumeona kwenye kitabu hapa, lakini tozo bado ni nyingi sana. Kwenye chai peke yake kuna tozo zaidi 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu na kwenye hotuba ya Rais na kwenye Mpango tunakwenda kwenye kilimo cha biashara maana yake kilimo cha biashara unakuwa *competitive* ukilinganisha na wenzako. Tuwaangalie Kenya kilimo chao chai, tozo ziko mbili tu; Uganda wana tozo moja; sisi tuna 13. Twende kwenye *avocadona* matunda matunda tuna tozo karibu 45; pamoja na kazi nzuri ya serikali bado jitihada zinatakiwa zifanyike. Nafahamu kuna *blue print* inaendelea, lakini kwa kweli *impact* kwa wakulima bado ni kubwa na *negative*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee eneo la wakulima ambalo ni la viwanda sasa hivi vyaa chai vilivyopo. Nipende kusema wana mchango wao mkubwa, lakini wanaweza wakachanga Zaidi. Kuna mmiliki mwenye viwanda vyaa chai ametoka Kenya anaitwa DL, sasa hivi anashindwa hata kulipa mishahara, anashindwa kulipa *pension*, ni miezi 12 wafanyakazi hata *pensions* zao hazijalipwa, wafanyakazi wana maisha magumu, wakulima wana maisha magumu, wana mwaga chai. mahindi ukikosa mwekezaji au ukikosa mnunuzi utaweka ghalani, utauza mwaka unaofuata, lakini chai ukikosa mnunuzi unamwaga. Kwa watu ambao wanaisha maisha magumu wanatafuta mitaji kwa shida, wanalima chai, wana kila haki ya kuhakikisha kwamba wanasaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mwekezaji huyu ni moja, amenunua viwanda vya chai lakini hajakamilisha process nzima ya ku-*transfer* viwanda vya chai na sababu kubwa tunaambiwa ni *TRA* kwamba wanasesma kuna *capital gain tax* hajalipwa, lakini anayelipa *capital gain tax* ni yule aliyeuza. Kwa hiyo huyu anashindwa kwenda kukopa, anashindwa kwendelea, anashindwa kuchukua chai, watu wanamwaga chai yao, lakini kosa siyo lake. Sasa kama tunataka mpango huu na tunataka chai iweze kwenda kuzalishwa zaidi na malengo ya Serikali ni kufanya chai kama zao la mkakati liweze kuingia na pesa za kigeni; tuwaangalie wawekezaji hawa, hata huyu mmoja ambaye ana viwanda karibu zaidi ya vinne na anaajiri zaidi ya watu 2,000 na anasaidia kwa kutoa mbolea, kwa kutoa madawa kwa kulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nlende kwenye moja lingine la *avocado*, *avocado it is not be a big business*, *avocado can be a big changer*, tunaita *green gold*, kwa kweli tunatakiwa tujipange vizuri na naomba sana Serikali tunapozungumzia miundombinu wenzeshi, lazima tuangalie zao hili. Kwenye mazao ya mbao naomba niseme na nimalizie kwa kusema, wakulima na wafanyabiashara wa Njombe wana hali mbaya sana, kwa sababu tunahitaji mahusiano mazuri kati yao na *TRA*, tunapokwenda siyo kuzuri kwa maana watu wanaona hakuna faida ya kulima misitu, wamelima misitu hawawezi kuiuza, hawawezi kupata faida, ni jambo tunatakiwa tulitiliee maanani na Waziri wa Fedha ameshaandikiwa ili atoe nafasi kwa hawa Watanzania, wafanyabiashara wa Njombe waweze kukaa na *TRA* kuona namna gani wata-*improve*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tunza Malapo atafuatiwa na Mheshimiwa Ali King na Mheshimiwa Ahmed Abudulwakili ajiandae.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo. Awali ya yote

nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenisababisha mimi na wenzangu leo tukawa hai, tuko ndani ya Bunge hili Tukufu. Suala la nishati ya umeme, ukiangalia kwenye Mpango wa Pili, *target* ilikuwa kufikia *megawatt* 4,915 lakini zilizofikiwa mpaka sasa hivi 1,602.3. Maana yake lengo halijafakiwa, kwa hiyo kama Serikali inayokusanya kodi za wananchi ina wajibu wa kuhakikisha inafikisha malengo ambayo wameahidi kwenye Mpango.

Mheshmiwa Mwenyekiti, licha ya kutofikiwa hivyo, kuna suala lingine ambalo ni la muhimu sana nataka niliseme. Kumekuwa na kusema vijiji elfu kumi na ngapi vimefikiwa na umeme, lakini tuangalie katika katika vile vijiji ni nyumba ngapi zimeunganishwa na huduma ya umeme. Mpaka sasa hivi kwa mijini ni asilimia 39.9 ya nyumba ndiyo zimeunganishwa na umeme na kwa vijijini ni asilimia 24.3 ya nyumba ndiyo zimeunganishwa na umeme, maana yake una nyumba 100 kwa vijijini, ni nyumba 24 tu zilizounganishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu kwa Serikali kwa umuhimu wa nishati ya umeme wanapopeleka umeme vijijini, basi wahakikishe wanapeleka nguzo karibu na maeneo ya wanaoishi watu ili iwe rahisi kwa wao kujunganishia umeme kwenye nyumba zao.

## TAARIFA

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tunza Malapo, kuna taarifa Mheshimiwa Hussein Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa mchangiaji, vile vijiji ambavyo vimeshafikiwa na umeme ni vijiji zaidi ya elfu tisa na kitu, haya masuala ya kuunganisha ni kaya ngapi zimeunganisha ni yule mhusika, mwenye nyumba yake alipie na awashiwe umeme, siyo jukumu la Serikali. Nilikuwa nampa taarifa hiyo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tunza Malapo, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei. Kazi ya Serikali ni kupeleka huduma karibu na wananchi. Kuna nguzo kumi ndiyo mtu umfikie kwenye nyumba yake, unamwambia ajiunganishie kwa nguzo kumi? Tuache bla bla bwana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mdau wa elimu sana, elimu ni uwezo, tunategemea mtu ambaye anapata elimu aelimike aweze kupambana na changamoto zilizoko katika maisha yake au maeneo yanayomzunguka. Tatizo kubwa ninaloliona kwenye elimu yetu ya Tanzania, tunaanza kufeli tangu mtoto anapoingia darasa la awali. Kimataifa *ration* inayokubalika ni Mwalimu mmoja wa awali kwa wanafunzi 25, lakini katika nchi yetu Mwalimu mmoja wa awali anafundisha watoto 104. Pata picha watoto wadogo, Mwalimu anahitajika kila mtoto amfuatilie, amejua kuandika, hiki ameelewa, una watoto 104 darasani, unawafuatilia vipi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tatizo linaanzia hapo. Ukienda shule za msingi mimi sisemi, kila mmoja wenu anajua hali ilivyo. Mwalimu unapita uandike ubaoni hata pakupita hakuna, tunataka watoto wakifika vyuo vyaa katii, wakifika vyuo vikuu wawe na ujuzi wawe na uwezo, wameutoa wapi wakati msingi huku chini ni mbovu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, ione umuhimu wa kutafuta *data* zilizo sahihi ili kusudi madarasa ya kutosha yajengwe, madawati ya kutosha yapatikane, Walimu wa kutosha wapatikane; kwa sababu ndiyo maana tunaambiwa kuna *projection* una *project* kwamba leo wameingia watoto 2,000 maana yake mwakani wanaweza kuingia 2,500 au 3,000; unatakiwa ujiaandae leo, usiwaache watoto nyumbani unasema mpaka madarasa, mpaka madawati yatengenezwe ndio watoto waende shule. Serikali isipende kuzima moto. Kuna sensa ya watu, kuna wataalam wa kuangalia *population* ya watu, watumie hizo *data* katika kuweka miundombinu ya elimu ili kusudi watoto wasome katika mazingira yaliyo bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongelea bandari ya Mtwara; natokea Mtwara, Mbunge wa Mtwara. Wakati sisi hatujaingia Bungeni, mimi Tunza sijaingia Bunge mwaka 2015 kwenda huko nyuma, Bandari ya Mtwara ilikuwa inafanya kazi. Kipindi cha msimu wa korosho meli nyigi kubwa zilikuwa zinakuja katika Bandari ya Mtwara. Nini maana meli za korosho kuja katika msimu, maana yake watu wa Mtwara walikuwa wanapata shughuli za kufanya.

Sasa kwa masikitiko makubwa tangu Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani meli Bandari ya Mtwara hakuna. Ukiuliza unaambiwa meli zina kuja Dar es Salaam, korosho zisafirishwe kwa barabara mpaka Dar es Salaam, kwa sababu kuzileta Mtwara meli ni gharama hakuna mizigo ya kupakia kutoka Dar es Salaam kuja Mtwara. Naomba niullize, kipindi kile meli zilipokuwa zinakuja Mtwara mizigo ilikuwa inapatikana wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, kama wanaona hakuna mizigo ya kuja Mtwara, wajitahidini kukaa na wafanyabiashara wapunguze kodi ili na Bandari ya Mtwara itumike, mtu aone nikienda kupakia korosho Mtwara kuna ahueni fulani kwa sababu uchumi wa kwetu sisi watu wa Mtwara tunategemea asilimia kubwa korosho. Korosho ukienda kupakia Dar es Salaam tunawaacha vijana na wanawake wa Mtwara hawana kazi. Sasa hivi Mtwara ukienda kuko kama msibani, korosho haieleweki, zinapakiliwa Bandari ya Dar es Salaam, watu wa Mtwara wanafanya shughuli gani? Hapa wanassema wamewekeza bilioni mia moja hamsini na ngapi sjui, zinakwenda kufanya nini wakati hakuna mkakati thabiti wa kuhakikisha bandari ile inatumika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huo uwekezaji unaofanya uendane sambamba na kuchochea meli zije Mtwara ili kusudi zifanye kazi katika Bandari ya Mtwara. Kama ni *issue* ya tozo ya kodi, Waziri wa Viwanda akae na wafanyabiasha aone ni kwa namna gani anakwenda kuiboresha bandari ile iweze kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la muhimu kwenye zao la korosho bado kuna malalamiko mengi, wakulima wa korosho wanalamika, wanadai, ili kuepusha malalamiko hayo na watu wapate haki zao, naishauri Serikali imwombe CAG, akafanye ukaguzi maalum, wale watu wote wanaodai walipwe madai yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo kidogo; kuna siku nilikuwa kwenye semina iliyoandaliwa na Wizara ya Kilimo, naambiwa nyanya za kwetu zinaoza, zinatupwa kwa sababu hazina *fibber* zinazotesheleza kutengeneza *tomato source*, mananasi ya kule Mkuranga na kwingine, yanaoza yanatupwa kwa sababu hayana ubora, maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiniambia mimi Serikali imeshindwa kupeleka pesa, wataalam wetu wakatafiti, wajue hitaji la soko ni nini. Mkulima akiletewa mbegu bora atalima. Leo mkulima analima, anavuna nyanya zinaishia kuliwa na mbuzi, lakini leo tunamwambia akalime. Hivi nyie mnaijua kazi ya kulima, ilivyo ngumu. Kwa hiyo tunataka wakulima walime, wazalishe kwa tija na mazao wanayopata yaweze kutumika katika viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba hayo niliyoyaongea yafanyiwe kazi kwa maendeleo ya watu wa Kusini na kwa Taifa kwa ujumla. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ali King atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Abdulwakil na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nashukuru sana kwa Mwenyezi Mungu kutupa uhai na uzima, lakini pili, nikishukuru wewe kwa kunipa hii nafasi kuweza kujadili Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda katika maoni yangu kwenye Mpango huu, kuna msemo mmoja wa kiaribu unasema *lisani-l-hali haswa umilisan-l-bakabi*; lugha ya hali ilivyo ni fasaha zaidi kuliko lugha ya maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo mzungumzaji aliyejita anasema kwamba Serikali hii iliwardanganya watu katika umeme, umeme haukufika vizuri vijijini. Wewe tazama hali ya kura zilizokuwemo humu zilivyoenea, ni fasaha Zaidi, halafu tazama na zile zilizobakia, kwa hiyo hii lugha na hii hali ya humu ndani ni fasaha zaidi kuliko maneno. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite moja kwa moja katika kuboresha mapendekezo ya huu Mpango. Wizara ya Fedha imetuletea Mpango. Katika Sura ya Sita, wameeleza ugharamiaji wa Mpango na wamesema kwamba Mpango huu utagharamiwa kwa jumla ya triliioni 114. Wakasema sekta ya umma triliioni 74 na sekta binafsi triliioni 40, lakini tukiangalia Mpango uliopita, Serikali ilisema kwamba sekta ya umma Mpango wote utaghari mu triliioni 107, sekta ya umma itatumia triliioni 59 na sekta binafsi triliioni 48. Lakini matokeo baada ya miaka minne, sekta ya umma imetumia triliioni 34.9 ambayo ni sawa na asilimia 77 ya miaka minne; lakini sekta binafsi imetumia triliioni 32.6 ambayo ni sawasawa na asilimia 85.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye sekta binafsi, hizi triliioni 32, ni sawa kwa miaka minne, ina maana kwamba kwa miaka mitano sekta binafsi itafika triliioni 40.75. Sasa tumesema tutafanya maboresho kwenye sekta binafsi, huu Mpango umeeleza mambo ya *blue Print*, umeeleza mambo ya uwekezaji, umeeleza kuondosha vikwazo vingi. Sasa kwa nini tumeipa sekta binafsi triliioni 40, wakati mwaka huu bila marekebisho yoyote, tunaweza kufika triliioni 40 ndani ya miaka hii mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naiomba Serikali ikafikirie tena katika ugharamiaji wa Mpango huu kuwa sekta binafsi haitoshi kwa triliioni 40, tunao uwezo wa kufika zaidi ya triliioni 40 endapo yale maboresho katika Mpango huu kuhusiana na sekta binafsi yatafanyika. Hilo ndilo pendekezo langu la kwanza, kwa sababu tukifika miaka mitano kamili tutakuwa tumeshapita triliioni 40. Je haya maboresho *plus* tutapata ngapi? Naomba hilo wakalifanye kazi, watakapokuja na Mpango waje watueleze nini kinaweza kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nizungumzie katika Sekta ya Uvuvi. Tumepanga kukuza pato la Taifa kutoka asilimia 7 kwenda asilimia 8; pato la mtu mmoja mmoja dola 1,080 mpaka dola 3,000. Kwenye Sekta ya Uvuvi tunesema kwamba inachangia katika pato hili la Taifa kwa asilimia 1.8 tunataka ichangie asilimia tatu. Ukuaji wa sekta tutatoka kutoka asilimia 3.7 mpaka asilimia 3.9. Uzalishaji kutoka tani 497,000 mpaka tani 600,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa uvuvi huu wa bahari kuu hiki kiwango tulichokiweka ni kidogo kutokana na *activities* zinazotakiwa kufanya katika uvuvi wa bahari kuu. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijaribu kuweka tena haya malengo kwa sababu ukuaji wa asilimia 3.9 tunaweza tukazidi endapo tutatumia fursa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo moja ambalo sikuliona katika Mpango huu. Katika Sura ya Tano Mpango huu umezungumzia mambo mawili; ununuzi wa meli na ujenzi wa Bandari ya Mbegani lakini uvuvi wa Bahari Kuu una mambo mengi ambapo tukitazama hotuba ya Rais imesema kwamba kutakuwepo na viwanda vya uchakataji wa samaki. Hili tungeliona pale katika ile *item* ya 13, katika lile jedwali ambalo limeeleza *flagship project*, lakini hapa tumekosea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu; sekta binafsi ili tuweze kuiwezesha kuingia katika uchumi huu wa uvuvi wa Bahari Kuu ina maana kwamba ni lazima tupime tuna samaki wa kiasi gani. Hata gesi, ili uchimbe gesi unatakiwa ujue kwamba ipo gesi kiasi gani. Tuna ukubwa wa bahari na tunajua ukubwa wa bahari, lakini wingi wa samaki tunaulewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta binafsi wanahitaji kuelewa wingi wa samaki halafu wao watakwenda kukopa. Wakiandika *proposals* zao za kutaka maombi ya kupewa fedha ni lazima waeleze *viability* ya mpango. *Viability* ya mpango, moja, ni lazima waoneshe *cash flow* ambayo itakuwa inapatikana kutokana na huo uvuvi wa samaki. Kwa

hiyo, ni lazima wingi wa samaki nao utajwe ili kuwapa kigezo hawa wenzetu wa sekta binafsi waweze kukopa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele imegonga Mheshimiwa.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Shukrani sana. Mheshimiwa Ahmed Abdulwakil, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, Mheshimiwa Seif Gulamali ajiandae.

**MHE. AHMED YAHYA ABDULWAKIL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Natumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi na kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako hili tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapohapo nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kwahani kule Zanzibar ambao kwa imani moja wamenileta hapa niwe mwakilishi wao. Walikuwa na simanzi kwa vile wanaona kama wameondokewa na Mbunge mwaminifu, mtiifu na mwenye bidii, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nawakahikishia kwa nafsi yangu kwamba mimi naweza na nitawapa utumishi uliotukuka na kufuta machozi madogo madogo ambayo walikuwa wanayatoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu na Mawasiliano na kwa kiasi fulani nitajikita zaidi katika kuuchangia Mpango huu wa Miaka Mitano. Nchi yetu kama hii kwa kitendo cha Rais wetu mpPENDWA kuanzisha reli iendayo kasi kwa kutumia fedha zetu za ndani kwa kipindi

hiki ni suala la kumpongeza na kumtakia mafanikio mema katika safari hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilibahatika kidogo kusafiri (mtundu wa kusafiri), ninakona reli kama hii ya Shirika la Reli la Marekani linaitwa Acela inayochukua abiria na mizigo kutoka Washington DC mpaka New York kwa mwendo wa saa nne na nilipanda shirika hilo. Leo nchi kama yetu ya Tanzania hili ni jambo la mfano, Rais wetu mpendwa ameidhinisha zaidi ya shilingi trillioni saba na kuendelea na reli inaendelea. Kwa hiyo, hili ni jambo la kuigwa na huyu ni Rais wa kuombewa dua kila siku kwa madhehebu yote ili aweze kuishi na aweze kutufikisha salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuchangia kuhusu Shirika la Ndege la ATC. Shirika la Ndege la ATC kila mmoja leo anaona mafaniklo yake na limeweza kwa mara ya kwanza katika utawala wa Dkt. John Pombe Magufuli kutoa gawio (*dividend*) kwa Serikali. Kwa hiyo, hili ni jambo la mfano; amefufua shirika hili na leo lina ndege zaidi ya tisa na nyingine za mizigo ziko mbioni zinakuja. Kwa hiyo, hili ni jambo la mfano katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni ilivyointia *COVID* tumeona *deterioration* ya bidhaa kuja kwetu Tanzania. Shirika la Ndege la Ethiopia limetumia nafasi ya kuchukua mizigo ya wafanyabiashara kuleta Tanzania. Ni jambo la faraja kusikia kwamba ndege ya mizigo inakuja na iko njiani. Kwa hiyo, uchumi wetu utazidi kuhuika kwa kuwa sasa hivi tunatumia ndege yetu wenywewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hivyo tu, nadokeza kwamba hivi karibuni shirika hili baada ya hii *COVID* kuondoka, lina mpango wa kuazisha safari za kuelekea Gatwick pamoja na London, Heathrow. Kwa hiyo, Watanzania hapa watakuwa wanapanda *direct flight* kutoka *Julius Kambarage Nyerere Airport* mpaka Gatwick. Kwa hiyo, hili ni jambo la mfano kwa Shirika la Ndege na hizi zote ni juhudhi za Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli; hongera sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho katika uchangiaji wangu, natoa ushauri kwamba uvuvi wa Bahari Kuu ambao unachochaea uchumi wetu uangalie ofisi za Zanzibar. Hapa katikati utoaji wa leseni ulisababisha ofisi ya Zanzibar kidogo kutikisika. Wavuvi wenye meli walikuwa wengi lakini alibakia mvuvi mmoja tu ndiye aliyepewa leseni. Kwa hiyo, zipo dalili za kuwasaili ikiwa hali imetengemaa na wakati wa utoaji wa leseni za meli za uvuvi wakaangalie kwa makini sana kutoa leseni kwa wakati na *fairilii* kusudi ile *shake* ya ofisi isije ikatokea tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jumla mimi naunga mkono mpango huu kwa asilimia 100 ili mambo yaende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Gulamali, Mheshimiwa Abubakari Asenga ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Mpango wa Tano wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ya msingi tunapotaka kufanya mabadiliko ya kiuchumi na kwenye biashara. Ukichukua mfano wa nchi ya China ilipotaka kufanya mabadiliko yake kwenye masuala ya uchumi na biashara zaidi ya miaka 40 walikuwa wakiendelea kusuguana na sheria na sera zao. Mipango na mikakati yao ilikuwa imekaa vizuri; ilikuwa ikijali muda, lakini ukienda kwenye mambo ya sheria na sera zao zilikuwa zinawarudisha nyuma na zikafanya uchumi wao kuendelea kuwa duni, ulishindwa kuendelea kukua, tegemezi na usiozingatia ushindani wa kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye walipoamua sasa kuanza kubadili sera na sheria zao ndipo walipoanza kuleta maendeleo makubwa na ndani ya miaka nane kwa ripoti za Benki ya Dunia, walikuwa wanakua mara mbili zaidi ya *GDP*

ambayo ilikuwa ni kwa asilimia 9.5. Ndipo walipoweza sasa kutoa umaskini kwa watu wao zaidi ya milioni 800 maana tunapoongelea China ni watu zaidi ya milioni 1,400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa Mpango huu wa kwetu wa Maendeleo wa Miaka Mitano ni mzuri na umezingatia *standard* na spidi au umejikita katika muda lakini kikwazo kikubwa kitakachokuja kutukuta, katika ukurasa wa tano wa maeneo ya muhimu ya kuzingatia ambao Mpango unaeleza, umeeleza mambo mazuri lakini haukuweka misisitizo katika kuhakikisha kwamba tunabadili na sisi sheria na sera zetu ambazo huwa zinatusababisha tusiende kwa spidi au tusiende kwa wakati ule ambao tumeupanga, hicho kipengele hakijawekwa. Kwa hiyo, tunaomba tushauri kwamba katika Mpango huu tujaribu kuangalia namna gani tutabadilisha sheria na sera zetu ili ziweze kuendana na muda ili tuweze kuutekeleza huu mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi sana tumekuwa tukipanga vitu vingi lakini unakuta kuna sheria zinakinzana. Tunakwenda kwa spidi tunataka kuinua utalii, Mpango unatuambia kwamba tutoke katika watalii 1,500,000 mpaka itakapofika 2025 tuwe tumefika watalii 5,000,000, lakini kuna sera nyingine ambazo zipo sasa zinahusiana na masuala ya kutoa vibali au *permit* za kuishi, unakuta zinakinzana na ile sera ya sisi kuboresha spidi ya kuendeleza utalii wetu au kuboresha spidi ya uwekezaji. Mwekezaji anakuja katika taifa letu, amekuja na mtaji, anakuja kupambana na Sheria ya *Labour* ambapo yeye anataka kuja na mke wake lakini sheria inamkatalia asije na mke wake au anapata usumbufu kupata *permit* ya kuishi na mke wake. Sasa unakuta vitu kama hivi vinakuwa vinakinzana, tusipoziangalia sheria na sera zetu, bado hatutaweza kuutekeleza huu Mpango kwa wakati kama ambavyo tunatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukajifunza kutoka kwenye Sekta ya Madini, namna ambavyo madini yamechangia kwenye maendeleo yetu katika Mpango wa Pili, ni kwa sababu pia yalifanyika mabadiliko makubwa ya kisheria kwenye sheria za madini na ile ikatusababisha

tukaenda vizuri. Kwa hiyo, ushauri ni kwamba tunaomba sheria na sera nazo ziangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kujua kwamba tuna mkinzano wa kisheria na mipango yetu utaona mara nyingi sana mambo yetu mengi yanakwenda kwa waraka, matamko, yanakuwa kama ya zimamoto hivi. Kwa sababu kama sheria ingekuwa inakwenda sawasawa na mipango, hivi vitu vya zimamoto, kwenda kwa matamko na nyaraka visingekuwa vinakwenda namna hii. Hii inaonesha namna gani sheria yetu inawezekana haiko sawasawa na mipango ile ambayo tunaiweka. Kwa hiyo, tujitahidi kubadilisha sheria zetu na tujitahidi kuangalia mabadiliko makubwa kwenye sera zetu ili tuweze kwenda sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wetu unatakiwa ujengwe sasa kwa misingi ya soko. Tositengeneze tu mpango kwamba tulime mazao haya zaidi, tulime kitu hiki au kile zaidi, hebu tuangalie soko lina uhitaji gani. Kama tunasema tuna uhitaji mkubwa wa mafuta ya alizeti, huko ndiko sasa tutengeneze mpango namna gani tunawashawishi wakulima ili waveze kulima alizeti na namna gani tunatengeneza sheria ambayo itazuia uingizaji wa mafuta ya alizeti kwenye nchi yetu ili soko letu la ndani lenyewe lianze kuwa ni soko kabla hatujategemea soko la nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, lazima ...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Seif Gulamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Asenga, Mheshimiwa Nusrat Hanje ajiandae.

**WABUNGE FULANI:** Gulamali hayupo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mheshimiwa Anna Lupembe ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kupata dakika tano za kuchangia Mpango wetu wa Maendeleo Awamu ya Tatu. Ukiusoma ule mpango na hotuba ya Mheshimiwa Waziri utaona wazi kwamba umejikita katika shabaha nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza unasema, kuhakikisha kuwa uchumi wetu unakua kati ya asilimia 6 na asilimia 8. Pili, kuhakikisha kuwa mapato ya Halmashauri zetu yanatoka asilimia 15 mpaka 16.8 ya pato la Taifa. Tatu, ni kulinda mfumuko wa bei (*inflation*) tubaki katika *single digit* ya asilimia 3 mpaka asilimia 5. Nne, kuendelea ku-*maintain* hifadhi ya fedha za kigeni walau kwa miezi minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kilombero kazi yangu kubwa ni kuwakilisha mawazo na maoni yao kuhusu Mpango huu. Mathalani, ili kufikia shabaha hii ambayo imeandikwa hapa na Mheshimiwa Waziri katika Mpango wetu wa Halmashauri kujitegemea kwa hadi asilimia 16.8, kama walivyosema Wabunge wenzangu wengine waliotangulia, ni wazi kwamba tukijikita katika kilimo tunaweza kufanikisha jambo hili. Kwa mfano kwenye zao la miwa ya sukari, Mheshimiwa Rais alishaelekeza kwamba nchi yetu ijitegemee kwa sukari na wakulima wetu wamewekeza katika zao hili. Hata hivyo, taarifa za Wizara katika Mpango zinasema tunatupa miwa tani milioni moja kwa mwaka. Uwekezaji wa miwa peke yake katika Jimbo la Kilombero utakuza mapato ya Halmashauri kwa *two percent* na hapo tayari tutakuwa tumefikia shabaha ya pili ya Mpango wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni miradi mkakati katika Mpango wetu wa Maendeleo. Mathalani, Serikali imesema itaendelea kuwezesha miradi mkakati ili

kuziwezesha tena Halmashauri. Jimbo langu la Kilombera na wananchi wetu, tayari wana andiko kuhusu soko na namna gani soko na stendi zitakavyokuza mapato ya Halmashauri kufikia shabaha ya Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne ni kilimo kwa maana ya mpunga. Amezungumza mchangiaji wa kwanza, Mheshimiwa Prof. Muhongo hapa kwamba tuwekeza katika kilimo ili tuweze kuendelea. Amesema pia watu duniani ni karibu bilioni saba na nusu ya watu duniani wanatumia mpunga. Jimbo la Kilombero linazalisha mpunga kwa zaidi ya asilimia 70. Katika Mpango huu endapo tutawekeza katika kilimo cha mpunga kwa kiwango kubwa, tunaweza kufikia shabaha ya Mpango huu ambao ni kukuza mapato ya Halmashauri kutoka asilimia 15 mpaka asilimia 16.8. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine ni mambo ya miundombinu. Mheshimiwa Waziri kama ulivyozungumza, mara kadhaa tunesema katika kilimo ambacho tunataka kukiza ili tuweze kufikia maendeleo ya ukuaji wa uchumi kwa asilimia 6 -8 lazima tuwe na miundombinu ya kutosha ya kusafirisha mazao ya wananchi na wakulima wetu vijiji. Ndiyo maana mara nyangi tukisimama hapa tunazungumzia habari ya barabara ambazo zimekuwa historia kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri tukajikita pia katika kuboresha miundombinu yetu. Mathalani katika Jimbo la Kilombero, tuna barabara hii tunaizungumzia mara zote ya Ifakara – Kidatu ambayo itaunganisha Wilaya za Ulanga, Malinyi, Mlimba, Kilombero, Mikumi na Mkoa wa Morogoro. Hatimaye itawawezesha wakulima wetu kuuza bidhaa zao vizuri na kuchangia katika pato letu la Taifa na kuchangia katika Mpango wetu wa maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni fursa mbalimbali ambazo zinatokea katika kilimo kwa kuwakumbuka wananchi hawa. Matahlani, alizungumza mama yangu mmoja Mbunge wa Morogoro hapa kwamba zamani kulikuwa na huduma za matrepta katika vijiji vyetu. Katika

Mpango huu wa Maendeleo ambao tumesema asilimia karibu 80 ya wananchi ni wakulima, endapo tutarejesha matrekta katika vijiji vyetu tunaweza kufikia malengo yetu na hasa kwa Mkoa wa Morogoro ambao mimi ni Mbunge katika moja ya majimbo yake na umechaguliwa kuwa ghalaa la taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, endapo mpango wa maendeleo utakumbuka hii mikoa ambayo ni ghalaa la taifa, *automatically* tutakuza kilimo na tutapata maendeleo ya haraka na kufikia shabaha ya Mpango ya uchumi kukua kwa asilimia 6 mpaka 8, mapato ya Halmashauri kutoka asilimia 15 mpaka 16.8 kwa pato la Taifa, tatalinda mfumuko wa bei na tunaweza kuuza mazao yetu nje kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nawasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Seif Gulamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mheshimiwa Anna Lupembe ajiandae.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa wa Tatu. Kwanza naipongeza Wizara kwa Mpango tulioumaliza wa 2016 – 2021, pia kwa Mpango huu wa 2021 – 2026. Mpango ni mzuri, tunapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nishauri tu kwenye sekta ya kilimo. Tumekuwa na kawaida ya kutoa fedha nyingi sana kwenye Wizara mbalimbali hasa za Ujenzi, Afya na Elimu. Naomba kama Taifa, katika kuelekea kukabiliana na Mpango huu wa Tatu, tuwekeze fedha nyingi sana kwenye sekta ya kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu tumekuwa na uzalishaji wa mazao mbalimbali kama kahawa, korosho, mahindi, mpunga na mengineyo. Pamoja na mazao hayo

yote, ukienda kuangalia katika Mataifa ndani ya Afrika yanayo-export huwezi kukuta nchi yetu katika nchi 10 bora zinazouza mazao yetu nje ya nchi. Sasa tuangalie jinsi gani tunaweza tukatengeneza Mpango ambao ukatufanya nchi ya Tanzania kuingia angalau hata kwenye kumi bora kwa nchi za Afrika zinazo-export mazao yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na Mipango mingi sana. Toka mpango wa Kwanza, wa Pili na sasa tuko Mpango wa Tatu. Hata hivyo, katika Mipango yote hii hatujawekeza vya kutosha katika sekta ya kilimo. Tukichukua fedha zetu tukaenda kuwekeza kwenda uchimbaji wa mabwawa, kwenye maeneo yenye mvua za kutosha, tukakusanya maji, tusiruhusu maji yetu yakapotea; pia tukatengeneza skimu za umwagiliaji; tukatengeneza utaratibu wa kuzalisha mazao ya kutosheleza ndani ya nchi yetu; na tukatengeneza mazingira ya balozi zetu zikafanya kazi ya kutafuta masoko ya mazao ya wananchi wetu. Mheshimiwa Rais anasema anataka kuzalisha mabilionea Tanzania; mabilionea wako kwenye kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kule Ulaya wakati wanaendelea ilikuwa ni masuala ya kilimo. Hata biashara ya utumwa ilikuwa ni biashara ya kilimo. Tuwekeze kwenye kilimo, tutapata fedha; tutapata kilimo cha kutosheleza, tutauza nje, tutapata dola, tutatengeneza ajira ndani ya watu wetu, ajira zitaongezeka, tutapunguza tatizo la ajira kwa vijana wetu na tutaongeza mzunguko wa fedha ndani ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiangalia, kikifika kipindi cha masika hata mabasi hayana abiria, hata treni zinapungua abiria, hata ndege abiria wanapungua; watu wanawekeza kwenye kilimo. Mpango wetu huu ujielekeze kwenye kuwekeza angalau hata shilingi trilloni moja, tuombe tupeleke kwenye kilimo. Tuchukue trekta tuwapelekee wakulima wetu kwenye kila kijiji, tuhakikishe kuwa kuna trekta, kuna zana za kuwawezesha wakulima wetu wafanye kazi ya kilimo cha uhakika, sasa hivi wanatumia kilimo cha jembe la mkono, kilimo ambacho hawana uhakika nacho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuptitia kilimo tutajikomboa, tutapata utajiri, tutapata dola za kutosha, mzunguko wa fedha utakuwa mkubwa, umaskini utapungua na njaa tutakuwa hatuna. Nchi yetu kijiografia imebarikiwa na ardhi ya kutosha, ina mvua za kutosha, imebarikiwa kuwa na kila kitu, tumeshindwa kuwekeza kwenye kilimo, uwezesho ambao inatakiwa tuone matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo kwenye kilimo bado hatujayaona. Mheshimiwa Waziri, kama kweli tunataka tukomboe Taifa hili, tuwekeze kwenye kilimo. Tunatambua wananchi wetu wanavyohangaika, asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima. Sasa kama ni wakulima mbona hatupeleki fedha za kutosha kwenye kilimo? Kwa nini tusiende kujenga mabwawa? Kama tumefanya operesheni ya ujenzi wa shule, operesheni ya ujenzi wa vituo vya afya, tutafanya operesheni ya ujenzi wa mabwawa na ujenzi wa skimu za kumwagilia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nusrat Hanje, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge ajiandae.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi. Naomba nianze kwa kutoa masikitiko yangu kwa Waheshimiwa Wabunge vijana ambao wako kwenye Bunge hili ambao kimsingi zaidi ya asilimia 60 ni vijana. Natoa masikitiko yangu kwa sababu kama vijana, tunao wajibu kama ambavyo kila kizazi kina wajibu wake, kama vijana tunao wajibu wa kulisaidia Taifa hili kwa sababu tuna Tanzania moja tu, sasa haiwezekani vijana tuko zaidi ya asilimia 60 kwenye Bunge hili lakini tunashindwa kutoa msaada kwa ajili ya kusaidia Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe wito kwa vijana ambao wengine wameshachangia, lakini najua wanaweza kuchangia tena kwa maandishi wakashauri yaliyo

bora na mema kwa ajili ya Taifa hili. Ambao bado, nawashauri, hatuna Tanzania nyingine, tuna Tanzania hii moja, tutoe michango yenye tija kusaidia Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mpango wa Mwaka Mmoja...

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat, nasikia kuna taarifa mahali. Hebu ngoja tuelewane kidogo. Subiri kwanza Mheshimiwa Saashisha.

Mheshimiwa Nusrat, takwimu za kuwatuhumu vijana wote humu ndani, unamaanisha hakuna kijana aliyesimama akatoa mchango! Yaani wataanza kutoa mchango baada ya wewe kutoa mchango? Maana umeisema kwa namna kana kwamba vijana wote waliochangia, hakuna wazo walilotoa kabisa. (*Makof*)

**MBUNGE FULANI:** Afute kauli.

**MWENYEKITI:** Hiyo haikai sawasawa. Nanyi mnakumbuka takwimu alizozitoa Mheshimiwa Spika humu ndani. Mimi nilisikiliza michango yote, nami huhudhuria Bunge kila siku, Wabunge vijana wanafanya kazi nzuri.

**MBUNGE FULANI:** Alikuwa gerezani, arudishwe ndani.

**MWENYEKITI:** Wanaishauri Serikali, wametoa mawazo ya kuboresha maisha ya vijana. Wameeleza kuhusu mikopo, kuwekeza kwenye mitandao, kilimo na kuhusu Benki ya Vijana. Tunataka nini jamani? Mheshimiwa Nusrat, ongezea pale ambapo wenzako wamechangia. Lile ambalo wenzako hawajalionia, changia wewe, lakini usioneshe kana kwamba hakuna kijana anayetoea mchango humu ndani isipokuwa wewe. Hapana, hiyo haikai sawasawa. (*Makof*)

**MBUNGE FULANI:** Anawaza kufukuzwa kwenye chama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat endelea. (*Makofi*)

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Labda ningefika mpaka mwisho ndiyo mngejua namaanisha nini.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni-*recognize* kwa waliyozungumza, kwa sababu kimsingi hakuna tupu iliyo tupu kabisa. Kwa hiyo, kuna waliyoyazungumza.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hanje, ngoja kwanza. Hebu tutulie kidogo.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimesimama.

**MBUNGE FULANI:** Kutachafuka humu ndani! Vijana tumeongea, tumefanya kazi kubwa! Kutachafuka humu!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimesimama, kwa hiyo, mkae. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tuelewane jambo moja. Nimeeleza hapa kwa kirefu nikiwa nimekaa. Nimelazimika kusimama kwa sababu Bunge hili watu wanaotakiwa kusimamia utaratibu ni wale wanaosimamia vikao. Na mimi nimeeleza vizuri; michango ya vijana waliopita, wa vyama vyote ambao wameshachangia, wamefanya kazi nzuri. (*Makofi/Kicheko*)

Hiyo michango waliyooitoa ni ya muhimu yote. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Sana!

**MWENYEKITI:** Hakuna kijana aliyesimama hapa ambaye hajatoa mchangano wa muhimu kwenyepapendekazo haya ya Mpango. Kwa muktadha huo, ndiyo maana nimemwambia Mheshimiwa Nusrat, naye ni kijana, aanzie pale ambapo wenzake wameishia, achangie mchangano wake. Yale ambayo wanaona...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mtulie kidogo, mkitajwa majina, mnakuwa wa kwanza. Mtulie msikilize. Nikiwa nimesimama hakuna mtu anaruhusiwa kuzungumza. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Kweli! (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tuelewane vizuri; na tuheshimiane. Nikiwa nimesimama, Bunge linatakiwa kutulia.

**MBUNGE FULANI:** Sawa.

**MWENYEKITI:** *It is only me who should be speaking because I have the right to speak.* (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, nikiwa nazungumza, kila mtu anapaswa kunyamaza. Ndiyo kanuni zetu zinavyosema. Tusome Kanuni, tuzielewe ili humu ndani tuheshimiane kama tunavyoitana Waheshimiwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, hoja ya kwamba hakuna tupu, tupu kabisa, hakuna Mbunge ye yote aliye m tupu humu ndani. Kila Mbunge analo jambo ambalo wale waliomtuma wana amini atalifanya humu ndani. Ndiyo maana kanuni zinamlinda kila Mbunge ana popata fursa ya kuchangia. Nami ni kazi yangu kumlinda kila Mbunge kwa mujibu wa kanuni zetu. (*Makofi*)

Bunge letu hili, alishasema Mheshimiwa Spika wakati linaanza, tukiamua kuliletea dharau, tunajidharau wenyewe. Tukiamua kuli heshimu, tunalitafutia heshima sisi wenyewe. Kwa hiyo, humu ndani tuheshimiane kama ambavyo sisi tume amua kuheshimiana na wale walio tutuma wanatuita Waheshimiwa. Kila Mbunge anao mchango wake, hakuna Mbunge aliye tupu humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nizungumze, kwa sababu mipango ilikuwa imepangwa kwa miaka 15 kwa miaka mitano mitano, *for the last ten years*, ripoti za CAG zinaonyesha kuna failure kubwa sana katika utekelezaji wa mipango. Bajeti zinapangwa, mambo haya endi kwa sababu...

**MHE. JAQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haijawahi kutokea Mbunge akaweka mapendekezo au akazungumza...

**MHE. JAQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat kuna taarifa. Mheshimiwa Jaqueline Msongozi.

**MHE. JAQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nataka tu nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumza, kwanza afute kauli yake aliooongea kwanza, halafu ndiyo aendelee na mchango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.  
*(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walzungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimeshatoa maelezo ya namna ya kwenda kuanzia hapa tulipo. Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nazungumza kwamba, tunafeli kwa sababu hatuna sheria. Ibara ya 63(3)(c) inaruhusu Bunge kutunga sheria ya kusimamia mipango kwa ajili ya kusaidia uwajibikaji na kusaidia mipango kufanya kazi. Mpaka sasa *for the last ten years* hatujawahi kuletewa Muswada. *By then* mimi nimekuja lakini hakuna Muswada uliowahi kuletewa hapa Bungeni (*If I am not right*, kuna wakongwe watasema) kwa ajili ya kusaidia ufanikishaji na usimamiaji wa mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kila siku tunapanga, tunarudi hapa kwenye kilimo. Tunaona kabisa tumetoka hatua moja, tumeenda hatua mbili mbele, tumerudi nane nyuma. Tunarudi tunasema tunapanga tena. Bajeti haiendi mathalan...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** ... bajeti ya maendeleo imetekelizwa kwa asilimia 17.55.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat kuna taarifa. Mheshimiwa Ndaisaba.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kumpatia taarifa Mheshimiwa Nusrat. Katika maelezo yake amesema kwamba tunafeli kwa sababu hatuna sheria ya kusimamia mipango. Naomba nimfahamishe kwamba kila jambo linalotungwa; bajeti ya Serikali, lina sheria mama na lina-fall/kwene specific category ambayo ina sheria zake. Ukienda kwenye kilimo kuna sheria, kwenye maji kuna sheria, kwenye barabara kuna sheria. Sheria zile ndizo zinazoratibu utekelezaji wa mipango ya Serikali

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiyo sheria nyingine anayotaka iibuke sheria juu ya sheria ni ya namna gani? Naomba apooke taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei hiyo taarifa kwa sababu nimezungumza kitu kingine na amezungumza kitu kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wabunge sasa hicho nilichokizungumza kama vijana tungeweza kusimama pamoja tukashauri Serikali ilette Muswada kwa ajili ya kuhakikisha mipango tunayoipanga, itekelezwe ili tuepuke *budget reallocation*, tuepuke kutokupeleka bajeti kama zinavyopangwa kwenye Bunge la Bajeti, wanapanga bajeti hazipelekwi, Mpango wa Maendeleo...

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** ... bajeti ya maendeleo kwenye kilimo imepelekwa asilimia 17.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** ...asilimia 82 haijapelekwa...

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa Mheshimiwa Nusrat hii itakuwa taarifa ya mwisho. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Hussein Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji anayeongea ni kana kwamba sisi wazee ama wenye umri mkubwa, hatustahiki kuchangia Mpango wa Maendeleo. Tumeletwa na wananchi na wametuamini pamoja na umri wetu kuja kuchangia maendeleo na kufikisha mipango yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa, vijana wanataka kuleta ubaguzi wakati tumeongoza kwenye kura kwa asilimia nydingi pamoja na umri wetu mkubwa. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumsikilize. Mheshimiwa Nusrat, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mzee wangu shikamoo! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaheshimu wazee wote, lakini tunafahamu hata Wamasai wapo humu ndani, morani; huwezi kufananisha *age*. Yaani hiyo *age conflict*. Ila nawaheshimu sana wazee wangu. Mpo! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumza kwamba bajeti ya maendeleo kwenye kilimo haijaenda kwa asilimia 82. Tuna shida ya mbegu kwenye Taifa, tuna tatizo la

mbegu kwenye Taifa, lakini Serikali imetenga mashamba tisa ya kuzalisha mbegu. Ni shamba moja tu ambalo linazalisha mbegu, linafanya kazi mwaka mzima. Mashamba mengine yote nane yanategemea kilimo kwa kudra za Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwenye jambo moja. Mheshimiwa Spika juzi alivyokuwa kwenye kitu alitoa mfano akasema anatamani tupate kitu cha ziada kuwasaidia vijana wetu, anachukia kuwaona wako kwenye *pool table*. Naomba ku-declare *interest*, mimi ni Mwalimu. Kama nchi, tuna tatizo kwenye elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika elimu, watoto wetu wanakosa vitu vitatu vyta msingi na Waziri wa Elimu yupo asikilize. Elimu yetu haina *career guidance*, haina *personal development*. Leo tunazungumza *soft skills*, wasomi wengi wanaotoka vyuo vikuu, inawezekana nikiwemo mimi na wengi wetu humu na wengine wako nje, tunakosa vitu vyta msingi. Tunafundishwa kwenye *Civics Communication Skills*, tunafundishwa *self-esteem, self-confidence* na nini, lakini tunashindwa ku-connect na maisha halisi. Ndiyo maana kuna *motivation speakers*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu Mheshimiwa Eric Shigongo yule pale anaelewa, ndiyo maana leo kuna *motivation speakers* wengi kwa sababu tunashindwa, yaani hatuwezi ku-connect maisha ya shule na nini kipo mtaani, ndiyo maana watu hawawezi kujiongeza. Falsafa ya Kuanzia sokoni, watu walitakiwa wajifunze shule, siyo wanamaliza shule, ndiyo wanatoka wanakuja kuambiwa kwenye biashara tuanzie sokoni. *No!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna kitu kingine cha msingi tunakosa. Leo Waheshimiwa Wabunge wanakalishwa chini wanafundishwa *investment*, shule wanasoma pesa, lakini hawasomi *financial management*; elimu yetu inakosa *financial management*; tunasoma *Book Keeping* na *Commerce* (makabati), haina reality kwenye ukweli. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikatoa mchango wangu pia kwenye maandishi kuhusiana na elimu; nishauri kwa sababu kila mtu ana akili (*everybody is genius*), lakini *if you judge a fish by its ability to climb a tree*, anaishi maisha yake yote hajui kama yeye ana akili. Kwa hiyo, naweza nikashauri hiyo kwa sababu natamani kuona tunafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naishia hapo. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ni nani anayesema Kuhusu Utaratibu, simwoni. Kanuni inayovunjwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru. Kanuni ya 70 katika mchango wa mchangiaji aliyekaa; na kwa sababu imekuwa ni utaratibu wake pia kuzungumza mambo ambayo ni ya uwongo ndani ya Bunge hili. La kwanza, jambo ambalo limevunja kanuni ni kuzungumza kwamba Ibara ya 63 ya Katiba ambayo inaelekeza kweli kwamba zitatungiwa sheria katika utekelezaji wa mipango, lakini ni vizuri akajua kwamba nchi hii inaongozwa kwa mujibu wa katiba na sheria iliyopo inayohusiana na masuala ya mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo *Finance Act*, pamoja na hayo katika utekelezaji wa kila jambo kuna sheria ambazo zinasimamia utaratibu wake; za kiwizara; na tuna *regulations* ambazo zimetungwa kwenye Wizara. Sambamba na hilo, naomba kama jambo hili amelisema na ana uhakika nalo alitolee ushahidi ili chombo kama hiki chenye heshima kubwa kisishushiwe hadhi yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunatambua wenzetu hawa pengine kwa sababu ya *election trauma* huwa kuna magonjwa ya kitaalam...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa haya ni kama *psychosomatic, stress and depression*. Kwa hiyo, unapopatwa na matatizo kama haya lazima twende nao vizuri sana wenzetu kwa sababu *psychosomatic, stress and depression* kwa maana ya msongo wa mawazo unaweza ukasababisha watu wakatoka kwenye kanuni na kuongea lugha ambazo siyo za Kibunge. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kuwasilisha hilo.

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Amesimama Mheshimiwa Patrobash Katambi kwa mujibu wa Kanuni ya 70 akisema mchangiaji aliyekuwa anachangia amevunja hiyo Kanuni kwa kusema uongo na Kanuni hii inakataza kusema uongo. Ameeleza maelezo marefu akisema Mheshimiwa Nusrat amesema uongo kwa maana ya matumizi ya Katiba, Ibara ya 63 inayoeleza kuhusu madaraka ya Bunge na mambo mbalimbali.

Waheshimiwa Wabunge, mambo mengine haya tutaendelea kujifunza, kwa hivyo, tusiwe na wasiwasi lakini ndiyo maana tunakumbushana kila wakati watu kusoma Kanuni, kuzielewa ili hapa ndani tuweze kutoa michango ile ambayo inalipeleka Taifa letu mbele. Kwa sababu tukishafika hapa siyo suala la kuvuta kamba, ni suala la kulisaidia Taifa

hili, limetuamini sisi sote humu ndani kwamba tunafaa kuwa wawakilishi wa Tanzania nzima na kufanya maamuzi kwa niaba yao. (*Makofii*)

Sasa Mheshimiwa alitaja Katiba, Ibara ya 63, nitatoa maelezo kwa kifupi kwa sababu sisi wote humu ndani tumeshaambiwa mtu ye yeyote anayeweza kusoma na kuandika anaweza kuja humu ndani.

Kwa hiyo, kila mtu akasome hizi Kanuni na Katiba ili anapoutoa mchango wake, kwa sababu maneno yote unayozungumza humu ndani ukiacha yale yanayofutwa kwa utaratibu ni kwamba yanabaki kama Taarifa Rasmi za Bunge. Mtu atakuja kusoma huko baadaye habari zako atajua humu ndani ulikuwa unazungumza nini.

Nilisimama hapa nikaeleza kabla ya kusimama mara hii, nimeeleza kwa kirefu kabisa kwamba humu ndani tuheshimiane kila mchango una umuhimu wake. Mtagundua Mheshimiwa Nusrat amemaliza mchango, yeye kama kijana, hapa kila mtu ana cha kwake alichokiona kwamba ni mchango katika kile alichokisema lakini yupo atakayetoka hapa ndani asielewe hata kazungumza nini kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Kwa hiyo, kwa muktadha huo, ndiyo maana ni muhimu kila mtu kuheshimu mchango wa mwenzake. (*Makofii*)

Sasa Katiba yetu, Ibara ya 63 ukikisoma chote lakini mimi sitasoma chote, nitaenda Ibara ndogo ya (3) inasema: "Kwa madhumuni ya utekelezaji wa mamlaka yake, Bunge laweza...". Kipengele cha (c) na (d) vinasema hivi:

"(c) Kujadili na kuidhinisha Mpango wowote wa muda mrefu au muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo.

(d) Kutunga sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kuwapo sheria".

Waheshimiwa Wabunge, kwa hivyo tukisoma haya mambo tutaelewa namna ya kuzzungumza hoja zetu. Si kila jambo litatungiwa sheria, si kila jambo! Lile linalohitaji kutungiwa sheria, Bunge litatunga sheria. Ninyi mnafahamu Mpango wa muda mrefu unatoa dira tunakoelekea kama Taifa lakini mpango wa muda mfupi unatoa dira wakati wa bajeti tutakuwa tunatenga fedha kwa ajili ya mambo gani ili kutekelea huo Mpango wetu. (*Makofi*)

Kwa hivyo, michango hii mliyoitoa, wengine mlchangia wakati wa Mpango wa muda mfupi. Mpango wa muda mfupi mtagundua katika kipindi hiki unakuja hapa kila mwaka ili kuiambia Serikali haya ndiyo mawazo yetu kayawekeni vizuri, leteni hapa kuomba fedha tuwape mkatekeleze.

Waheshimiwa Wabunge, nawaombe sana tuyasome mambo haya tuyaelewe. Ndiyo maana humu tunao watu wa kila namna, wachumi wapo watatueleza ya uchumi, wale ambao hawakujaaliwa sana na wao watatueleza ya wananchi wao, tukiyaweka yote pamoja, tunasonga mbele vizuri. Kwa hivyo, tuheshimu mawazo ya kila mtu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu utaratibu ulioomba kwamba kuna Kanuni labda imevunjwa ama vipi nieleze hivi, katika kujifunza huku tutaendelea taratibu na ninyi sio wageni kwangu, tukishafika mahali tutajua hizi Kanuni zinamaanisha nini lakini kwa leo niishie hapo, tunaendelea kujifunza. (*Makofi*)

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**WABUNGE FULANI:** Aaaa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Niliomba Kuhusu Utaratibu lakini ulivyosimama nikakaa kwa heshima. Kwa hiyo, muache ye ye afanye *ruling*, tafadhali sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko, naomba ukae.

Tunaendelea, Mheshimiwa Anna Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Mpango ulio mbele yetu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita upande wa *TARURA* kwa sababu nimeona Wabunge wengi wanaongelea kuhusu masuala ya kilimo. Asilimia kubwa katika nchi yetu ya Tanzania ni wakulima na Wabunge wengi wamesema kuwa kilimo kitatufikisha mbali zaidi kwa ajili ya kuongeza uchumi wa Watanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mifuko mbalimbali ambayo tumeshaiwека katika Bunge hill, mfano Mfuko wa Maji na tumeona jinsi gani mifuko hiyo inavyosaidia maendeleo katika nchi yetu. Naomba kupitia Mpango wetu tuenze kutafuta Mfuko wa *TARURA* kupitia mitandao yetu ya simu. Tukipata shilingi 10 katika kila *call* nafikiri tutapata hela nyingi sana ambapo tutafungua mfuko mkubwa kwa sababu kwenye mitandao yetu ya simu hatujawahi kuchukua kitu chochote kwa ajili ya maendeleo ya jambo lolote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mfuko wa Maji tunachukua kwenye petroli na dizeli, sasa hivi tuchukue kwenye mitandao ya simu kwa ajili ya *TARURA*. Wananchi wetu wakilima vizuri na barabara zetu zikawa nzuri ina maana uchumi wa nchi yetu utakuwa mkubwa zaidi kupitia wakulima na vilevile Taifa letu litaongeza kipato kupitia kilimo chetu. Naomba sana *TARURA* itafutiwe mfuko maalum kwa ajili ya kuchangia mfuko huo ili tuweze kupata manufaa kupitia barabara zetu za vijijiini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende upande wa elimu. Najua toka Awamu ya Tano ni bure. Ilivyoingia elimu bure tulianza kupata wanafunzi wengi ambapo darasa la kwanza au darasa la awali tulikuwa tunaingiza watoto 1,000 shule zingine mpaka 1,200. Tutambue kuwa lazima tuweke mpango

maalum kuanzia sasa hivi tujipange vizuri ili baada ya miaka saba inayokuja mbele yetu tuwe na madarasa mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tu unakuta darasa moja lina watoto 80, tunakuja kuanza kuhangaika na *pressure* lakini tutambue kuanzia Awamu ya Tano imeanza kuwa na watoto 1,000 darasa la kwanza ina maana mpaka sasa hivi watoto 1,000 wako darasa la sita kwa darasa moja. Sasa ni lazima tuanze kuweka mikakati ya kuelekea sekondari tuwe na madarasa mengi ili tuweze kupata manufaa zaidi na elimu ikaendelea kuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tutambue kuwa lazima sasa tuwekeze katika kutoa ajira. Tutoe ajira kwa walimu elimu ya shule za msingi na sekondari kwa sababu walimu wetu ni wachache sana na kila siku tunajenga shule za sekondari, tunajenga shule za msingi, wanafunzi wanaongezeka lakini kasi ya kuongeza walimu haipo. Naomba sana Serikali sasa hivi ijiwekeze kuanza kuweka mkakati wa ajira kwa ajili ya walimu wa kufundisha watoto wetu kwa sababu ni wachache sana na tunaendelea kufungua shule siku hadi siku, shule za kata zinafunguliwa siku hadi siku...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, kengele imegonga.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Eng. Mwanaisha Ullenge* atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea, Mheshimiwa Tumaini Magessa ajiandae.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Mpango wa Miaka Mitatu wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu kwamba Serikali yetu imewekeza kwa kiwango kikubwa katika upanuzi wa bandari zetu. Nafikiri ni maono makubwa pia ya Rais wetu kuboresha bandari zetu kwa sababu amepanua barabara ya Morogoro lakini pia amejenga na reli, yote haya ni ili kuleta ufanisi katika biashara ya bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba Serikali iweke mpango kuhakikisha ina-enforce law ili basi ile *slow moving traffic* katika barabara ya Morogoro na *fast moving traffic* zisiweze kuchanganyika pamoja ili *intended use* ya zile *fly overs* ambazo zimetengenezwa ziweze kuleta maana katika Taifa letu. Ndugu zetu wanaotumia maguta, mikokoteni ni muhimu kwa Taifa letu pia lakini haileti mantiki tuweze kutengeneza *fly over* ili *fast moving traffic* zikimbie halafu unavuka unashuka chini unakutana na guta na mkokoteni.

Naomba sheria na taratibu nzuri ziwekwe ili kuhakikisha kwamba watumiaji hawa wanatafuta namna ya kufikisha mizigo yao sokoni Kariakoo lakini sio kwa kutumia barabara ile iliyopanuliwa na inayotaka mgari yaende haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie pia kwenye suala zima la *parking lots*. Serikali imekuwa ikikusanya mapato kwa maana ya *parking fees* katika mitaa yetu wakati zile barabara zimetengenezwa kwa upana ule kwa sababu maalum. Leo sehemu ya barabara inatumika kama *parking lots*, hii inakwenda kinyume na matumizi halisi ya barabara. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali iweke mpango na kwa kuwa sasa tunakwenda kuwa na *adequate public transport*, tunazo *DART* lakini tutakuwa na treni za mjini, Serikali iweke Mpango wa kutengenza *parking* kule ambapo *DART* inaanzia ili mtu anapotoka nyumbani kwake aweze ku-park gari yake sehemu salama na aingie katikati ya Majiji yetu bila ku-congest majiji yetu kuliko kutumia maeneo ya barabara. Hii inakwenda *against* na mipango halisi ya ku-design barabara zile. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba kuchangia maana halisi ya *DART* (*Dar es Salaam Rapid Transit*) au *DORT* (*Dodoma Rapid Transit*), mana halisi ni kuhakikisha kwamba katika kila kituo chetu cha mwendokasi kunakuwa na *schedule* ya kupita kwa magari yale. Kwa maana kwamba labda gari ya kwanza itaanza saa 11, nyingine itakuwa saa 11:10 ndiyo maana ya *Rapid Transit*. Kama hatuwezi kuweka hizo *schedule* zikafahamika *Rapid Transit* hazitakuwa na maana, zitakuwa sawasawa na daladala zetu tu, hamna tofauti. Kwa hiyo, niiombe Serikali iweke Mpango wa kuhakikisha kwamba hizi tunazoiita *Rapid Transit* zinafika kwenye kituo kwa *interval* ambazo zitakuwa known kwa wananchi ili nao waweze kutoka katika nyumba zao na waweze kutumia usafiri bila kukaa muda mrefu katika vituo vyetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepanua bandari zetu na imepanua pia bandari ya Tanga lakini kiukweli *TRA* wanachangia kuhakikisha bandari ambazo ziko nje ya Dar es Salaam hazipati wateja kwa sababu *tax clearance* inachelewa. Dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu ni Mbunge wa Tanga Mjini amekuwa aki-*hustle* kutafuta wateja watumie Bandari ya Tanga baada ya kuwa imeshaongezwa kina chake lakini *unfortunately* wateja wanakimbilia Bandari ya Dar es Salaam kwa sababu *tax clearance* inachelewa bandari za mikoani.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea, atafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini Magessa, Mheshimiwa Justin Nyamoga ajiandae.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii uliyonipatia ili niweze kuchangia kwenye Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuongea mbele ya Bunge lako Tukufu, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii kuwa kati ya wawakilishi wa wananchi kwenye Bunge hili la Kumi na Mbili. Nafahamu umuhimu na ukubwa wa nafasi hii, hivyo, namuomba Mwenyezi Mungu akapate kunipa busara na hekima hasa kwa hiki kipindi changu cha miaka mitano ili niweze kuwaongoza watu wake kwa haki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata fursa ya kuusoma vizuri Mpango huu lakini kutokana na muda nimeamua ushauri wangu wote wa kitaalam niuweke kwenye maandishi hivyo baada ya hapa nitakabidhi meza yao ushauri wangu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa hizi dakika chache ulizonipatia, naomba niongee mambo machache hasa yanayohusiana na Jimbo langu la Korogwe Mjini. Nafahamu Mpango huu hasa umejikita kuimarisha uchumi kwenye Sekta ya Viwanda na Biashara. Hata hivyo, ili tuweze kufikia malengo hayo, naomba tuzingatie ushiriki wa wanawake katika uchumi wa viwanda na biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu umuhimu wa wanawake katika kukuza uchumi. Hii hata kwenye Biblia inadhihirishwa, inasema wanawake ni Jeshi kubwa. Hata hivyo, ushiriki wa wanawake kwenye sekta ya uchumi umeathiriwa sana na changamoto mbalimbali kwenye jamii zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu la Korogwe Mjini, ushiriki wa wanawake kwenye shughuli za uchumi na biashara pamoja na viwanda umeathiriwa sana na tatizo la maji. Wamama wa Korogwe badala ya kujihusisha kwenye shughuli za kiuchumi wamekuwa wakipoteza muda mwingi kutafuta maji kwa ajili ya kuhudumia familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yamekuwa changamoto kubwa ambayo imewapotezea *focus* wamama wa Korogwe hivyo kupunguza kasi ya uchumi na maendeleo ya Jimbo letu la Korogwe Mjini. Hivyo nimuombe kaka yangu Mheshimiwa Aweso aone namna gani tunatatua tatizo hili ili akina mama wa Korogwe wakape fursa ya kushiriki kwenye uchumi badala ya kuhudumia familia zao kutafuta maji usiku mzima. Kwa wastani kwenye Jimbo langu tunapata maji mara moja kwa wiki, hivyo tunaomba tuangaliwe kwa jicho la kipekee. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu pasipo afya bora ni vigumu kuweza kufikia haya maendeleo tuliyoyaainisha kwenye Mpango huu. Hivyo, kwenye sekta ya afya kwenye Jimbo langu la Korogwe pia ni changamoto kubwa. Tuna hospitali yetu moja ya wilaya ambayo tunaitegemea kwenye Jimbo letu la Korogwe, lakini sio Korogwe tu pamoja na wilaya nydingine za jirani; hospitali hii ni chakavu sana imejengwa tangu mwaka 1952 hivyo haiwezi kukidhi mahitaji ya huduma za afya kwenye jimbo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba Wizara husika ione namna gani inatutatulia changamoto hii. Aidha, tukarabatiwe hospitali ile kwa viwango vikubwa au kujengewa hospitali nydingine, ili watu wapate afya bora tuweze kukimbizana na shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba niweze kuungana na watu wengine wengi waliochangia, umuhimu wa miundombinu ya barabara katika kukuza uchumi na kuweza kufikia Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu la Korogwe Mjini tuna barabara muhimu sana, barabara hiyo inatuunganisha watu wa Korogwe Mjini, watu wa Korogwe Vijiji, pamoja na Mkinga. Barabara ambayo inatoka Korogwe – Kwa Mndolwa – Magoma, tuliahidiwa na Rais pamoja na Waziri Mkuu tutatengenezewa barabara hii, hivyo namwomba Waziri mhusika wa Wizara hii aweze kutujengea barabara hiyo ili kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tumaini Magesa, atafuatiwa na Mheshimiwa Justin Nyamoga na Mheshimiwa Shamsia Aziz Mtamba ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kunipatia nafasi ya kuongea katika Bunge hili kuchangia katika Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka Mitano na wa Mwaka Mmoja. Ni dhahiri kwamba, ukurasa wa tano umeonesha wazi kwamba, nguzo za Mpango huu wa Maendeleo zimejikita kwenye sehemu tatu; ya kwanza ni utawala bora. Utawala bora sina mashaka kwa namna ambavyo unaendeshwa sasa kwa sababu ya haki na uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguzo ya pili ni ukuaji wa uchumi; ukuaji wa uchumi tumeuona kwamba, uchumi unakua, lakini kuna mambo kadhaa ambayo tunatakiwa tuyapitie. Wabunge wengi wameeleza juu ya kilimo, ni kweli kabisa kwamba, Watanzania zaidi ya asilimia 75 wameajiriwa kwenye kilimo na bajeti tunayoipeleka kwenye kilimo ni ndogo sana. Kama hiyo *graph* ya ukuaji wa uchumi ni *linear* maana yake tunapoondo tu kuwafanya wale wasihusike katika uchangiaji wa pato la Taifa, lazima uchumi wetu utaonekana haukui haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo iko hoja tunataka kuongeza bajeti, lakini sisi tunaotoka vijijini kule watu wamezalisha mchele haujauzwa hadi leo upo, mahindi yapo yamezalishwa hayajauzwa. Maana yake kuna hoja ya masoko hapa haijaka vizuri ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ndugu zangu wanaitwa *TMX*, wameshughulika na suala hili, lakini kila mmoja ana mpunga ndani, ana mahindi ndani na biashara haifanyiki. Kwa hiyo, tunapokwenda kwenye hoja hii, lazima tutafiti tujue kwamba, tuna masoko ya kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna udongo wa kila aina mahali tunapoishi. Hii Wizara ya Kilimo inatakiwa ipewe fedha kwa ajili ya utafiti. Kuna mahali fulani niliwahi kuishi wakaniambia hapa hapahitaji mbolea udongo wake una madini mengi sana, maana yake hawana elimu ya kutosha kujua nini wanatakiwa kufanya kwenye kuzalisha. Kwa hiyo, niseme tu wazi tunahitaji kuchangia kwa kiwango kikubwa kwenye Wizara ya Kilimo, ili tuweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye ukuaji wa uchumi, ukiangalia vipaumbele kwenye ukurasa wa 101 inasema wazi kwamba, tutachochea uchumi shirikishi na shindani, lakini ukirudi kwenye ukurasa namba 64 kwenye Mpango huu, utagundua kwamba, kuna mahali fulani sekta binafsi haikuhusika vizuri kuna vitu ambavyo vilikwenda vyatichefuchefu. Ukiangalia *Clause 3(iii)*, utagundua kuna habari ya ulipaji wa kodi imeandikwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninakotoka Katoro nina wafanyabiashara zaidi ya 5,000 pale Mjini Katoro, wana ugomvi na *TRA* kuanzia asubuhi hadi jioni. Nina mashaka sasa kama tunataka kukuza uwekezaji na uchumi, hiyo ni katika kipaumbele cha tatu, inaonekana kuna tatizo katika *TRA* na wafanyabiashara, tutakuzaje sasa uwekezaji na uchumi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima sasa hivi tuanze kutengeneza kama ni ushirikishi na shindani tuhakikishe kwamba, *TRA* wanafanya urafiki na hawa wafanyabiashara wasiwakadirie vitu ambavyo havipo. *TRA* wamekuwa wanarudi nyuma miaka mitano halafu wanamwambia mtu sasa unatakiwa kulipa milioni 300; millioni 300 na yeye mtaji wake ni milioni 150, kimsingi huyu amefilisika. Kwa hiyo, niombi sana hoja yetu ya msingi ni kuhakikisha kwamba, sasa uchumi wetu unaweza ukakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona madini yatakuwa kutoka asilimia 5.2 kwenda asilimia 10. Tumeona kilimo kinatakiwa kichangie kutoka asilimia 27, bahati mbaya inaonekana mpaka baada ya miaka mitano hakitakuwa

kimechangia sana ukiangalia kwenye kumbukumbu ukurasa 104, lakini niseme tu wazi ni lazima tuhakikishe kwamba sasa hivi masoko yapo, lakini tukiendelea kuzalisha na masoko hayapo tutakuwa tumefanya mchezo wa kuigiza na uchumi wetu hautaweza kupanda kwa sababu, wananchi hawatazalisha sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Justin Nyamoga, atafuatiwa na Mheshimiwa Shamsia Aziz Mtamba na Mheshimiwa Ritta Kabati ajiandae.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii. Nimepitia Mpango huu na ningependa kuchangia kwenye mambo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu mfumo wa kodi hasa kwa wafanyabiashara wa mazao mbalimbali ya misitu na mazao ya mbogamboga. Sheria ya kodi hii inamtaka kila mfanyakibashara mwenye mzunguko unaofikia shilingi milioni 14 basi awe na mashine ya *EFD* na kwa hiyo, haikuzingatia baadhi ya vitu ambavyo vinawakwaza wafanyabiashara. Nitoe mfano kidogo kwamba, wako watu ambaa wanauza mara moja tu, kwa mfano wakulima wa miti ya mbaa anachana mbaa na anauza anaweza akapata milioni 30 na akapeleka mzigo wake au wafanyabiashara wa mazao wanaonunua kidogokidogo na mzigo unafika kwa kiwango hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna utaratibu wa mageti ambapo yule mwenye mzigo akifika pale, basi anadaiwa risiti ya mahali alikonunua. Hii inatakiwa kurekebishwa kwa sababu kwa kufanya hivyo inawataka watu wengi sana ambaa ni wakulima wa kawaida, watu wengi sana ambaa ni wafanyabiashara wa mara moja, huo mzunguko wanaupata kwa haraka na sidhani kama tuko

tayari kugawa mashine za *EFD* kwa wakulima, tuko tayari kugawa mashine za *EFD* kwa mtu anayechana mbao mara moja tu akauza. Irekebishwe ili iseme wafanyabiashara wa maduka au wafanyabiashara wenye sehemu ya kudumu kwa sababu, ndiko ilikolenga, lakini haiku-*specify* kwa hiyo, wale wa *TRA* wanapajaribu ku-*execute* wanasababisha usumbufu kwa baadhi ya wafanyabiashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kuzungumza ni ujenzi wa viwanda vya kimkakati. Juzi hapa nilitembelea kiwanda kimoja cha kutengeneza samani na kimejengwa na *VETA* kiko hapa Dodoma. Nikajiuliza sababu, iliyofanya *VETA* kujenga kiwanda hapa kwa sababu, ni cha samani; sikuona kama kuna misitu ya kutosha, kuna miti ya kutosha na hiyo ni taasisi ya umma. Ningeshauri viwanda vya kimkakati kama kile, laiti kama kingejengwa mahali kama Kilolo, Mufindi au Mafinga ambako kuna miti ya kutosha maana yake ni kwamba, hata shida ya madawati ingekuwa historia kwa sababu, kingeweza kufanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba hizi taasisi za umma, taasisi kama *VETA* na magereza ambao wanataka kuwekeza kwenye viwanda waangalie mazingira, hasa hivi viwanda vya samani. Sasa kwenye huu Mpango iangaliwe, tunaposema viwanda vya kimkakati basi vijengwe kule ambako mazao hayo yanazalishwa badala ya kuweka mahali kwa sababu ambazo huenda haziwezi kuleta tija kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni kuhusu barabara, hasa *TARURA*, ambalo limezungumzwa na watu wengi. Naunga mkono wale wanaosema kitafutwe chanzo kingine, uundwe Mfuko mwagine wa peke yake na tuangalie kwenye sekta ya mawasiliano, ili tupate fungu la kutosha, tuweze kutatua changamoto ya barabara kwa sababu, baada ya hapo hiyo ndio itakayokuwa mwarobaini wa matatizo tulionayo, ili pia *TANROADS* iweze kubakia na hela za kutosha kwenye Mfuko wake ilionao sasa, kwa sababu, kama tukigawa kwa kiwango

kikubwa tutaifilisi *TANROADS* na itashindwa kufanya kazi tutarudi hapa tena kulalamika. Kwa hiyo, Mfuko mwingine ni muhimu ili kwamba, tusiifilisi *TANROADS* na *TARURA* itafutiwe chanzo kingine ambacho kitasababisha pato la Mfuko wa *TARURA* kuwa *stable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ningependa kuzungumzia suala zima la ajira kwa vijana na kuweka mazingira wezeshi na rafiki. Watu wengi sana wanamaliza *form four* wanapata *division four* na wengine wanapata *division zero* na hao wengi hatujawawekea utaratibu wowote. Tukiendelea hivi ina maana kwenye vijiji vyetu na kwenye maeneo yetu kuna vijana wengi ambao hawajawekewa mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza vyuo hivi vya ufundi vitakapo jengwa, vyuo hivi vya katii, viangalle taaluma maalum kwenye haya maeneo. Ikiwa ni maeneo kama kule kwetu basi ufundi wa kutengeneza samani, ufundi wa aina mbalimbali, lakini pia kufundisha masuala mazima ya kilimo na aina mbalimbali za kilimo zinazolimwa kwenye maeneo husika, ili wale vijana wanaopata *division four* na wanaopata *division zero* tusiwaache bila kuweka mpango maalum kwamba, maendeleo yao ya maisha yao yatakuwaje kwa sababu ni wengi na hao watakuja kuwa watu ambao hawana kitu chochote wanacheweza kufanya. Hilo ni janga ambalo kama tusipoliangalia si jambo zuri kwa maendeleo ya Watanzania.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele imegonga, ahsante sana.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante san ana naunga mkono hoja. *(Makofii)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shamsia Aziz Mtamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Ibondo Ramadhan Abeid ajiandae.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia katika Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya nzuri na leo hii nikaweza kusimama katika Bunge hili, lakini pia nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Mtwara Vijijiini kwa heshima kubwa ambayo wamenipa na leo hii nikaweza kurudi tena katika Bunge hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, gesi inayotumika kuzalisha umeme Kinyerezi inatoka Mtwara katika Kijiji cha Msimbati, inapitia Madimba ndipo inaposafirishwa kuelekea Kinyerezi. Kwa mshangao mkubwa sana sehemu ambako inatoka gesi asilia, Msimbati, miundombinu ya barabara ni mibovu mno. Barabara ni mbovu haipitiki kabisa hasa kipindi hiki cha masika. Hivyo, niiombe Serikali katika Mpango huu wa Maendeleo irekebishe barabara hii muhimu ambayo inaleta uchumi wa Taifa, ijengwe kwa kiwango cha lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaoishi katika eneo ambalo inatoka gesi wana mazingira duni sana. Hivyo, niiombe Serikali iwaangalie wananchi hawa kwa kuwawekea mazingira ya kuwaboreshea afya bora, elimu pamoja na uchumi kiujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu wa Mtwara na Kusini kwa ujumla Mwenyezi Mungu ametujalia tuna korosho nzuri na bora kabisa, lakini pia tuna gesi asilia, lakini pia tuna bandari kubwa ambayo ina kina krefu. Kwa masikitiko makubwa sana Bandari hii ya Mtwara haifanyi kazi ipasavyo ukilinganisha na Serikali ilivyotumia pesa nydingi kuwekeza katika Bandari hii ya Mtwara; haifanyi kazi, hii inanyima maendeleo kwa Taifa na maendeleo kwa watu wa Kusini kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe ni shahidi. Nikiwa natoka Mtwara naelekea Dar-es-Salaam natumia barabara, lakini napishana na malori njiani ambayo yamebeba simenti pamoja na korosho. Mizigo hii ingeweza

kupitia katika bandari yetu ya Mtwara, lakini inatumia barabara. Hii inaleta uharibifu mkubwa wa barabara na inaipa Serikali jukumu kubwa la kuikarabati barabara hii mara kwa mara. Sasa niishauri Serikali katika Mpango huu ione umuhimu mkubwa sana wa kuitumia Bandari ya Mtwara ambayo italeta maendeleo kwa watu wa Kusini, lakini pia kwa Taifa kwa ujumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma tulikuwa tunaziona meli nyingi zikifika katika bandari yetu ya Mtwara na vijana wengi wa Mtwara waliweza kupata ajira...

*(Hapa kengele ililia)*

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuni... eeh, si nimesikia kengele?

**MWENYEKITI:** Ni kengele ya kwanza Mheshimiwa, bado ya pili.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Serikali na niishauri kwa ajili ya Taifa kwa ujumla, ione umuhimu wa kuwekeza katika Bandari hii ya Mtwara ili iweze kufanya kazi ipasavyo. Bandari hii ingeweza kupata mizigo mingi kutoka Songea, Makambako, lakini pia na sehemu nyinginezo, wangeweza kuitumia bandari hii, leo hii hali ya maisha ya watu wa Mtwara yamekuwa magumu kwelikweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi walikuwa wanajipatia ajira katika bandari hii, lakini cha kushangaza bandari hii imetupwa kabisa, imesahaulika kabisa wakati bandari hii ina kina kirefu cha kupokea meli zaidi hata ya 15 au 20. Kwa hiyo, niiombe Serikali ione umuhimu wa kuitumia bandari hii. Ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Shukrani sana. Mheshimiwa Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Igondo Ramadhan Abeid na Mheshimiwa Michael Constantine Mwakamo ajiandae.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Mpango wa Tano wa Maendeleo. Naomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia, kwanza kabisa nianze na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kupata tuzo na kushika nafasi ya pili kwa kiongozi bora wa Marais katika Afrika, akiongozwa na Rais wa Ghana. Tuzo hiyo imetolewa na *African Leadership* ambayo Makao Makuu yake yako London, kwa kweli, nani kama Magufuli? (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo niendelee kumpongeza pia Mheshimiwa Mpango kwa kutuletea Mpango wake ili tuweze kuuchangia hapa Bungeni. Pia, nimpongeze hata Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kwa kuweza kuwasilisha mpango vizuri katika Bunge letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tunaelekea kwenye uchumi wa viwanda. Katika kuelekea kwenye uchumi wa viwanda ni muhimu sana Mpango wetu ujikite kuhakikisha kwamba, barabara za kiuchumi zinapitika wakati wote, kwa sababu barabara zetu nyingi hazipitiki wakati wa mvua. Kwa hiyo, niiombe Serikali yetu ifanye upembuzi yakinifu kuhakikisha barabara zile za kiuchumi zinapitika na ikiwezekana zijengwe kwa kiwango cha lami, ili tuweze kupeleka malighafi katika viwanda yvetu. Vilevile kupunguza vifo vya akinamama na watoto katika maeneo yetu hasa ya vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano katika Mkoa wetu wa Iringa, zipo barabara za kiuchumi ambazo kwa kweli wakati wa masika hazipitiki. Mheshimiwa Kihenzile jana alikuwa anachangia na akataja baadhi pia ya maeneo ambayo hayapitiki kabisa na sasa hivi kuna malori yamekwama karibu wiki nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye baadhi ya barabara zetu za kiuchumi; kuna barabara ya Nyololo - Mtwango kama kilomita 40; ya Mafinga - Mgololo, Mafinga – Mapanda; Ipogolo – Kilolo; na Kilolo – Idete. Hizi ni baadhi tu ya barabara za kiuchumi ambazo tuna imani kabisa kama zitafanyiwa kazi vizuri pato la Taifa litaongezeka kwa sababu magari yatapita muda wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuchangia kuhusiana na mradi wa *REGROW* ambao ni mradi wa kuendeleza maliasili na kukuza utalii Kusini mwa Tanzania. Mradi huu ulikuwa unatekelezwa na fedha za World Bank na utafaidisha Mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Katavi, Rukwa pamoja na Ruvuma na Makao Makuu yake ni Iringa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuutambulisha mradi huu ulikuwepo na ulikuwa mgeni rasmi lakini hatujaona maliasili na utalii katika Mikoa yetu hii ya Kusini tunafanyaje huu utalii? Tulikuwa tuna imani kabisa huu mradi ungesaidia kuleta ajira nyingi sana kupitia utalii na pato la Mikoa yetu ya Kusini na tulitegemea tuanze mashindano kati ya Mikoa ya Kaskazini na Kusini ili tuweze kupata kipato kikubwa cha taifa kupitia miradi ya utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kujua, je, Maliasili sasa wamejipangaje? Huu mradi unaanza lini? Kabla hatujapata hizi fedha, je, wanatangaza, maana yake biashara ni matangazo, wanatangaza vivutio vilivyopo katika maeneo yetu ya Kusini? Vivutio Kusini viko vingi sana na siku ile ulishuhudia Wakuu wa Mikoa wote walieleza vivutio vizuri sana katika kila mkoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sasa Serikali ianze kutumia hata pato la ndani kabla ya kupata hizi fedha tuhakikishe tunatengeneza vivutio vyetu ili viweze kupitika tupate watalii wa ndani na wa nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono 100% Mpango huu wa Taifa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo na Mheshimiwa Kabula Enock Shitobeloo ajiandae. Mheshimiwa Ighondo?

**WABUNGE FULANI:** Hayupo.

**MWENYEKITI:** Hayupo, Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, atafuatiwa na Mheshimiwa Kabula Enock Shitobeloo na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga ajiandae.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri mwenye dhamana kwa ajili ya hotuba nzuri au mpango mzuri ambaao amewasilisha kwetu. kabla ya kupoteza muda niseme naunga mkono hoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu leo hii nimepokea taarifa kutoka kwa Mkurugenzi kwamba amekubali ombi letu. Lipo ombi maalum ambalo tuliwasilisha kwenye ofisi yake kwa ajili ya kupata eneo la uwekezaji eka 4,000 pale Kwala. Mkurugenzi amenithibitishia kwamba barua tumepokea leo na tumepata eneo hilo. Naishukuru sana Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na shukrani hiso, mimi nimejaribu kuupitia Mpango lakini pia nimesikiliza vizuri mchango wa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na namna ambavyo ameishauri Serikali juu ya kuongeza mapato yatakayoweza kusaidia ku-boost maendeleo ya nchi yetu. Kwenye maeneo hayo, yeye amejaribu kuoanisha uunganishwaji wa bandari ya Bagamoyo na matumizi ya reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kibaha vijijini lina reli mbili kubwa na ya tatu inakutana pale Mzenga; tuna reli ya kati, reli ya mwendokasi ambayo kwa wazo hili la Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kama wataitumia bandari ya Bagamoyo kwa ajili ya kwenda kwenye reli zile maana

yake lazima wataimarisha ujenzi wa barabara ya Bagamoyo – Mlandizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo na mimi niithibitishie Serikali maeneo haya ni muhimu kuendelezwa hasa ukizingatia kwamba pale Mlandizi kuna eneo la *UFC* ambalo limepimwa na Serikali viwanja kadhaa kwa ajili ya uwekezaji. Kwa hiyo, niiombe Serikali iwekeze nguvu kwenye maeneo haya kwa ajili ya kuongeza uchumi wa nchi hii kwa sababu wawekezaji watajenga viwanda katika maeneo yale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, niipongeze pia Serikali tunao mradi wa bandari kavu pale Kwala na unaenda sambamba na ujenzi wa barabara kutoka pale Vigwaza – Kwala. Katika eneo hilo hilo pia ambapo mradi huo unaendelea ndiko ambako tumepewa eneo la eka 4000 kwa ajili ya kupima viwanja vya uendelezaji. Kwa hiyo, niiombe Serikali katika miradi hii ambayo wameiruhusu kufanyika, ni vizuri tukawekeza kwa haraka kwa sababu wawekezaji wakichukua maeneo hayo watakuwa wanaongeza pato la Taifa hili na kwa kufanya hivyo nchi hii itakuwa imeongeza uchumi na huu mpango ambao umekuja mbele yetu utatekelezeka kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu kwamba Mkoa wa Pwani una viwanda vya kutosha. Katika Jimbo la Kibaha Vijiji tunavyo viwanda mbalimbali kikiwepo kiwanda kimoja ambacho kimetajwa kwenye hotuba hii cha Tan Choice. Kiwanda hiki kinashughulika na suala zima la uvunaji wa mazao ya mifugo, wanachinja ng'ombe 1,000 na mbuzi 1,000 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kiwanda kile wanakutana na changamoto mbalimbali na moja ya changamoto ni masoko. Niwaombe Serikali wawasaidie watu wale na nishukuru Waziri wa Mifugo alifika pale mwezi uliopita na aliweza kuwaona na walimpa hii changamoto. Kwa hiyo, niwaombe waweze kuwasaidia ile changamoto ambayo waliiwasilisha ili waweze kumaliza tatizo lao lile na waweze

kufanyabiashara vy a kutosha na kuingiza pesa kwenye nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo pia jambo moja ambalo nataka nilizungumzie, juzi hapa tumesikia Waziri wa TAMISEMI akiwaamuru au akiwaagiza Wakurugenzi baadhi ya vyanzo vy a mapato waendelee kukusanya, hapa nataka nijaribu kutoa uzoefu kidogo. Watendaji hawa wa Kata ambao wamerudishiwa kazi hii ya kukusanya mapato ni watendaji ambao wana kazi nydingi kweli kweli.

Kwa hiyo, kwa kuwaamini wao kuendelea kufanya na kazi ya ukusanyaji wa mapato tunaendelea kupoteza mapato kwa sababu wanaogopa kuifanya kazi hii na wengi wanadaiwa na wengine wana kesi mbalimbali mahakamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali kwenye eneo hili, badala ya kuwalundikia mzigo Watendaji wa Kata kukusanya mapato haya hasa kodi za majengo, ardhi, mabango na mambo mengine, ni vizuri sana kama ambavyo wamechangia Wabunge wenzangu tungeweza kutafuta wataalamu maalum wanaoweza kusimamia ukusanyaji wa mapato, tukaiondoa kazi hii mikononi mwa Watendaji wa Kata ili waweze kuzifanya kazi hizo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu gani watendaji hawa wamekuwa woga sana sasa hivi kwa sababu wana kesi mbalimbali zinawakabili juu ya ukusanyaji huu. Kwa hiyo, wanaweza wakategea wasiifanye kazi hii na mapato haya yasipatikane.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyoo ningeomba...

**MWENYEKITI:** Kengele imegonga Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelu atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo ajiandae.

**MHE. KABULA E. SHITOBELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii ya kuchangia katika Mpango huu wa Maendeleo ya Taifa. Pia napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake kwa kunijaalia afya njema hata nimesimama katika Bunge hili na kuchangia hoja hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma Mapendekezo ya Mpango ni mazuri sana na yana faida kubwa kwa Watanzania wote. Nami nitajikita zaidi katika hoja ya kukuza na kuchangia uchumi wetu kupitia zao la parachichi. *Nina-declare interest* nami ni mdau katika biashara ya parachichi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya parachichi ni kubwa sana na ni zao ambalo linaweza kutuletea kipato kikubwa hasa kutuletea pesa nyngi za kigeni kama tukilizingatia na kama Serikali hii itaweza kuliona ni zao bora kabisa la biashara kama mazao mengine kama korosho, pamba au kahawa. Zao hili likisimamiwa vizuri linaweza kutukuzia uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao hili limekuwa likilimwa na wakulima wadogo wadogo lakini kama likiwekewa mkakati, likatangazwa na wananchi wote wakahimizwa hasa wa Mikoa ya Njombe, Kilolo (Iringa) na Mbeya (Tukuyu) ambapo zao hili linapatikana kwa wingi na ni zao bora kabisa tutaweza kukuza uchumi wa Taifa. Zao hili mpaka sasa limeajiri wanawake wengi sana katika viwanda vya ku-process wakati matunda haya yakipelekwa nje ya nchi. Wanawake wengi ndiyo wanatumika ku-process zao lile mpaka kusafirishwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijikite kuzungumzia changamoto ya zao hili. Kama mimi nikiwa mdau nimeweza kuona changamoto mbalimbali hasa kwenye kusafirisha tunda hili. Matatizo yenewe ni jinsi ya kusafirisha mazao haya kutoka Njombe kwenda nchi kama Europe kwa sababu zao hili linauzika zaidi Europe pia *Middle East* hapa Dubai na Arabuni yote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo liliopo kwa sasa ni usafiri hasa kwenye kontena aina ya *CL*. Kwa Tanzania katika bandari yetu ya Dar es Salaam hakuna kontena kama hizo, inabidi mfanyabiashara wa zao hili aweke *booking* Nairobi, kontena litoke Mombasa lije mpaka Njombe, likifika Njombe ndio upakie ule mzigo urudi tena Mombasa ndio uweze kuondoka. Sasa tatizo linakuja wapi? Pale inapotokea tatizo lolote au *delay* yoyote njiani na mkulima au mfanyabiashara anakuwa ameshachukua matunda yako pale kwenye *park house*, sasa inapochelewa labda siku moja au siku mbili yale matunda yakija kusafirishwa kufika sehemu husika tayari yanakuwa ni *reject*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu Tukufu iangalie jinsi gani itatusaidia au itawasaidia wakulima na wafanyabiashara wa zao hili kuhakikisha kuna zile kontena za *CL* au *facility* za usafiri madhubuti pale Dar es Salaam ili *at least* mkulima tunda linaposafirishwa kufika kule Ulaya liwe katika hadhi na ubora wa Kimataifa. Ombi langu sasa kwa Serikali ni kuangalia hivyo vitu muhimu hasa upande wa makontena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ningeomba zao hili lihamasishwe sehemu mbalimbali, najua hata Bukoba au Ngara linakubali kabisa...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele imeshagonga. (*Makof*)

Mheshimiwa Nicodemus Maganga atafuatiwa na Mheshimiwa Dennis Londo na Mheshimiwa Mohammed Maulid Ali ajiandae.

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa mara ya pili nimesimama mbele ya Bunge hili Tukufu kutumia nafasi hii kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nitumie neno ku-*declare interest*, mambo yote toka tumeanza kujadili Mpango binafsi nimeuelewa vizuri sana. Niwaombe tu Wabunge wenzangu wote ni vyema tumtangulize Mungu tunapokuwa tunaishauri Serikali tusiishie tu kulalamika sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ni mdogo sana, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja, mimi ni mkulima, mfanyakabiashara pia ni mwanasiasa, naomba kwenye upande wa kilimo niishauri Serikali, ni vyema sasa wakulima tupatiwe vifaa vya kilimo kama matrekta, mimi natokea Wilaya ya wakulima pale Mbogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kwenye upande wa biashara, wafanyakabiashara tumekuwa na kilio kikubwa kwenye hili taifa la Tanzania. Mimi nilikuwa mionganoni mwa wafanyakabiashara *East Africa Community* lakini Watanzania tumefeli kufanya biashara na mataifa mengine. Kwa maana hiyo hii ajenda ni vyema Serikali iichukue kwa mapana na marefu sana, tumeshindwa yaani kila kona tumefeli, masoko yote sisi tunaonekana tuko chini. Chanzo kikubwa kabisa ni haya mabenki yetu ya ndani. Benki za hapa Tanzania riba zake ziko juu sana, ni tofauti na mabenki mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea suala la uchumi lina mapana na marefu sana. Mimi somo langu lilikuwa ni moja tu shuleni, ni uchumi peke yake. Kwa hiyo, tunapokuwa tunaongelea neno uchumi, kwanza uchumi umelenga sana sana kwenye mafuta, mimi nauza mafuta

ya *petrol*/*diesel*, tukiangalia vizuri Serikali kwenye upande wa mafuta na tukiangalia mataifa mengine yanayotuzunguka bei ya mafuta ni ya chini sana. Kwa maana hiyo Serikali ikitibu kwenye tozo hizo za mafuta zikiwemo faini za *EWURA* milioni 20 kila kosa moja, tutasonga mbele sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Geita ni wachimbaji, kwa kuwa Serikali inatuhakikishia kwamba imekusanya vya kutosha watupe vifaa vya kuchimbibia. Sisi tuna elimu kubwa ya uchimbaji ila hatuna *capital*. Serikali ikituwezesha ikatupa vifaa vya kuchimba wenyewe na sisi tutaishi kwa raha na amani kwenye nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande mwingine ni elimu, kuna dada yangu pale alizungumza *point* sana, naomba nimuunge mkono, elimu yetu ya Kitanzania inamuandaa mtu kuwa maskini, tunaandaliwa kuwa waajiriwa. Leo Wabunge wote humu tukiangaliana mfukoni tumetumwa na watu wetu kuja kuwatafutia ajira. Kwa maoni yangu ninavyoona kabisa ajira karibia zote zimejaa, kwa hiyo, ni vema walimu wawe wakweli kuanzia kule shulenii. Nimpongeze Waziri wa Elimu kuna siku moja alitangaza kwamba atapima uelewa maana suala la vyeti walikagua watumishi wote ila kwenye uelewa hapo na mimi bado nafikiria sijui atatumia taaluma ipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kubwa kabisa linalotufanya kurudi nyuma kwenye hili Taifa letu la Tanzania ni kule kutokujituma katika kazi. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu pamoja na ndugu zangu wote mnaonisikia, tunao ugonjwa Tanzania hapa wa kutokufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu amekuwa ni jemedari mkuu akituhamasisha tufanye kazi. Tatizo kubwa sisi ni wepesi wa kuridhika, tukipata tu hizi posho kidogo na mishahara hii ya Kibunge tunazziacha kazi za msingi za kuweza kutuingizia maarifa na kutuzalishia mali nyingi. Kwa hiyo, niwaombe Wabunge wenzangu sisi ni vyema tukawe kielelezo kwenye jamii tukafanye kazi hata hivi viwanda

tunavyovisema na kilimo tukaanze sisi Wabunge kulima ili Taifa letu liweze kupata manufaa. Hata maandiko yanasema sisi viongozi ni barua tunasomwa na watu wote. Kwa maana hiyo tukifanya vizuri kanzia sisi Wabunge na wale tunaowaongoza watatufuata.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele imegonga.

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ila muda haujatosha, nitaleta mchango wangu kwa maandishi, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Sawa, ahsante sana. Mheshimiwa Dennis Londo atafuatiwa na Mheshimiwa Mohammed Maulid Ali na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle ajiandae.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine nishukuru kitit chako kwa kunipa nafasi hii ya kuzungumza mbele ya Bunge lako Tukufu likiwa limeketi kama kamati. Kimsingi kwa sababu muda hautoshi, naomba nijielekeze zaidi kwenye sekta ya utalii. Sekta ya Utalii katika nchi yetu bado hatujaitendea haki, kwa sababu pamoja na kwamba tuna vivutio vingi vya asili, lakini bado tumeshindwa kuhakikisha kwamba sehemu kubwa ya vijana wetu hasa ambaao wanaweza wakaenda kwenye elimu ya kati ama vyuo vyetu vya VETA wakapata elimu ambayo inaweza kuwasaidia kujikita katika tasnia ya utalii na kujajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nimepata nafasi ama bahati ya kuishi kwenye nchi mbalimbali zinazotegemea sana utalii. Gharama ya utalii kwetu ni kubwa mno na hata tafiti zinaonesha kwamba kati ya watalii mia moja ambaao wanatembelea Tanzania ni 20 tu ambaao wanarudi. Idadi hii ndogo mno, ni lazima sasa kama Serikali tujikite kutafuta sababu kwa nini watalii hawa mia hawarudi wote ama

hawawi mabalozi kwa wengine kwa ajili ya kuvutia vivutio vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo naomba kujikita ni eneo la kilimo; tumekuwa na *slogan* nyingi; kilimo kwanza, kilimo uti wa mgongo, lakini kimsingi Mtanzania hahitaji hizi kauli mbiu, kilimo kwake ndio kila kitu, amezaliwa anategemea kilimo, amesomeshwa na kilimo, anaishi kwa kilimo, haitaji mtu kumpa kauli mbiu, anahitaji mazingira rafiki ya ye ye kujikita kwenye kilimo. Mazingira ambayo tumemwekeea sasa hivi si rafiki. Naomba nitumie mfano wa wakulima wa miwa katika Bonde la Kilombero, nilizungumza mwanzo kwamba kati ya tani 900,000 ambazo mkulima wa miwa anazalisha pale Kilombero, ni tani 600,000 tu ambazo zinaweza kununuliwa na kiwanda pekee cha llovo, tani 300,000 zinaharibikia mashambani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira hayo bado tunasema miwa ni zao la kimkakati, lakini ni zao la kimkakati hakuna mazingira wezeshi ya kuhakikisha kwamba mkulima wa miwa ana soko la uhakika. Matokeo yake sasa hivi watu wamekata tamaa, pendekezo langu naomba Serikali iwe inaagiza sukari kwa sababu jukumu la kuagiza *deficit* anaachiwa mzalishaji ambaye ndiye mwenye jukumu la kuhakikisha ananunua miwa ya kulima; na kwa kuwa sukari ya kuagiza ni bei rahisi ukilinganisha na sukari ya kuzalisha; mzalishaji huyo wa sukari badala ya kum-*encourage* mkulima kuzalisha amekuwa kikwazo kwake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba Serikali ihakikishe kwamba inaenda kumsimamia llovo kukamilisha upanuzi wa kiwanda ili kuhakikisha kwamba mkulima ana soko la uhakika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kengele imegonga.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mohammed Maulid Ali atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, tutamalizia na Mheshimiwa Alexander Mnyeti.

**MHE. MOHAMMED MAULID ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kwa mara ya kwanza kabisa niweze kuongea kwenye Bunge lako Tukufu. Kwanza kabisa naomba niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki, pamoja na Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuniwezesha na kuniamini kuwa Mbunge katika jumbe hilo ili niweze kuwatumikia wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika hili utajikita katika mambo matatu; kwanza kilimo, pili viwanda na tatu barabara. Imeelezwa hapa kwamba zaidi ya asilimia 66 ya Watanzania wanategemea kuendesha maisha yao ya kila siku kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, imeelezwa vilevile katika Mpango huu kwamba kiasi cha viwanda 8,477 vimeanzishwa ili kuchochea ajira kadhaa zilizokusudiwa katika nchi. Mchango wangu upo kwenye suala la tatu la barabara. Mambo haya matatu yaani barabara, kilimo na viwanda vinakwenda sambamba, kama kimoja kikiwa kimetetereka vingine viwili havitakwenda sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zetu vijijini haziko katika hali nzuri, wasiwasi wangu sijui kama viwanda hivi vitafanya kazi vizuri wakati malighafi au *raw materials* zinatoka vijijini.

Kwa hiyo, basi niungane na Wabunge wengine waliochangia kwamba *TARURA* iongezwe fedha ili na wao waweze kuzitengeneza barabara hizi ili huu mzunguko ambaao tunauzungumzia hapa uweze kuwa vizuri, *otherwise* viwanda hivi vitashindwa kufanya kazi kama tulivyotoka huko nyuma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani mchango wangu kwa leo ni huo tu. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, tutamalizia na Mheshimiwa Alexander Mnyeti.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Mpango huu wa Miaka Mitano wa Serikali. Niende moja kwa moja kwenye Mpango ambao umewasilishwa na Serikali. Kwanza nipongeze sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kuwasilisha Mpango huu kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ameuwasilisha vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma Mpango huu mzima Mpango wetu ni mzuri sana na umeweke vipaumbele vyote vizuri. Na uksoma kwenye ukurasa wa 88 wa mapendeleko ya Mpango huu wa Miaka Mitano, Serikali imetamka wazi kwamba sekta ya kilimo itaendelea kuwa kitovu cha ukuzaji wa viwanda na maisha ya watu. Huu ni ukweli ambao Wabunge wote humu ndani tunaujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mchango ufuatao kuhusu sekta ya kilimo; wakati fulani ukitazama takwimu za Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Nchi yetu, utakuta kwamba kwenye kilimo zilipelekwa fedha bilioni 188 tu. Sasa kama kilimo ndio kitovu cha kukuza viwanda, unaweza kuona ule msemo ambao alikuwa anasema Rais wetu wa Nne, kwamba *zilongwa mbali, zitendwa mbali*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi? Ukitazama kwenye sekta ya kilimo, iko mipango mizuri imewekwa hapa kwamba Serikali itaboresha suala la utafiti mbegu bora, Maafisa Ugani na kadhalika. Naishauri Serikali kwa sababu maeneo mengi ya kilimo ambapo mazao ya kimkakati kama kahawa, chai, korosho, pamba na mazao mengine, haya maeneo hatuwezi kuweka kipaumbele cha kupeleka mbegu bora na wataalam na utafiti wakati miundombinu yake haiwezeshi kilimo kile kuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali kwenye maeneo ambayo kuna mazao ya kimkakati, Mpango huu ubainishe kwamba yatapewa kipaumbele cha miundombinu kama ya barabara, miundombinu ya umeme, miundombinu ya afya, ili kusudi kama unasema Jimbo la Lupembe kwa mfano lina zao la mkakati ambalo ni chai na eneo hili linalo viwanda, lakini wakati huo huo kwenye eneo hilo barabara hazipitiki, umeme hakuna, maji hakuna, Mpango huu hauwezi kufanikiwa. Ushauri wangu ulikuwa ni huo kwamba Mpango huu uendane na maeneo ya vipaumbele ili kusudi uakisi uhalisia wa mpango wenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ambayo napenda kuchangia kwa ufupi, lipo jambo limesemwa na Wabunge wengi humu ndani, Wabunge wengi tumetoa maoni kwamba Serikali haina fedha na Wabunge wamependekeza njia mbalimbali za kupata fedha. Nataka niseme eneo lingine ambalo wengi hatujalisema shida yetu kwenye utekelezaji wa hii Mipango ya Serikali kwa maoni yangu siyo fedha tu, lipo tatizo lingine la kutofanya maamuzi kwa wakati kwa watu wenyewe mamlaka ya kufanya maamuzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwa mfano, yuko Mbunge mwenzangu wa Njombe Mjini amezungumza hapa, kwa mfano yupo mwekezaji wa zao la chai ambaye yeye anashindwa kuendesha kiwanda kwa sababu tu watu wa Hazina wanashindwa kufanya maamuzi wa jinsi yeye aweze kusamehewa kodi na kuendesha biashara yake ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo pia mengine, mfano eneo kama la Kilolo, kuna mashamba ya chai yametelekezwa ni mapori, kwa sababu tu maamuzi hayajafanyika ni nani akawekeze maeneo haya. Kwa hiyo, naomba sana watu wa Serikali wafanye maamuzi, *decision making* ni kipaumbele muhimu sana kwa utekelezaji wa Mpango huu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alexander Mnyeti.

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Pia nitumie nafasi hii kuwashukuru Wanamisungwi kwa kunipitisha bila kupingwa na Madiwani wangu wote 27 na hatimaye sasa tupo humu kwa ajili ya kuwatumikia Wanamisungwi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamesemwa, mchango wangu nitajikita kwenye mambo matatu, jambo la kwanza ni kweli kwamba Taifa letu msingi wake mkubwa ni kilimo na kwa sababu hiyo tuna kila sababu ya kuelekeza nguvu kubwa kwenye kilimo tuwasaidie wakulima wetu hawa ili waweze kuleta tija kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mashamba makubwa ambayo Serikali iliwapa wawekezaji ili wayaendeleze, lakini kwa masikitiko makubwa mashamba hayo mengi yametelekezwa na hao wawekezaji na hakuna kinachoendelea. Sasa niombe Wizara ya Ardhi, kama kuna namna yoyote ya kufanya mashamba hayo ama yarudi kwa wawekezaji wengine ama yarudi kwa wananchi ili wananchi waweze kuzalisha. Mashamba hayo wawekezaji unakuta mwekezaji mmoja anamiliki mashamba ekari 20,000, wengine ekari 50,000, wengine hivi, lakini ukiangalia uendelezaji wa mashamba hayo ni asilimia nne hadi 10, eneo lingine liliobaki lote liko wazi halilimwi na wananchi wanashangaa Serikali inashangaa na mwekezaji anashangaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama kweli lengo letu ni kuzuia kuagiza vitu nje ya nchi, hebu basi tutengeneze mazingira ya kuzalisha hayo mashamba yafanye kazi ili basi tuongeze pato la Taifa kwa namna hiyo, vinginevyo tutaendelea kuagiza choroko, ngono, nyanya, vitunguu, kila kitu tunaagiza kutoka nje lakini mashamba tunayo hayafanyiwi kazi. Ukienda kule Bassutu kuna mashamba ngano, tunasema tunaagiza ngano, wakati mashamba tunayo lakini hakuna anayeyalima. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tuko *serious* na hii mipango, *otherwise* mipango ya kwenye karatasi kama kweli tunataka tutoke hapa tulipo, yako mambo makubwa ambayo tunatakiwa tuchukue hatua ili basi tuweze kutoka hapa tulipokwama. Mashamba yametekelezwa, nenda Lotiana mashamba makubwa yametekelezwa. Leo Tanzania bado tunaagiza nyama kutoka nje ya nchi. Hii mipango, ni kweli ni mipango mizuri lakini utekelezaji wake mbona tunakwama, mashamba yametekelezwa, hatuendi kwenye kugota kwenye pointi ya kwamba tunatokaje kwenye hili tatizo lilitokwamisha, haya makaratasi ni mazuri kwa sababu yameandikwa na *Professors*, ma-*PhD holder* lakini utekelezaji wake. Nazungumza utekelezaji wa namna gani tunakwama hapo tulipokwamia. Kwa hiyo, naomba hili niishauri sana Serikali kama kweli tuko *serious* hebu mtoke hapa tulipokwama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tumeanzisha viwanda vingi sana kwenye Taifa letu kwa muda mfupi, hongera sana Serikali kwa kazi hii nzuri. Hata hivyo, nasikitika kukujulisha kwamba viwanda hivi baada ya muda vitakufa vyote, kwa sababu hatuna malighafi yakuendesha hivyo viwanda, tunazalisha wapi? Unaniambia tunaanzisha viwanda ni kweli kule Iringa viwanda vya kuchakata mbao, lakini viwanda hivi miti iko wapi? Miti iko wapi, viwanda vinaanzishwa kule Misungwi, vinaanzishwa Kahama, vinaanzishwa wapi vya kuchakata pamba, pamba iko wapi? Tuwahamasishhe wakulima wetu walime, tuwawezeshe pembejeo za kilimo walime. Hii Habari ya kumfurahisha mkuu wa nchi kwamba tunaanzisha viwanda, halafu baada ya miaka sita vimekufa, hii nataka niseme tutashindwa na tunashindwa *very soon* kwa sababu hatuwahamasishi wananchi kulima, hatuwatengenezei mazingira mazuri wananchi wetu waweze kulima, waweze kupatiwa pembejeo za kilimo, matrekta na kila kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kiwanda chetu cha mbolea; leo mbolea tunanunua 60,000 mpaka 55,000 kwa mfuko wa kilo 25 mpaka 50. Sasa tuna Kiwanda chetu kule Minjingu, kiwanda peke kwenye Taifa letu, lakini Serikali ni

kama wamekipuuza, bado wanaagiza mbolea nje ya nchi, inafika mbolea hapa kwa 50,000 mpaka 60,000, lakini kile kiwanda kipo, Serikali ikikiwezesha kidogo tunaweza tukanunua mbolea 20,000 mpaka 15,000 kwa sababu tuna uwezo wa kutengeneza mbolea yetu wenyewe kwenye Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nataka niwaambie....

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele imeshagonga.

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Shukrani sana. Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Mipango kwa sasa imekamilisha kazi zake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.53 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 11 Februari, 2021, Saa Tatu Asubuhi)*